ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais
11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake

16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali
23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole
35.Mhe. Omar Ali Shehe	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni
47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba

57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka
67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Saba – Tarehe 1 April, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Ali Mzee Ali) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa mwaka 2010. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji (Mwenyekiti wa Kamati ya PAC): Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC) kwa mwaka 2009/2010. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 4

Ngoma na Kamari katika Viwanja vya Sikukuu

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Katika kusherehekea sikukuu ya Eid el Hajj iliyopita Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi iliwataka wafanyabiashara wanaoendesha michezo na burudani katika viwanja vya sikukuu kuacha kupiga ngoma za rusha roho na kutokuchezesha michezo ya kamari. Aidha, waliruhusiwa kupiga ngoma za asili kama vile mbwa kachoka, kidumbaki na kadhalika, na kumaliza shughuli zote ifikapo saa nne usiku. Hatua hiyo ya Serikali ni ya kupongezwa.

(a) Mhe. Waziri, ili kupunguza zaidi matendo maovu katika jamii. Kwa nini Serikali isipige marufuku shughuli kama hizo zinazoendeshwa katika vilabu vya pombe hasa katika maeneo ya miji.

(b) Ni tofauti gani ya madhara yapatikanayo katika ngoma za asili na zile za kisasa za rusha roho.

(c) Hatua hiyo ya Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi ilifanikiwa kiasi gani.

(d) Kama zoezi hilo limefanikiwa vizuri. Kwa nini Halmashauri nyengine, Mabaraza ya Miji na Manispaa ya Mji wa Zanzibar zisifuate mfano huo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Serikali kwa kupitia Baraza la Sanaa haitoi vibali vya kupiga muziki wa *disco* na rusha roho katika baa zilizomo katika maeneo ya watu. Baraza la Sanaa linatoa vibali vya kupiga muziki katika zile kumbi maalum tu *(Sound Proof Halls)* zilizojengwa kwa ajili ya kupiga muziki huo.

(b) Tofauti za madhara zilizopo ni kuwa ngoma za asili huwa zinalinda na kuenzi mila, silka na utamaduni wa Mzanzibari, wakati zile za *disco* na rusharoho huwa zinapotosha.

(c) Hatua hiyo ya Serikali kupiga marufuku upigaji wa *disco* na rusharoho katika viwanja vya sikukuu imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwani uvunjaji wa sheria ulipungua sana, watoto wadogo walirejea nyumbani mapema; kesi za unyanyasaji kijinsia hasa kwa watoto wanawari zimepungua kwa kiasi kikubwa. Vitendo vya uhalifu na uporaji navyo vimepungua kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba ngoma za disco haziendi sambamba na utamaduni wa Mzanzibari. Je, serikali itakuwa tayari kupiga marufuku.

Swali (b) kwa kuwa moja kati ya sherehe muhimu za sikukuu ni kuwafanya watu watembeleane. Sasa Mhe. Waziri atatunga kanuni kwamba badala ya kwenda viwanja vya kupiga ngoma watu waanze kutembeleana kuliko kupiga ngoma.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ngoma na *disco* pamoja na serikali iweze kupiga marufuku, pia kutembeleana ndio ninajiuliza wakishakutembeleana kutakuwa na kitu gani. Maana kila ninavyotaka kulizungumza halitoki hili neno. Kawaida ya sikukuu yetu watoto wetu wanakwenda viwanjani wananunua pipi, muhogo wa kuchoma wanakula wanacheza.

Sasa iwe hiyo haipo sikukuu imeshamalizika lakini watu wawe wanatembeleana. Nafikiri tungeshauriana zaidi kupata utaratibu ambao kusema kweli utatuwezesha watoto wetu waishi katika hali ya usalama na furaha. Kama ndio lazima kutembeleana basi uwekwe utaratibu kutembeleana wapi, kuanzia saa ngapi mpaka saa ngapi. *(Kicheko)*

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, mantiki nzima ya swali na jinsi Mhe. Waziri alivyojibu ni kuenzi mila, silka na utamaduni wa Mzanzibari.

Kwa kuwa yote haya yaliyozungumzwa hapa yanaambatana na mambo ambayo hayafai kiutamaduni wetu. Je, kile kivazi ambacho watu sasa hivi wanakwenda uchi kabisa Mhe. Waziri hakukiona. Kama kakiona hatua gani zinachukuliwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nasikitika kusema kwamba kivazi hicho mimi sijakiona. Lakini hata hivyo niko tayari kushirikiana na Mhe. Zakiya Omar Juma ili tuangalie kivazi anachokusudia ni kipi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Zakiya Omar Juma utashirikiana na Mhe. Waziri kuhusu kivazi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa siku ile ya sikukuu ni siku tukufu na sisi maadili yetu ya kiislam yanatuhimiza mambo matukufu. Kwa sababu ngoma, disco na rusharoho hayafai yote. Je, Mhe. Waziri haoni bora siku hiyo tukawa tunamsifu Mtume Muhammad (SAW) kwa mauled na kusoma kurani kutwa nzima na siku ya pili yake.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ukweli kusherehekea sikukuu ni juu ya wananchi wenyewe watachagua watasherehekea vipi. Sisi wajibu wetu kutazama tu je, hizi sikukuu zinavyoendeshwa zinalinda silka zetu. Kama zinalinda tuwaachie wafurahi watoto kwa sababu karibu mwezi mzima mtu alikuwa anafunga kwa hivyo mwezi umeshaandama afurahi.

Mhe. Mwenyekiti, ningeshauri kwamba bado kama tunahisi utaratibu huu unapotosha basi tungekaa tukaangalia utaratibu gani tuufanye ili tuweze kuwaongoza hawa vijana wetu. Kwa sababu utaratibu wa hizi sikukuu za aina hii ni miaka mingi sana unatumika huu, sasa kama tunataka kuuondosha ni vizuri basi tushirikiane.

Nam. 56

Matatizo ya Maji na Dakhalia Chuo cha Fedha Chwaka

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 94

Hatua za Kupambana na Upotevu wa Fedha

Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi - Aliuliza:-

(a) Kwa kuwa tatizo la upotevu wa fedha katika taasisi za Serikali limekuwa kubwa katika miaka ya karibuni, Serikali imechukua hatua gani za dharura na za kuendelea ili kupambana na upotevu wa aina hiyo.

(b) Hatua hizo zimepata mafanikio gani na zimepambana na vikwazo gani.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) (MBLM) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 94 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi katika Idara yake ya Mhasibu Mkuu wa Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbali mbali za kukumbushana katika masuala ya udhibiti na usalama wa fedha za Serikali kwa nia ya kuondosha kasoro zilizopo, ila inaonekana bado sheria na taratibu zilizopo hazizingatiwi na kufuatwa ipasavyo. Kama nilivyosema nafikiri wiki iliyopita nilipokuwa nikijibu swali kama hili.

(a) Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo Wizara ya Fedha imenunua makasha makubwa na madogo *(safe and strong boxes)* na hutolewa bure pale Taasisi inapotoa taarifa ya kwamba inahitajia. Si rahisi kwa Afisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kujua kwamba Taasisi inahitaji au ina hitilafu katika afisi yake bila ya kuripotiwa. Afisi hii huwa inashirikiana na Taasisi husika pale panapohitajika kupatiwa ufumbuzi kwa kasoro iliyopo katika usalama na uhifadhi wa fedha za Umma.

(b) Taratibu za uhifadhi na usalama wa Fedha za Umma unafahamika ila unavunjwa kwa makusudi kwa baadhi ya maeneo kwa malengo ya kufanyika kwa wizi. Wizara ya Fedha na Uchumi kupitia Afisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ipo tayari saa zote kushirikiana na Taasisi yoyote yenye upungufu katika suala zima la uhifadhi wa fedha za Serikali, kinachotakiwa kutolewa kwa taarifa iwapo kuna hitilafu katika afisi yenye kuhifadhia fedha za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naahidi mbele ya Baraza lako tukufu kwamba tutaendelea kutoa huduma zinazohitajika katika kuhakikisha kwamba kuna usalama wa vyumba, makasha na sehemu za kuhifadhia fedha za serikali kwa kushirikiana na taasisi husika ambapo ni muhimu kutoa taarifa zenye kuonesha kuwepo na kasoro au hitilafu zinazoweza kusababisha fedha za serikali kuibwa.

Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakubaliana nami kwamba badala ya kusubiri wapelekewe taarifa na taasisi husika, basi wakaandaa utaratibu maalum ofisi yake kupita na kukagua katika afisi hizo ili kuona kwamba vile vigezo vinavyotakiwa hasa katika uhifadhi wa fedha za serikali vimefikiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) (MBLM) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, ushauri alioutoa mzuri na tutaufanyia kazi.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, matatizo ya upotevu wa fedha za serikali yapo ya namna mbili, kuna yale yanayotokana na uhifadhi na kuna yale yanayotokana na udokozi. Kwa sababu taarifa za upotevu wa fedha za serikali mara nyingi hutolewa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuthibitishwa na kuripotiwa na Kamati ya *PAC* ya Baraza lako tukufu.

Je, Wizara ya Fedha ambayo ndio yenye jukumu la kufuatilia taarifa ya *PAC*. Ni mara ngapi imewawajibisha watendaji ambao wanahusika na upotevu wa mali ya serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) (MBLM) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimuongezee tu Mhe. Said Ali Mbarouk ile aliyosema kwamba moja mpaka Afisi ya *PAC* iweze kugundua, hiyo ni aina moja ya *revelation* ya hilo tatizo. Lakini moja ni kuvunjwa hasa. Kuna afisi za wahasibu unakwenda asubuhi kumevunjwa mageti, milango au nyengine hata hakuvunjwi. Sasa nafikiri hiyo kidogo Mhe. Said kaisahau, lakini hiyo ndio mara nyingi inayotokezea.

Sasa kesi kama hizo sisi mara nyingi moja kwa moja tunawaachia vyombo vya Polisi na Mahakama. Wanakwenda wenyewe Polisi wanafanya uchunguzi wao na hatimaye wanachukua hatua za kuwadhibiti wahusika kusaidia kutoa ushahidi na kama ikiyumkinika kuwafikisha Mahakamani wahusika.

Lakini hizi habari zinazotolewa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hizo mara nyingi zikiletwa basi Afisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali inazifanyia kazi kwanza kwa kuchunguza lile suala lenyewe na kuthibitisha. Ikitoka ithibati hatua ya kwanza ni kama nilivyosema nafikiri sote tunaifuatilia vizuri Sheria Nam. 5 ile ya Fedha ambapo zimetolewa taratibu zote mle na kila kosa lifanywe kosa gani.

Lakini kubwa haraka sana yule mhasibu mhusika anasimamishwa kazi *pending* uchunguzi zaidi na ikiyumkinika anafikishwa Mahakamani na taratibu za kisheria zinachukuliwa.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika shughuli ya upotevu wa fedha huwa pia kunahusishwa na uibiwaji wa mishahara katika taasisi mbali mbali.

Kwa mfano, katika mwaka 2007/2008 mishahara iliibiwa katika Kikosi cha Valantia yenye thamani ya shilingi 23,240, 000/=. Kwa sababu upotevu huu wa mishahara hauwahusishi wale ambao walipaswa kulipwa mishahara ile, lakini baada ya kuibiwa mishahara hiyo wafanyakazi wale hadi hii leo hawajalipwa mishahara yao. Je, serikali inasemaje kuhusu suala hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) (MBLM) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri lazima tukubaliane kuna mambo mawili hapa. Serikali imetimiza wajibu wake pesa imelipa zikatoka *cashier* akenda akachukua benki, zimefika mpaka tayari hizi walipwe. Sasa aliyefanya kosa si serikali hapo, aliyefanya kosa huyo mhusika.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema wacha kwenda Mahakamani au Polisi wanafanya uchunguzi wao, Mahakama itaamua nini kifanywe. Sio kwamba leo kumeibiwa fedha serikali itoe nyengine ikalipe, nafikiri Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji si jambo jema hilo. Tuwaachie kwanza wenyewe wenye taratibu za sheria wanasemaje.

Sasa wajibu wetu tumekwenda kwenye sheria na wao wataelekeza kifanywe nini. Sifikiri *immediately* kwamba siku ya pili tu zimeibiwa zile uwaambie serikali itoe nyengine, nafikiri *is unfair*. Wacha tuone kwanza vyombo hivi vya taratibu za kiserikali vya Mahakama na Polisi wanasemaje. Pengine hukumu itakuwa yule ni mzembe alipe, hata kama milioni 20 atakatwa kidogo kidogo mpaka zipatikane.

Nam. 67

Hatari ya Kutoweka Kilimo cha Mwani

Mhe. Ali Abdalla Ali - Aliuliza:-

Idara ya Mazingira imewahi kutoa tahadhari kupitia Gazeti la Zanzibar Leo Toleo Nam. 2948 la Jumanne tarehe 16/2/2010 kuwa biashara ya mwani hapa Zanzibar ipo hatarini kufa na kupotea kabisa endapo Hoteli za Kitalii hazitodhibitiwa kumwaga baharini maji machafu yatokayo mahotelini na ambayo husababisha uchafuzi wa mazingira.

(a) Mhe. Waziri kwa kuwa Wizara yako ndio wahusika wakuu katika udhibiti wa mazingira. Je, kuna mkakati gani ili kunusuru kilimo cha mwani.

(b) Wakulima waliojitolea kuwekeza katika kilimo cha mwani kuwa kinamama. Je, ni zao gani mbadala watatafutiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 67 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi. Kuhusiana na hili, tafiti mbali mbali zinaendelea kufanyika kupitia mradi wa *MACEMP* ipo Kampuni ya *Birr* ambayo inafanya utafiti wa mwani huo huko kisiwa cha Fundo Pemba, hadi sasa utafiti unaendelea kutafuta mbegu ya mwani mnene *(cottonii)* ambao huoteshwa katika maji mengi.

(a) Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mazingira imewahi kutoa tahadhari kupitia Gazeti la Zanzibar Leo Nam. 2948 la Jumanne tarehe 16/2/2010 kuwa biashara ya mwani hapa Zanzibar ipo hatarini kupungua uzalishaji endapo Hoteli za Kitalii hazitodhibitiwa kumwaga baharini maji machafu kutoka kwenye hoteli hizo ambayo husababisha uchafuzi wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, katika kukinusuru kilimo cha mwani, Wizara yangu imo katika kuandaa viwango vya mazingira ambavyo vitakavyowezesha wale wote watakaoharibu au kuchafua mazingira wadhibitiwe kisheria. Aidha, Wizara kupitia Idara ya Mazingira imefanikiwa katika hatua za awali kuanzisha viwango vya maji machafu ambavyo vitaelekeza maji yanayomwagwa baharini yawe na kiasi gani cha kemikali na virutubisho.

(b) Mhe. Mwenyekiti, wale wote wanaojishughulisha na kilimo cha mwani pindi ikitokea hali mbaya ya uzalishaji wa mwani, serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira itaendelea na jitihada zake za kusaidia kupitia miradi yake ya *PADEP*.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kupitia Baraza lako tukufu tunatoa wito kwa wenye mahoteli yote kuiga mfano wa Hoteli ya Kempinski ambayo maji yake machafu hayaendi kule baharini na wanayatumia kwa kuyarejesha kwa ajili ya kazi za mboga mboga. Huu ni mfano mzuri na Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira sasa hivi anajiandaa kutoa toleo maalum kwa mahoteli yote kuhusu tahadhari hii.

Pamoja na kwamba tahadhari imeshatolewa kupitia magazeti, lakini Mhe. Waziri ndie mwenye wajibu wa kutoa tahadhari hiyo na atafanya toleo hilo maalum wakati wowote kuanzia sasa hivi baada ya kumalizika kikao hiki cha Baraza.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, leo katika mawio nimesikia bonde la Mahonda, Mtomchanga na sehemu nyengine lipo tatizo la umwagaji maji machafu yanayotokana na Kiwanda cha Sukari Mahonda.

Maji hayo ni machafu yanayotoka na kuharibu mazingira na ni hatari kwa watoto wanaokoga katika bonde hilo.

Je, Mhe. Waziri serikali ina mpango gani ikishirikiana na wizara kulichukulia hatua suala hili kabla ya kutokea madhara.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli taarifa hii mimi binafsi ndio kwanza naipata. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kiwanda kile kimekodishwa kwa hivyo kipo chini ya Wizara ya Fedha, lakini wizara mama ni sisi Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira.

Lakini napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba mara tu baada ya Baraza hili, mimi na Mhe. Waziri wa Fedha kutokana na matatizo mbali mbali yanayoendelea katika kiwanda kile tumekubaliana kwamba ipo haja twende *physical* tukafanye ziara pamoja na kukaa kitako na uongozi wa kiwanda kile tutazame tunafanya nini.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, wakulima wa mwani mwanzo kabisa walikuwa wanalima mwani wao katika maeneo ya karibu kabisa na fukwe. Lakini baadae ikaonekana kwamba wawekezaji wa mahoteli maeneo yale mengi wanayahitaji kwa ajili ya kuimarisha sekta ya Utalii. Kwa kuwa mambo yote mawili yanakwenda sambamba utalii unaingiza fedha katika nchi yetu, lakini pia wakulima wanajipatia rizki kwa maisha yao ya kila siku.

Lakini kwa upande mwengine Mhe. Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba hivi sasa tatizo la mwani nchini hususan mwani aina ya *cotonii* una bei kubwa lakini kilimo chake kinahitaji maji mengi.

Je, kwa kuzingatia hilo la kilimo hiki muhimu na tunaambiwa mbegu hii pia haistawi vizuri Zanzibar inastawi kwa shida lakini ina bei nzuri. Hivyo wizara ina mpango gani wa makusudi kuwapatia vifaa vya uvuvi akinamama na wakulima wengine ili wafike katika hayo maji mengi wafanye kazi zao vizuri kwa usalama wao.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi Mhe. Mjumbe amependekeza kuwa kutokana na tatizo la wakulima wa mwani kwamba itabidi sasa hivi wasogee walime mwani katika maji makubwa basi wawezeshwe. Kwa hivyo, suala hili tumelipokea na tutakaa kitako na wahusika wa idara yetu ya uvivi ili kutazama ni namna gani tutaweza kuwasaidia kina mama hawa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ukulima wa mwani wengi wanaofanya kazi ya kulima mwani ni wanawake na wanawake kama tunavyowajua hali zao, pamoja na kuwa mambo mengi wanayaweza lakini mpaka sasa hatujapata taarifa ya kuwa wanawake na wao wana utaalamu wa kuweza kuvaa vioo na kuzamia chini kwenye maji, na kwa sababu sasa hivi mwani unatakiwa ulimwe kwenye maji mengi

Je, Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atachukua juhudi gani ya kuwafundisha wanawake kuvaa vioo ili waweze kutumia katika upandaji wa mwani baharini.?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe amesema kwamba kina mama wawezeshwe ili waweze kufanya kazi zao vizuri za kuzamia kwa kuvaa vioo kama wanavyofanya kina baba katika sehemu mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kuvaa vioo pengine ni hapa kwetu tu, lakini ukitizama kama mnafuatilia katika TV au mtandao basi kina mama huko Europe kazi hiyo wanaifanya vizuri sana ya kuvaa vioo na kuzamia chini. Kwa hivyo, suala hili tutalichukua na kutizama vipi tutaweza kulisaidia suala hili au la. Kwa hivyo, napenda kumuhakikishia Mhe. Subeit kwamba hili jambo ni zuri, ni jipya kwetu sisi na linafaa kwa kweli. Wakati kina mama kama walivyosema wenyewe na sisi tuna amini hivyo kwamba wanaweza.

Nam. 85

Mchango wa BADEA

Mhe. Fatma Abdalla Tamim: (Kny: Mhe. Mkongwe Nassor Juma) – Aliuliza:-

Pamoja na uingizwaji mzuri wa fedha za mchango wa serikali katika miradi ya ujenzi wa majengo ya skuli, bado mchango wa wahisani katika baadhi ya miradi ya ujenzi wa maskuli hasa ile inayofadhiliwa na BADEA haitoshi na unafanya maendeleo ya miradi hiyo ya ujenzi kuzorota.

Je, wizara inafanya juhudi gani ili miradi hiyo ipate mafanikio yanayotarajiwa?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe Mjumbe swali lake nambari 85 kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kumekuwa na uingizwaji mzuri wa fedha za serikali katika kuhudumia kazi za maendelea katika sekta ya elimu. Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Februari 2010, jumla ya Shs. 1,670,000,000/= zilikuwa zimekwisha kutolewa na kutumika katika miradi mbali mbali ya maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa wahisani mchango wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) katika mradi wa elimu mbadala na amali umekamilika na mradi huu sasa umeshafungwa rasmi. Mhe. Mwenyekiti, kazi ya ujenzi wa kituo cha elimu mbadala huko Wingwi Mtemani Pemba zinatekelezwa kwa fedha za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mradi uimarishaji wa elimu ya lazima unaogharimiwa na SMZ na Benki ya Dunia, ni kweli kuwa kulikuwa kuna ucheleweshwaji mkubwa katika kuidhinisha hati za zabuni, kulikokuwa kukifanywa na Benki ya Dunia na hivyo kucheleweshwa utekelezaji wa baadhi ya kazi za mradi huo.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo tatizo hilo hivi sasa limepungua sana baada ya kufanywa mazungumzo baina ya viongozi wa pande mbili hizi. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa zabuni za wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa skuli 15 za sekondari za Unguja na Pemba zimeshatangazwa, na skuli 3 kwa Mkoa wa Kaskazini zabuni zake zimeshafunguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa ujenzi wa skuli mbili za sekondari huko Kibuteni Unguja na Mkanyageni kwa Pemba, unaogharamiwa kwa pamoja kati ya SMZ na BADEA, zabuni za washauri wajenzi *consultant* zimefunguliwa na kufanyiwa tathmini na hivi karibuni zitapelekwa BADEA kwa ajili ya kupata maamuzi kabla ya mshauri mjenzi kuchaguliwa rasmi. Mhe. Mwenyekiti, tunatarajia kusaini mkataba wa Kampuni ya Mshauri Mjenzi ya skuli hizi mbili mwishoni mwa mwezi wa Aprili, mwaka 2010.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Chuo Kikuu cha Taifa unaogharamiwa na SMZ na BADEA, ingawa kulikuwa kuna ucheleweshaji wa malipo ya awali ya mkandarasi kutokana na fedha za BADEA kuchelewa, lakini tatizo hilo hivi sasa pia limekwisha na mkandarasi amelipwa malipo yake yote.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Februari 2010, jumla ya USD 1,185,766.93 sawa na TShs. 1,490,710,611.38 zililipwa na BADEA ambazo ni sawa na asilimia 25 ya fedha zilizotengwa. Kwa sasa hakuna madai yoyote ambayo yanadaiwa na mkandarasi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi, ingawa SMZ imetoa fedha zote zilizotengwa kwa mwaka uliokusudiwa ambazo ni sawa na milioni 400,000,000/= kwa mradi huu, fedha za mhisani ambaye ni Shirika la Maendeleo ya Misaada la Sweden hadi leo hazijatolewa.

Mhe. Mwenyekiti, kuchelewa kupatikana kwa fedha hizo kumetokana na kuchelewa kukamilika kwa taratibu za mkataba wa msaada huo baina ya SMZ na Ubalozi wa Sweden uliopo Tanzania. Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo mazungumzo yaliyofanyika hivi karibuni baina ya pande hizi mbili kukubaliana

kukamilisha taratibu zilizobakia ili msaada huo uweze kutolewa kabla ya kumalizika mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kuwezesha kuingizia fedha kwa wakati na hivyo kuwezesha kutekeleza miradi yetu ya maendeleo, hata pale fedha za wahisani zilipokuwa zikichelewa, ahsante.

Nam. 23

Matumizi ya Vifaa vya Uchunguzi Mnazi Mmoja

Mhe. Hija Hassan Hija: (Kny: Mhe. Abass Juma Muhunzi) – Aliuliza:-

Kwanza natoa shukrani kwa wizara kupitia kwa Mhe. Waziri kwa kukamilisha miradi ya uboreshaji huduma za afya katika Hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja, hasa miradi ya *CT Scan* na ukarabati majengo.

(a) Kwa kuwa kifaa hiki cha CT Scan ni kimoja tu kwa Unguja na Pemba Je, kuna utaratibu wowote katika wizara ili wale wagonjwa wanaopata rufaa moja kwa moja kutoka Pemba wapate huduma za haraka bila malipo ya ziada?

(b) Kwa kuwa tokea kifaa hicho kiwasili na kuanza huduma kumekuwa na madai mengi ya ughali wa malipo ya huduma zake je, mkabala na changamoto hii ya malipo utumiaji kwa wananchi wa kawaida unaendelea vipi?

(c) Je, kazi ya chombo hiki cha aina ya CT Scan zinatafautiana vipi na zile za X-Ray na Ultra Sound na tokea CT Scan ianze kazi, X-Ray na Ultra Sound zimeathirika vipi?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 23 lenvye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, wanaopata rufaa kutoka Pemba kwa ajili ya CT Scan watatakiwa kulipa malipo kwa ajili ya kipimo hicho kama wagonjwa wengine wanaotoka Unguja. Isipokuwa utaratibu umewekwa kwa agizo la Mhe. Rais alivyosema azma ya Mapinduzi ya Jamhuri ya mwaka 1964 ni kuwapatia huduma za afya bila ya kujali kipato chao.

(b) Mhe. Mwenyekiti, tokea kuanza kasi kwa mtambo huu wa CT Scan, mwezi wa Aprili 2009 mpaka Disemba 2009, jumla ya wagonjwa 336 wamefanyiwa uchunguzi na kati ya hao 102 walisamehewa malipo ya kipimo hicho.

(c) Mhe. Mwenyekiti, CT Scan ni kipimo cha uchunguzi huwa kuna ngazi mbali mbali za uchunguzi, hivyo kuwepo kwa CT Scan hakufanyi uchunguzi wa vipimo vyengine, kama X-Ray na Ultra Sound kutotumika. CT Scan ni kipimo cha hali ya juu cha maradhi. Kwa mwaka jana 2009 Januari mpaka Disemba jumla ya X-Ray 10,393 zilipigwa, na Ultra Sound 5,061 zilifanywa na CT Scan 336 zilifanyika, ahsante.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, ulipoanza kuja mtambo huu wa CT Scan tuliufurahia sana, hasa kwa maelezo ya Mhe. Waziri. Tulitegemea kwamba matokeo yatakayoonekana kwa mgonjwa atakayechunguzwa yatapatikana mara moja. Lakini kwa bahati mbaya mpaka mwezi uliopita, wasomaji wa matokeo hatuwatambui vizuri.

(a) Je, kwa nini hawatafuti wasomaji wa matokeo ya mgonjwa ili wakapata majibu haraka?

(b) Kwa wale wanaotoka Pemba huwa wanakuja kwa boti na wengi wao wakifika hapa wanakuwa hawana nyumba za kukaa, huwa wanakaa mahoteli. Je, huko kuchelewesha kuwapa matokeo ya wagonjwa si mtawazidishia gharama zaidi. Je, wizara ina mpango gani wa kuoana kwamba imejenga nyumba moja ya akiba kwa wale wanaotoka mbali wawe wanahifadhiwa pale?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa kweli kipindi kilichopita hapa, wakati tulikuwa na tatizo la umeme, kweli filamu zetu zilikuwa zinachelewa kusomwa na ni kweli alikuwepo msomaji mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba sasa hivi hali imekuwa ni nzuri, mimi mwenyewe nimefika kwenye kitengo hicho siku mbili zilizopita, sasa hivi hali ni nzuri. Kwa mara ya mwisho hiyo juzi nilipopita walisema kuwa, filamu zilizobakia ambazo hazijasomwa kwa siku ile zilikuwa ni tano tu. Kwa hivyo, hali ni nzuri.

Lakini kama hiyo haitoshi Mhe. Mwenyekiti, tayari ameshakuja yule mtaalamu wetu, yaani *Radiologist* wetu mwengine ambaye ni Mzanzibari na ni mzalendo ameshafika na hivi sasa yuko kwenye likizo kidogo na karibu ataanza kazi, ana kama wiki moja na nusu kapewa mapumziko baada ya kutoka masomoni. Kwa hivyo, atasaidiana na huyu mtaalamu wetu wa Kichina kusoma filamu hizo. Kwa hivyo, naamini sasa hivi kitakachoendelea filamu hazitokaa tena, zitakuwa zinapigwa na hapo hapo zinasomwa na watu wanapata matokeo yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa wale wanaotoka Pemba, kama lile jibu la mwanzo nililokwishaeleza kuwa hivi sasa uchelewaji utakuwa haupo, kwa hivyo haina haja sasa hivi kutafutiwa nyumba maalum ya kukaa. Watafikia hospitali watapigwa picha hizo, watapata majibu yao na hali itakuwa nzuri . Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salima Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, CT Scan ni kifaa kizuri ambacho kinatumika kwa ajili ya kutambua maradhi tofauti. Kifaa hiki ni kikubwa na kimo katika sehemu maalum.

Mhe. Mwenyekiti, swali langu ni kuwa pamoja na umuhimu na faida ya kuwa na kifaa hiki tulichonacho.

(a) Je, kifaa chenyewe katika kufanyakazi kwake hakitowi mionzi yoyote na kadhalika?
(b) Ikiwa hivyo ndivyo, ni mara ngapi mgonjwa anaweza akapimwa kwa kutumia kifaa hiki na baada ya hapo ikawa hawezi kutumiwa nacho tena, kama kinadhara?
(c) Kama kinadhara kutokana na kazi yake kubwa inayofanywa, kuna wafanyakazi wanakaa mule kwa muda mrefu sana, sijui wafanyakazi hawa ni kwa kila kipindi gani kama kuna mionzi yenye dhara, ili wafanyakazi hawa kuweza kupima afya zao?
(d) Je, kuna chochote cha kutumia kama chakula na kadhalika katika kufanya kazi yao, ili waweze kupungukiwa na hiyo dhara?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, nataka kumuhakikishia Mhe. Mjumbe kuwa chombo chetu cha CT Scan hakina mionzi ya sumu, mionzi ilioko ni mionzi ya kawaida na kwa mionzi hii mgonjwa anaweza akapimwa na wala hasipatwe na tatizo lolote.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mara ngapi apimwe ili asipate matatizo. Suala hili linategemea daktari atakavyoshauri kuwa mgonjwa yule apimwe mara ngapi. Lakini kipimo kama hiki mara nyingi mtu hawezi kurudia hapo kwa hapo, yaani baada ya muda mfupi akarudia tena. Vipimo kama hivi huwa vinapimwa kwa uhakika, linaonekana mtu tatizo lake lote lililokuwepo ndani ya mwili na baada ya kwishakuonekana, kwa hivyo, kwanza huwa anatumia dawa na pindi akitaka tena kujakuangaliwa tena basi anaweza kuja kuangaliwa tena na wala hapati madhara yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu wafanyakazi kuathirika. Wafanyakazi mpaka sasa hivi bado hatujapata taarifa ya kuwa wameathirika kutokana na mionzi hiyo. Lakini kwa utaratibu kwa upande wa chakula mara nyingi huwa wanatakiwa kama panakuwa na uwezo waweze kutumia maziwa, kwa sababu wakati mwengine ukitumia muda mrefu, ile mionzi inaweza ikakuletea tatizo, lakini sio kubwa sana. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Mhe. Mwenyekiti, wakati anajibu swali la msingi Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba wale wananchi ambao hawana uwezo katika huduma hii ya CT Scan wanakuwa wanapata msamaha. Swali langu ni kuwa,

(a) Ni vigezo vipi vinavyotumika katika huko kutoa msamaha?
(b) Nani anayethibitisha kweli kwamba huyu mwananchi ana uwezo au hana uwezo?
(c) Je, havitumiki vigezo vya kujuana zaidi kuliko vigezo vya umaskini?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:

(a) Mhe. Mwenyekiti, vigezo vinavyotumika ni kuwa mgonjwa anapoletwa pale na akasema kuwa yeye hana uwezo wa kulipa, kinachofanyika ni kwamba kama mgonjwa hajiwezi basi ni jamaa zake, kama mgonjwa mwenyewe anajiweza ni yeye mwenyewe anatakiwa alete barua ya sheha. Sheha ndiye anayekaa na wananchi wetu na ndiye anayejua nani mwenye tatizo na nani mwenye uwezo.

(b) Kuhusu nani anayethibitisha, tunacho kitengo chetu cha uhusiano au tunakiita kwa jina jengine mama huruma. Kiko kitengo pale karibu na afisi kama unakwenda kwa Mkurugenzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mama huyu yeye ndiye anayehusika na masuala yote yale ambayo watu wanakuja pale wasiojiweza na anawaelekeza nini cha kufanya, taarifa zikishakufika kwake tu basi huyo mgonjwa anasamehewa na kuweza kupatiwa kipimo hicho.

(c) Kuhusu suala la kujuana, kwa kweli hilo hatuna kabisa. Mtu yeyote tunayemjua au tusiyemjua, madhali ana uwezo basi alipe na kama unamjua hana uwezo pia atasaidiwa. Kwa hivyo, suala la kujuana Mhe. Mwenyekiti halipo, kwa hivyo watu wote waliokuwa hawana uwezo wanasaidiwa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kidogo niongezee ili Waheshimiwa Wajumbe wazidi kutufahamu.

Sisi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tunapenda wananchi wetu wapate huduma hii kwa bei ya chini au nafuu na hata bure, lakini sasa hivi kwa mujibu wa utaratibu tunaokwenda nao basi miaka miwili tuna-*guarantee* ya *supplier* kwamba huduma hii ataigharamia yeye.

Kwa hivyo, baada ya miaka miwili *service* ya kuifanyia CT Scan kwa mwaka ni dolla 12, bila ya kubadilisha *tube*. Kama tutabadilisha *tube* basi inatakiwa tulipie dolla 50,000. Box la filamu ambapo zimo filamu 100 ni nusu milioni, ile dawa ya kupakwa yule mgonjwa 50 mls ni 33,000. Kwa hivyo, gharama ya kuendesha CT Scan ni kubwa. Lakini sasa hivi kwa miaka hii miwili tumefungua *account*, kinachopatikana tunakiweka ili baadae tusipate usumbufu wa kuendesha CT Scan.

Kwa hivyo, tunachokifanya tunahakikisha kwamba hakuna upendeleo, aliyekuwa na uwezo basi achangie tena bei yetu sisi Zanzibar ni rahisi ukilinganisha na ndugu zetu wa hapo Tanzania Bara. Kwa hivyo, wale wenye uwezo wa chini au hawana uwezo kabisa, tunawafanya wasilipe chochote na wale tunaowaona kidogo afadhali basi walipe angalau asilimia 50 na wale wenye uwezo basi wachangie ili hapo baadae tuweze kuendesha CT Scan bila ya matatizo yoyote.

Keshokutwa tarehe 20 Aprili tunatimiza mwaka mmoja kwa kuweka CT Scan.

Nam. 24

Hospitali ya Abdalla Mzee

Mhe. Hija Hassan Hija: (Kny: Mhe. Abass Juma Muhunzi) – Aliuliza:-

Moja ya matatizo ya hospitali ya Abdalla Mzee ni uchakavu wa majengo yake na vifaa vikiwemo vitanda vya kulalia wagonjwa.

(a) Je, ni lini hospitali hiyo ambayo ni kama hospitali ya rufaa kwa Pemba itafanyiwa marekebisho makubwa, ikiwemo ukarabati wa majengo na uwekaji wa vifaa vya kisasa?

(b) Je, zipo nyumba kwa ajili ya madaktari hasa wale wa zamu za usiku. Je, panapotokea dharura wakati wa usiku upatikanaji wa madaktari wa zamu unakabiliwa vipi kwa hospitali hiyo?

(c) Je, kuna malipo yoyote ya *overtime* kwa madaktari na wahudumu wengine wanaotoa huduma baada ya saa za kazi kwa hospitali zetu Unguja na Pemba?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 24 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Hospitali ya Abdalla Mzee inatumika kama hospitali ya rufaa kwa Pemba, kwani ina madaktari bingwa kutoka Jamhuri ya Watu wa China, takriban ni wa fani nyingi ukilinganisha na hospitali nyengine.

- Kwa hivi sasa Hospitali hii ya Adballa Mzee tunaendelea kuifanyia ukarabati mdogo hatua kwa hatua. Kama hivyo haitoshi hospitali hiyo tunategemea kuitia katika mpango wa awamu ya pili ya ADB ya matengenezo ya ya majengo ya wizara.
- Vile vile ndugu zetu wa Kichina wametuahidi baada ya watakapomaliza ujenzi wa nyumba za madaktari wa Kichina wataifanyia ukarabati mkubwa hospitali hiyo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, nyumba kwa ajili ya madaktari zipo na wanakaa madaktari wetu wa Kichina na wale wazalendo wanakaa katika nyumba zao.

- Muda mwingi daktari wa zamu huwa yupo hospitali, lakini kwa wakati wa usiku inapotokea dharura hutolewa gari kumfuata nyumbani.

(c) Mhe. Mwenyekiti, malipo ya *on call* yanapatikana na hutolewa kwa madaktari na wahudumu wengine kwa kadri zinapopatikana fedha, ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa matatizo yaliyokuwepo katika hospitali ya Abdalla Mzee ni kukosekana kwa wodi maalum ya viongozi yaani VIP wodi. Suala hili tunaelezwa vipi?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, suala hili au tatizo hili tumekwishalipata kwa muda mrefu na tumekwisha waagiza wafanyakazi wetu wa Hospitali ya Abdalla Mzee. Kuna chumba ambacho kilikuwa kimependekezwa na baadhi ya wajumbe hapa hapa kuwa basi hicho kingeandaliwa kikawa ni VIP.

Kwa hivyo, sisi tumewaelekeza wafanyakazi wetu huko Pemba kuwa chumba hicho wakitengeneze na kikishakamilika basi kitatumika kama ni VIP.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni kuna mbunge aliumwa na akalazwa katika

Hospitali ya Abdalla Mzee na ilitarajiwa kwamba angelazwa katika hicho chumba kilichotajwa cha pembeni, lakini kwa bahati mbaya alilazwa katika chumba cha kawaida na wagonjwa wengine.

Je, haionekani kwamba kutokulazwa kwa mheshimiwa katika chumba kinachohusika na badala yake akalazwa mtu mwengine katika chumba kile na yeye akalazwa na watu wengine, haionekani kwamba hapa imefanywa dharau tena ya makusudi?

Kama hii iliyofanywa ni dharau ya makusudi, Je wizara inahatua gani za kuchukua ili kuhakikisha kuwa waheshimiwa wanapatiwa nafasi inayostahiki?

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu ya Afya na Ustawi wa Jamii napenda nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba hatujafanya dharau, wala hatujamfanyia vibaya mheshimiwa huyo. Kwa sababu kwanza hatujui kwamba yule mheshimiwa ana maradhi gani, pengine kama ni mfupa kuna wodi maalum na kuna zana za kutiwa vitu pale, hatuwezi kujua.

Pili hatuwezi kujua kwamba chumba hicho kilichodhaniwa pengine kilikuwa na mgonjwa ambaye alihitaji kutengwa na wagonjwa wengine kwa maradhi aliyokuwa nayo. Kwa hivyo, hatuwezi kujibu jibu sahihi na tutakwenda kinyume tukimtajia mheshimiwa maradhi yake. Kwa hivyo, ikiwa tumelifanya kosa, basi tunakiri hatutofanya tena na tutafanya kama alivyotushauri Mhe. Mwakilishi, ahsante.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, wizara ya afya imejitahidi kutengeneza majengo vizuri sana, na inaonekana mradi wa GP5 kila eneo, unaweza kusaidia kwa sababu nafikiri sio chini ya nyumba 40 zimeshajengwa kwa madhumuni ya kuondoa tatizo.

(a) Lakini naomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba alionaje asitengeneze hospitali ya Abdalla Mzee akaona ni bora kuzijenga zile hospitali zilioko Pemba kwa mradi wa GP5 wakati Hospitali ya Abdalla Mzee ndio Hospitali ya Rufaa.

(b) Kuhusu uchakavu wa vitanda na magodoro. Juzi hapa alisifiwa mbunge fulani wa Mji Mkongwe, inaonekana kumbe wakishajihishwa wanaweza. Je, amewahi kumshirikisha Mhe. Mwakilishi wa Mkoani pamoja na mbunge, pia viongozi wa Wilaya ya Mkoani ili kuondoa matatizo kama haya madogo madogo

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda nimpongeze Mhe. Ame Mati Wadi. Pia jana aliuliza swali kuhusu vitanda vibovu na magodoro mabovu. Nilipojibu hapa Mhe. Mwenyekiti, naomba uniamini, baada ya kutoka hapa nikakutana na Meneja wa MNB Mr. Majid, basi leo kwa ile furaha yake ananikabidhi mashuka ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, ile furaha yake imetokana na Mhe. Ame Mati Wadi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Ame Mati saa 6:00 aje wizarani leo ili ashuhudie.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, mradi wa kujenga nyumba za madaktari 40, 20 Pemba na 20 Unguja, huu ni mradi wa ADB wa kupunguza vifo vya mama na watoto, yaani inatakiwa Kituo cha Afya kiwe na Nyumba ya Muuguzi wa koo mbili, anapotokea mzazi basi asitafutwe muuguzi pale pale inaharakishwa na kuzalishwa. Huo ndio mradi na wala sio ule aliousema wa JB5.

Kwa kweli mradi ule tumejenga Nyumba ya Daktari Micheweni kwa Mhe. Subeit Khamis Faki *(Makofi)*.

Kuhusu Hospitali ya Mkoani ya Abdalla Mzee ndugu zetu wa Kichina hivi sasa wanagharamia wenyewe kujenga nyumba zao wenyewe Madaktari wa Kichina. Nyumba zao mbili mwezi huu wa *April* zitamalizika, tena zitakuwa za kisasa ambazo zenye *furniture* za kisasa pamoja na *Solar Power* kubwa sana itakuwemo, yaani kila kitu kitawekwa.

Vile vile wametuahidi mambo yakimalizika wataingia kwenye hospitali, wameniambia wenyewe. Kwa maana hiyo, wataingia sehemu kama vile *Theater*, Maabara, *Maternity* pamoja na kuweka vyombo vya kisasa, yaanii wataifanya ile hospitali iwe ya hali ya juu. Haitoshi hivyo tumesema pia tutaitia kwenye

mradi wa *ADB*. Kwa hivyo, kuhusu vitanda na magodoro labda *NMB* wataiona Hospitali ya Abdalla Mzee *(Makofi)*.

Nam. 36

Ubovu wa Vyombo vya Usafiri wa Baharini na Bei za Juu za Nauli

Mhe. Haji Mkema Haji – Aliuliza:-

Serikali imebinafsisha Sekta ya Usafiri wa Baharini kwa lengo la kutoa huduma bora zenye gharama nafuu. Matokeo yake Wawekezaji wameingiza nchini vyombo vibovu na kutoza nauli za juu.

(a) Serikali kwa kiasi gani inasimamia bei za mizigo na nauli za abiria katika sekta ya bahari?

(b) Uingizaji wa magari umewekewa viwango kutokana na hali ya uchakavu wa gari. Je, utaratibu kama huo umewekwa kwa vyombo vya usafiri wa baharini. Kama umewekwa kwa nini haufuatwi na kupelekea kuingizwa nchini vyombo vibovu na vilivyochakaa sana?

(c) Wizara inachukua hatua gani kupambana na tabia ya wenye boti na meli kuuza tiketi chache kwa wasafiri na kutoa taarifa kwamba tiketi zimekwisha na baadaye walanguzi kuziuza kwa bei ya juu sana?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.36 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu kupitia Afisi ya Mrajis wa Meli Zanzibar haisimamii bei za mizigo na badala yake husimamia na kuangalia usalama wa meli katika kupakia mizigo hiyo pamoja na abiria. Kwa vile biashara huria hutegemea mapatano baina ya mwenye mzigo na mwenye meli.

Hata hivyo, hivi sasa wizara yangu kupitia Afisi hii ya Mrajis wa Meli haijapokea malalamiko yoyote kuhusiana na suala hilo.

Aidha kwa upande wa nauli za vyombo vya baharini. Wizara yangu kupitia Afisi ya Mrajis wa Meli Zanzibar kwa kushirikiana na wenye vyombo hivyo, ili kukubaliana viwango vya juu vya nauli kwa meli za mwendo wa kasi na mdogo.

(b) Napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa kuna tofauti kubwa baina ya magari na meli, kwa vyombo vya baharini hakuna muda maalum wa kuvitumia vyombo hivyo. Isipokuwa jambo hilo linasisitizwa na kufanyiwa matengenezo kwa vyombo husika kila wakati, ili chombo kiweze kuwa katika hali nzuri.

Hata hivyo, wizara yangu inaangalia uwezekano wa kuweka muda maalum wa kuruhusu chombo kuingizwa nchini ambacho kimeshatumika. Vile vile gharama za kununua vyombo vipya ni kubwa mno, ambapo wamiliki wa vyombo vya baharini hushindwa kununua vyombo vipya kutokana na gharama hizo.

Aidha napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako tukufu kwamba, vyombo vya usafiri wa baharini hapa Zanzibar vinasimamiwa na Sheria ya Zanzibar ya *Maritime Transport Act* ya mwaka 2006, ambayo haikutaja umri wa meli ambazo zinatarajiwa kusajiliwa Zanzibar.

Wizara yangu kupitia Afisi ya Mrajis wa Meli kabla ya kusajili meli hiyo huikagua kwa kina, kwa ajili ya kuangalia uzima pamoja na mapungufu ya vyombo husika.

(c) Wizara yangu kupitia Afisi ya Mrajis wa Meli Zanzibar imekuwa ikitoa matangazo kwenye vyombo vya habari kwa lengo la kuwahamasisha wananchi wanunue tiketi kwenye sehemu maalum zilizotengwa kwa ajili ya kuuzia tiketi hizo au wakala, ili kuepusha ulanguzi wa tiketi.

Wizara kupitia Afisi ya Mrajis wa Meli katika kutatua tatizo hilo imeamua tiketi zote ziuzwe kwa watu wenye vitambulisho tu. Kampuni yoyote itakayobainika kutokufanya hivyo au kushiriki katika ulanguzi, wizara yangu huchukua hatua za kuwapiga faini kutokana na Sheria ya *Maritime Act*.

Vile vile ninaomba ieleweke kuwa ulanguzi ni kitendo kilicho kinyume na sheria ya nchi. Hivyo, naliomba Jeshi la Polisi pamoja na taasisi nyengine za kisheria kuchukua hatua zinazofaa mara baada ya kubaini kuwepo kwa kitendo hicho.

Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Hivi karibuni kumekuwa na taarifa kwamba kuna meli ya Zanzibar imezama bandarini Dar-es-Salaam. Je, taarifa hii unayo Mhe. Waziri na kama unayo ni hatua gani imechukua wizara yangu kwa ajili ya kuangalia ni kitu gani kilichopelekea kuzama kwa meli hiyo?

(b) Mhe. Waziri wakati alipokuwa akijibu swali mama alisema kwamba kuna utaratibu wa kusajili meli hizi ambazo zinakuja hapa kwa ajili ya kuchukua abiria. Lakini kilichojitokeza ni kwamba kuna meli nyingi sana bado hazifanyikazi au muda wake umekwisha au vyovyote vile, yaani zinaonekana ni mbovu na bado zinaendelea kuelea katika bahari ya Zanzibar karibu na bandari.

Je, Mhe. Waziri wizara yake inao utaratibu gani wa kuziondoa meli hizi, kwa sababu hazileti mandhari nzuri kwa kuwa hazitumiki kwenye bandari yetu?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba hivi karibuni kiasi ya wiki moja au mbili nyuma meli ya zamani iliyokuwa ikiitwa MV. Pemba ilikuwa inatokea Dar-es-Salaam na mizigo ikagonga inasemekana ni boya au kitu chengine chenye uzito mkubwa na kutoboka chini na kuzama. Meli hii ilikuwa na mabaharia 12 na wote waliokolewa na wala hakuna abiria ambaye amefariki. Ilikuwa nje kidogo ya bandari ya Dar-es-Salaam na ilikuwa inaelekea Zanzibar

Kweli zipo meli nyingi pale katika eneo letu ya bandari ambazo zinaelea. Meli nyingi hizi zilikuja wakati ule ilipoanza Biashara Huria, kwa hivyo tulikuwa na meli ndogo ambazo zilifanyakazi. Lakini nyengine sio kama mbovu kabisa kabisa, isipokuwa zinaelea pale kwa sababu hazina soko tena, yaani watu hawataki kupanda vyombo vile kwa sababu ya maendeleo ya kuletwa meli nyengine mpya ambazo ni nzuri, basi wale wengine wameshindwa kuziendesha.

Kwa kweli wenyewe kwa wenyewe wamiliki wa meli wanauziana na nyengine wanazifanyia shughuli nyengine. Kwa mfano, meli yetu ya MV. Mapinduzi pia inaelea pale na tumo kwenye utaratibu wa kuiuza, ili nayo tuiondoe kwa sababu hatupendi kuwa na meli pale kwani ni hatari kwa usalama wa bandari yetu.

Mhe. Juma Duni Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wakati alipokuwa akijibu swali la msingi alieleza kwamba wao hawashughuliki na mizigo na badala yake wanashughulika na usalama wa abiria tu.

(a) Hivi Mhe. Waziri anajua kwamba tunaposubiri boti kupanda kwa ajili ya kuelekea au kutoka Dar-es-Salaam sehemu ya kusubiri kupanda boti ni dhaifu na wala si nzuri? Kwa kweli abiria wanapotaka kusafiri wanapata usumbufu na hiyo sehemu ambayo ipo imeshachakaa na upande mmoja imeezekwa tanga ambalo limetoboka lote hata mvua na jua halizui.

(b) Kuna taarifa kwamba kuna Mwekezaji ambaye anayo boti alitaka kujenga nafasi hiyo ya kupumzikia abiria, lakini amekataliwa. Hivi kuna ukweli wowote kuhusu suala hili?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, nikiri kwamba bado eneo letu la kuhifadhi abiria haliko katika hali nzuri. Lakini wizara yangu kupitia Shirika la Bandari linao mchakato wa kujenga jengo jipya la kisasa la abiria katika Bandari ya Malindi. Tumekubaliana kwamba Bandari ya Malindi wawe na jengo zuri zaidi kuliko yale ya Wete na Mkoani, ili liendane na hadhi ya Makao Makuu ya Shirika la Bandari *(Makofi)*.

Kuna taarifa kwamba kuna mmiliki wa meli ambaye alitaka kujenga. Kwa kweli habari hizo niliwahi kuzisikia lakini hatukumruhusu pale, kwa sababu yale masharti yake yeye na yetu sisi yamepishana. Isipokuwa mmiliki huyo alikuja kwa awamu ya pili na kutaka apewe baadhi ya sehemu kwa ajili ya kujenga afisi yake pamoja na afisi nyengine pale kwenye Bohari, tulimruhusu, yaani mimi mwenyewe, lakini bado sijaona hatua za ujenzi kuanza.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Katika swali mama Mhe. Mwakilishi aliuliza kuhusu tiketi za ulanguzi ambacho kipengele cha (c) na tiketi hizi zaidi hutokea wakati wa mwisho wa wiki. Kwa mfano, ukitoka Dar-es-Salaam kuja Zanzibar basi unaweza kwenda wakati muafaka kwenye vituo na kuambiwa tiketi zimekwisha, lakini kwa bahati nzuri ukija pembeni kidogo unaambiwa tiketi badala ya shilingi 18,000/- au 20,000/- ukaambiwa utoe shilingi 30,000/- mpaka 35,000/- unapata tiketi pale pale.

Kwa kuwa jibu lake Mhe. Waziri amemjibu kwamba anatoa wito kwa Vyombo vya Dola kufanyakazi zao vizuri kwa watu wanaofanya vitendo hivyo vya haramu. Je, kwa kuwa suala hili hapa Unguja lipo kwa asilimia ndogo, lakini adha inayotokea ni zaidi kwa upande wa kutoka Dar-es-Salaam kuja hapa Unguja. Hivyo, Mhe. Waziri atachukua hatua gani za makusudi angalau kuzungumza nao wanaohusika na vyombo hivi, ili kuliondoa tatizo hili?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kwa upande wa Tanzania Bara ulanguzi unafanyika zaidi kuliko Zanzibar.

Lakini Waheshimiwa Wajumbe lazima tufahamu kwamba mamlaka yetu sisi yapo kwa upande wa Zanzibar, upande wa Tanzania Bara wenye dhamana ya kuhakikisha usafiri uko salama ni Mamlaka ya Usafiri na Baharini na Nchi Kavu (*SUMATRA*), ambayo iko chini ya Wizara ya Miundombinu.

Hata hivyo, sisi na Wizara ya Miundombinu tunafanya mikutano, ambapo mkutano wetu wa mwisho tuliufanyia Chakechake Pemba na tulizungumza mambo haya. Hatimaye *SUMATRA* walifanya ziara ya kikazi, yaani walikuja Zanzibar na kwenda mpaka Pemba na kuandika ripoti yao na mimi walinipatia *copy* ya ripoti yao. Kwa kweli wamekiri kwamba kwa upande wa Dar-es-Salaam suala la ulanguzi wa tiketi linaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tuliwashauri kwamba ili kulipunguza tatizo hili na wao waanzishe utaratibu wa kuuza tiketi kwa kutumia majina halisi ya watu pamoja na vitambulisho. Nadhani ndilo suluhisho pekee la kupunguza ulanguzi wa tiketi katika bandari zetu hizi mbili.

Nam. 38

Ujenzi wa Barabara ya Kenya – Chambani

Mhe. Hija Hassan Hija (Kny: Mhe. Abass Juma Muhunzi) – Aliuliza:-

Kwa miaka zaidi ya 5 sasa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi imekuwa ikiahidi katika Baraza hili kuanzisha ujenzi wa barabara ya Kenya – Chambani. Pamoja na ahadi hiyo mimi Mwakilishi wa Jimbo la Chambani na Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi tumeshafanya ziara ya pamoja na kukagua barabara hiyo.

(a) Je, Mhe. Waziri, kilichokwamisha kuanza kwa ujenzi huu ni kitu gain?

(b) Kwa kuwa suala la ujenzi wa njia hiyo lilielezwa kwenye vipeperushi vya Ilani ya Uchaguzi wa CCM vilivyomwagwa kwenye eneo la Kenya Chambani wakati wa Kampeni za Uchaguzi wa 2005 vikieleza kwamba ujenzi huo ungefanyika ndani ya miaka mitano.

Je, Mhe. Waziri huoni kuwa kuendelea kudharau ujenzi wa njia hiyo ni kudharau Ilani ya Chama kinachojitayarisha tena kwa Uchaguzi Mkuu wa 2010?

(c) Baadhi ya sehemu za Chambani katika barabara itokayo Pujii – Chakalakati – Tumbini na kuelekea Ukutini kuna vikuta vya saruji vilivyowekwa na wizara miaka 3 iliyopita, lakini wananchi hawafahamu nini kinaataka kufanywa. Je, Mhe. Waziri utawaeleza nini wananchi wa Chambani juu ya jambo hilo, hasa wale wanaotaka kujenga pembeni mwa barabara hiyo?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 38 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Hakuna kilichokwamisha kuanza kwa ujenzi wa barabara ya Kenya Chambani, isipokuwa ni utaratibu wa mpango wa barabara sita ambazo zimepata ufadhili wa *NORAD*.

Kwa mujibu wa utaratibu wa mradi huo ni kuwa hivi sasa barabara ya Mtambile – Mwambe na Mtambile – Kangani zimeanza. Kabla ya kuweka lami barabara hizo kazi za usafishaji zitaanza kwa barabara mbili nyengine, ambazo ni barabara ya Mizingani – Wambaa na Kenya – Chambani, ambapo ujenzi huo unatarajiwa kuanza ndani ya mwaka huu wa fedha *(Makofi)*.

Kama nilivyoeleza hapo awali ni dhahiri kuwa wizara yangu inathamini sana barabara hiyo pamoja na kuthamini utekelezaji wa njia zote za ahadi za viongozi wakuu, kuendelea kuitekeleza kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi na matayarisho ya ushindi kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010.

Aidha vikuta vilivyowekwa kwenye barabara itokayo Pujini – Chakalakati hadi Tumbini kuelekea Ukutini, kwa ajili ya matayarisho ya barabara ya Ole – Kengeja yenye urefu wa kilomita 35.

Hivyo nachukua fursa hii kuwaomba wananchi wa maeneo hayo kutokuvamia kwa ujenzi wa aina yoyote maeneo yaliyowekwa vikuta hivyo ikiwa ni eneo la hifadhi ya barabara.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Kwa kuwa amekiri kwamba ujenzi wa barabara ya Kenya – Chambani uko kwenye *program* ya barabara sita za *NORAD*, ambapo tayari barabara ya Mtambile – Mwambe imeanza. Kwa hivyo, napongeza kwa kuanza ujenzi wa barabara ya Mtambile – Mwambe kwa hatua ya robo kilomita kwa lami.

(a) Barabara ya Kenya – Chambani ni miongoni mwa barabara sita za *program* ya mradi wa *NORAD*. Je, nataka nijue barabara ya Mgagadu – Kiwani ni *program* ipi na lini itamalizika?

(b) Je, Mhe. Waziri anajua kwamba barabara ile tokea juzi zilipoanza mvua za masika wananchi wanatembea kwa miguu barabara imekatika na yupo tayari kwenda kuona yeye na mimi?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Mgagadu – Kiwani inajengwa na SMZ kwa asilimia mia moja na lengo letu imalizike mwaka huu wa fedha *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, wiki tatu zilizopita nilikuwa huko na nilitembelea Mgagadu – Kiwani na tulikuwa tunaweka kifusi, ili mvua za masika zisitusumbue. Sasa kama Mhe. Mwakilishi ananihakikishia imekatika basi kwanza kabla sijakwenda nitawaagiza maafisa wangu wakaishughulikie, ili wananchi waweze kupita na tukimaliza Baraza Mwenyezi Mungu akitujaalia uhai na uzima baada ya Sikukuu ya Pasaka Mhe. Mwakilishi tunaweza kwenda Pemba mimi na wewe kwa ajili ya kuangalia eneo hilo *(Makofi)*.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza kabla sijauliza niipongeze Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kweli imefanya juhudi kubwa za kuzijenga barabara nyingi Unguja na Pemba *(Makofi)*.

Lakini baada ya pongezi hizo naomba nimuulize Mhe. Waziri. Kwa kuwa alisema kwamba viongozi wa juu waliahidi barabara nyingi zitajengwa zikiwemo zile sita za kule Pemba. Hata hivyo, Mhe. Rais alipokuja katika shughuli ya ufunguzi wa skuli Muyuni aliwaagiza Manaibu Waziri pamoja na watendaji waishughulikie barabara ya Kijini, ili angalau ipitike.

Vile vile Mhe. Rais alizungumza katika utoaji wa vifaa vya uvuvi kule Pwanimchangani, kwamba barabara ya Kijini ishughulikiwe haraka iwezekanavyo. Je, Mhe. Waziri hili hili agizo la Mhe. Rais agizo la Mhe. Naibu Waziri amelisahau pamoja na watendaji wake, kama amelisahau Mhe. Naibu Waziri najua amepitikiwa na wewe Mhe. Waziri utachukua hatua gain? *(Makofi)*.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Uongozi wa Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Amani imefanya kazi kubwa sana katika ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Kwa kweli sehemu ambazo zimefaidika sana moja ni Jimbo la Matemwe, kwa sababu lami iko kila upande. Kwa mfano, ukipita Pwanimchangani mpaka Matemwe na ukipita Matemwe yenyewe hali ndiyo hiyo. Kwa hivyo, barabara ni nyingi wanashindwa hata kuzitumia *(Makofi)*.

Pamoja na hayo bado tunayo nia na wala hatujasahau kwa barabara ya Kijini. Isipokuwa tulikuwa tunaangalia mbadala wake, ingawa tukiulizwa na Mhe. Mwakilishi anasema bora tupite njia ile ile, lakini tulikuwa tunaangalia eneo jengine tuikate. Kwa sababu lengo la serikali siku moja wakati unapotaka kwenda Nungwi usipitie Mkwajuni tena, yaani kama unatoka Matemwe, basi upitie kwa chini baharini moja kwa moja mpaka Nungwi *(Makofi)*.

Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi wote kwa jumla tunawahakikishia kwamba lengo la serikali lipo la kuijenga barabara ile ya Kijini au Muyuni wenyewe wanavyoita, kwa ajili ya kuweka sawa. Hivyo nadhani Jimbo la Matemwe litakuwa ni miongoni mwa majimbo bora kwa barabara Zanzibar *(Makofi)*.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu ya Mhe. Waziri nimelazimika niulize swali moja la nyongeza. Katika utekelezaji wa ujenzi wa barabara za Pemba, ninaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya kueneza barabara za lami tena za uhakika kwa wananchi wa visiwa hivi vya Unguja na Pemba na wala bila ya upendeleo, pia zinajengwa katika hali ya ubora.

Katika kipindi cha miezi miwili iliyopita nilibahatika kufanyakazi ya Kamati zako Mhe. Mwenyekiti za Baraza na kutembelea Pemba na kuona ujenzi wa barabara ya Mtambile – Kangani. Kwa kweli tumeona inajengwa kienyeji na watu wanatumia zana zile za asili.

(a) Je, Mhe. Waziri katika ujenzi huu hivi sasa, ambapo tunataka barabara za kisasa, baada ya ujenzi huo nadhani tutapata zile barabara zenye mipasuko katikati?

(b) Yapo matatizo ya zana au vipi, kwa sababu hivi sasa watu wanatumia vijembe kongoroka katika ujenzi wa barabara kwenye karne hii ya 22?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara hizo zinajengwa katika huo mtindo ambao unaouona wewe na wala si kwa bahati mbaya. Kwa kweli ule ni utaratibu wa masharti ya huo msaada wenyewe kwamba wananchi nao washirikishwe katika ujenzi, kwa ajili ya kupata ajira kwa lengo la kupunguza umasikini.

Kwa hivyo, kuna kazi ambazo zinafanywa kwa mikono na nyengine zinatumia vifaa. Kwa mfano, hiyo barabara ya Mtambile – Kangani, tumekata vilima kuanzia Mtambile mpaka Mjimbini vya vifaa vya kileo na bado kuna kilima kimoja ambacho kinaitwa Kilima Tanga na sijui kama ninakosea jina au vipi, lakini nacho hicho tutakikata kwa kutumia vifaa vya kileo.

Hivyo, baadaye kazi nyengine zitafanyika kwa mikono ikiwemo kuchimba misingi pamoja na mambo mengine. Lakini lami itawekwa na itakuwa barabara nzuri, kwa sababu wataalamu wetu wamekwenda Kenya na Afika ya Kusuni kwa ajili ya kuangalia jinsi gani wenzetu wanatengeza barabara kwa kutumia utaratibu huo.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, leo tunazo kamati tatu, moja hii inayoendelea ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii na mbili zinazofuata. Kwa hivyo, tunaomba watu wasirudie pamoja na kuchunga muda, ili tuweze kumaliza.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana asubuhi ya leo kuniorodhesha kuwa mtu wa mwanzo katika kuchangia Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Ripoti hiyo ambayo imewasilishwa jana na Mwenyekiti wake Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata).

Kwanza napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, wajumbe wa kamati pamoja na makatibu wao kwa taarifa nzuri ambayo wamewasilisha katika Baraza hili tukufu.

Kwa kweli, mimi nilipata machache wakati nilipoisoma na nitaomba labda zaidi ni ulize maswali kuliko mchango. Katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ripoti imezungumza kuwa kunaupungufu wa Madaktari Bingwa kwa maradhi ya Saratani. Kwa hivyo, wananchi wanapata tabu na inawalazimu kwenda Dar-es-Salaam katika Hospitali ya *Ocean Road* kwa ajili ya kutafuta matibabu zaidi.

Sasa niulize mwaka jana wakati tulipokuwa tukichangia hotuba ya Mhe. Waziri tulimpa rai, kwa sababu kamati hii kipindi kilichopita na mimi nilikuwa mjumbe na tulipata nafasi ya kwenda Hospitali ya *Ocean Road*. Wenzetu katika taarifa yao walisema kwamba wanao madaktari wa kutosha katika Kitengo kile cha *Ocean Road*, yaani wanao madaktari kiasi 43 ambapo ni Mabingwa.

Lakini katika kuwahoji tuliwaambia mnaweza kutupatia madaktari hao kuja Zanzibar kwa ajili ya kutusaidia. Walisema naam tunao uwezo na wala bila ya kuharibikiwa tutakuwa tunao uwezo wa kutoa mabingwa wetu watatu mpaka watano, ili kuja kutusaidia ndugu zetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, shauri hili tulilileta hapa kwa kutumia kikao hicho. Napenda kuuliza je serikali imechukua hatua gani ili kuhakikisha tunawaomba wataalamu hawa ndugu zetu kutoka Tanzania Bara kuja kutusaidia, wakati na sisi tunajitayarisha kutafuta Madaktari Bingwa Wazalendo.

Vile vile jambo jengine ambalo linahusiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ni ahadi za serikali. Kwa kweli hapa Wajumbe wa pande zote mbili tulikuwa na maswali kuhusu chakula cha wagonjwa kwamba kunakuwa na mapungufu na pia namna gani wanapata chakula na mara ngapi? Mhe. Waziri alisema wanapata chakula mara mbili kwa fedha wanazopata.

Pia Waheshimiwa Wajumbe wakawa na wasi wasi hata huo mlo mmoja hawawezi kupata, pamoja na madeni kwa wale wanaopeleka chakula katika hospitali zetu. Kazi hii imeagizwa kamati hii ikafanye. Kwa bahati mbaya Mhe. Mwenyekiti wajumbe wa kamati hii hawakutuletea taarifa hizi. Kamati ya Ahadi za Serikali imevunjwa makusudi, ili kamati husika za wizara hiyo zikafanyekazi huko.

Sasa naomba niulize hii ahadi ambayo imetolewa na Mhe. Spika aliagiza kamati hii ikafanyekazi, kwa nini hawakuchunguza habari hii na kutuletea, ili kuhakikisha kwamba tulikwenda sisi wizarani na tumeona chakula safi, wanapata chakula kadhaa na madeni hakuna. Ripoti hii inayomapungufu ya aina hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ninayo mambo mawili tu kuhusu Vyuo vya Amali na Ufundi pamoja na kauli za Waheshimiwa Mawaziri kwamba katika Vituo vyetu vya Ufundi na Mafunzo ya Amali kuwa kila mkoa inatarajiwa kuwa na kituo cha aina hii.

Wenzetu wa kamati watatuhakikishia vipi, mpango huu walipokwenda wizarani wameambiwa ni lini kila mkoa itakuwa tayari imeshapata kituo hicho. Kwa sababu vituo viliopo hivi sasa kama kipo mjini na kumtoa mtu Jambiani au Pete ama Ukongoroni na kuja mjini ni gharama na wengine watakuwa hawana uwezo. Mafunzo haya ndiyo yanayolenga kuwasaidia wale ambao hawakubahatika kwenda vyuo vya juu zaidi, sasa kuwekwa kila mkoa vitakuwa vinasaidia.

Kwa hivyo, niulize namna gani atatuhakikishia sisi kuhusiana na ile kauli ya kila mkoa itapatiwa vituo vya mafunzo ya amali.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ni kuhusiana na mambo ya historia pamoja na magofu. Tumeona magofu yanatengenezwa vizuri sana, lakini katika magofu hayo kuna ukosefu wa wataalamu au watu wenye uzoefu wa kuelezea historia ya mahala husika. Mhe. Mwenyekiti, ukenda Mkamandume unapata mtu tu kuja kuelezea historia pengine anapotosha habari ya pale, ukenda pale Dunga pia hakuna mtu anayeweza kuelezea historia ya pale. Kwa hivyo, serikali imejipanga vipi kuhakikisha wale ambao tumewawekea vielelezo vya kwenda kuangalia tutawaekea watu ambao watakuwa wanaeleza historia sahihi ya mahala pale ili anapoondoka lile lengo lake alipate.

Mhe. Mwenyekiti, mfano mzuri hapa Kanisa la Mkunazini ni mahala pa historia lakini ukenda kuna mtu maalum wamejiwekea kwa lugha mbili mpaka tatu anawaeleza wale watalii wanaofika pale na wanafaidika na historia ya pale. Lakini unaweza kwenda kwenye magofu yetu hakuna watu kama hao. Mhe. Mwenyekiti, je, yule anayekuja kupata faida ya pale kwa sababu hapana maelezo anakosekana. Sasa serikali imejidhatiti vipi kuhakikisha sehemu kama hizo wanakuwemo watu wa kuweza kutoa taaluma kwa watalii.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Wizara ya Wanawake na Watoto nina suala moja tu. Mhe. Mwenyekiti, kuna mfuko huu wa JK na AK bado ni gumzo kubwa huko mitaani, ingawa serikali inasema imeshatoa pesa hizo, lakini namna zilivyotolewa pengine zimetolewa sehemu moja tu lakini wananchi wengi wanalalamika. Mhe. Mwenyekiti, wakati tukiuliza katika Baraza hili Mhe. Waziri alieleza kuwa zoezi hili limeanza kwa pilot na kweli katika Mkoa wangu wa Kusini limeanza sehemu ya Paje na Kizimkazi, wengine kote hawajapata. Katika Wilaya ya Kati ni Cheju na Chwaka sehemu nyengine hazijapa, Kaskazini “B” ni Bumbwini na Kitope, Donge ndio hivi juzi kidogo ndio wamepata tena kwa kelele. Kwa hivyo, sasa hivi tunaambiwa pesa hizi hazipo tunaambiwa zimekwisha. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niwaulize wenzetu wa kamati wamejikita vipi kulidadisi hili kwani hii tamaa ya wananchi na kufaidika na fedha hizi zitapatikana ili kuwaondolea matatizo yale ya MKUZA ya kupunguza umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii nami nikapata nafasi ya kuchangia mawili matatu katika ripoti hii ya Kamati ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza kamati hii chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ali Suleiman Ali Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kutembelea na kutupa taarifa mbali mbali zinazohusu wizara ambazo wanazitembelea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumzia maeneo matatu, moja ni la Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii eneo jengine linahusu Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na la mwisho ambalo kidogo litafanana na la Mhe. Mkema la Wizara ya Wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, katika taarifa ya kamati ambayo wenzetu wametuwasilishia katika kitabu hiki ukurasa wa 36 kifungu cha 2.6.31 kumezungumziwa suala la kuwasilisha kama mradi huko Wizara ya Fedha suala la kuzifanyia matengenezo nyumba za wazee Sebleni.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nataka niipongeze sana Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mara ya kwanza kubuni jambo kama hili ambalo pengine linaweza kuwa ufumbuzi wa tatizo la nyumba za wazee Sebleni. Kama unakumbuka Mhe. Mwenyekiti, jambo hili limekuwa nikilizungumza sana tokea nimeingia katika Baraza lako hili tukufu hadi kesho na kesho kutwa tunaondoka. Lakini nashukuru kwamba kelele zangu kidogo Wizara ya Afya wamezisikia na hatua inaonesha kwamba lengo ni kuona nyumba zile zinafanyiwa matengenezo. Hii ni hatua nzuri na inatia moyo, isipokuwa sasa niiombe sana wizara hii ikubali jambo hili kwamba nyumba zetu zile ambazo tumezianzisha kwa makusudi tu na muasisi wa nyumba zile mzee wetu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume ambaye mwezi huu tunaadhimisha kumbukumbu zake basi tuzihifadhi na tuzienzi kwa sababu ni nyumba ambazo ziko katika hali mbaya.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Fedha wakati ule tunakaribia alikuwa yuko nje nikenda nikamwambia Mhe. Waziri hebu ingie ndani, nataka nitoe maelezo haya nay eye mwenyewe akiwemo humu ndani, pamoja na kuwa sio wizara yake lakini wizara yake ni wizara mama ambayo inahusisha wizara zote kwa hivyo ni vyema wakati ule tunapojadili wizara hizi na yeye awepo. Kwa sababu mheshimiwa matatizo mengi yanatokana na fedha. Kwa hivyo, ujumbe nafikiri Mhe. Waziri umefika maana sasa Wizara ya Afya tayari wameshanawa, sasa niko katika wizara yako ni kuona kwamba *proposal* ya *project* hii ya nyumba za wazee Sebleni basi inachukuliwa hatua na matengeneze ya ujenzi wa nyumba zile unaanza kwa sababu nyumba ziko katika hali mbaya. Kwa hivyo, nawapongeza Wizara ya Afya kwa hatua hii sasa kazi iko kwa Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ukurasa wa 41 wa ripoti hii kutangazwa kwa Bodi ya Shirika la Magazeti ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa hapa inaeleza kwamba kamati tayari imeshaarifiwa kwamba Bodi ya Shirika la Magazeti ya Serikali limeshateuliwa kwa kufuata maelekezo ya sheria iliyotajwa hapa sheria Nam. 11 kifungu kidogo cha 1 ya mwaka 2008 na tayari Mwenyekiti pamoja na wajumbe wake wameshatangazwa tayari kwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, lengo la sheria hii ni kuona kwamba Shirika la Magazeti ya Serikali likiwemo Gazeti la Zanzibar Leo linakuwa la kisasa na linaendana na ushindani. Kama tunavyojua kwamba sasa hivi kumekuwa na wimbi la magazeti ya watu binafsi. Tumepitisha sheria hii Nam. 11 cha sheria hii ya kuanzisha magazeti lengo ni kwamba gazeti letu hili au na magazeti mengine yatakayoanzishwa na serikali yaendane na wakati ikiwemo kuanzisha kwa gazeti la rangi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi gazeti letu la Zanzibar Leo tayari kila siku ya Ijumaa limekuwa likitoa gazeti la rangi ambalo linapendeza kweli kweli, sote tutakubaliana na hilo kwamba Gazeti la Zanzibar Leo la Ijumaa linakuwa tofauti na magazeti yale yanayotolewa siku nyengine. Mhe. Mwenyekiti, lengo la Shirika la Magazeti ya Serikali ni kuona kwamba siku zote linatoa magazeti ya rangi ili liendane na ushindani. Lakini sio gazeti la rangi tu ikiwemo na vitendea kazi na ripoti nyengine ambazo zimo katika taarifa.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo kwamba sheria iliyopitishwa imeipa mamlaka shirika lile kwamba liwe ni bodi *cooperate* liweze kujitegemea, liweze kufanya mambo yake. Lakini kwa kuwa shirika hili limeanzishwa hivi karibuni maana yake bado inaonekana uwezo wake ni mdogo na linahitaji kwenda kibiashara, linahitaji nyenzo, pia linahitaji lile lengo lililokusudiwa la kuliboresha liwe bora ili liweze kutimia. Pia linatahitaji kuwe na mabadiliko kutoka pale ambapo lilikuwa chini ya Idara ya Serikali sasa hivi limekuwa ni shirika la kujitegemea lazima mabadiliko yaweze kuonekana. Mabadiliko haya hayawezi kuja hivi hivi tu bila ya kuliwezesha shirika hili.

Kwa hivyo, bajeti ya mwaka jana Shirika hili la Magazeti ya Serikali bajeti yake haikuonesha mabadiliko yoyote. Bajeti yake ilikuwa ni sawa sawa na ile bajeti iliyokuwa ya serikali. Kwa hivyo, hebu tujiulize katika hali kama hiyo mabadiliko hayo yanawezekana, lile lengo la serikali la kufanya mabadiliko linawezekana. Kwa ujumla ni kwamba mabadiliko hayawezi kuja katika hali ile ile. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri na zaidi Mhe. Waziri wa Fedha ambaye nilimuomba awepo katika bajeti hii tutenge mtaji maalum wa kuliwezesha shirika hili, na mtaji peke yake ndio utakaoweza kulitoa hapa lilipo na kulipeleka katika eneo jengine.

Lakini ikiwa bado tutakuwa tunalibana, bado tunalipa bajeti zile zile za mwanzo maana yake lile lengo lilokusudiwa haliwezi kufikiwa. Kwa hivyo, nimesema nilizungumzie hili ili Mhe. Waziri alifahamu na Mhe. Waziri wa Fedha ambaye yupo na bajeti kesho kutwa kwamba safari hii tunataka tuone mabadiliko ya bajeti ya Shirika hili la Magazeti ya Serikali, tuliwezeshe ili liweze kujiendeleza. Mhe. Mwenyekiti, gazeti linahitaji kununua mtambo wa rangi wake mwenyewe binafsi kwa ajili ya kuchapisha magazeti ya rangi na kuendesha biashara liweze kujitegemea. Linahitaji kuwa na jengo la kisasa kwani sasa hivi jengo la Gazeti la Zanzibar Leo limekuwa kama gofu ukenda halipendezi, linahitaji vyombo vya kisasa, linahitaji wafanyakazi wake wawezeshwe kimaslahi.

Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani mfanyakazi wa idara hii alikuwa analipwa leo hii, lakini tayari tumeshafanya ni shirika bado maslahi ya wafanyakazi yanabakia pale pale. Hilo haliwezekani lazima na wafanyakazi na wao waone mabadiliko kwamba kweli tulikuwa idara sasa hivi tumekuwa ni shirika. Kwa hivyo, naomba mabadiliko haya yawezekane na haya yote hayawezi kuja bila ya kuliwezesha hili shirika, na shirika hili tutakapoliwezesha basi litaweza kujitegemea na hatimae serikali ikaondosha mkono wake likaweza kwenda mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie na Wizara ya Kazi, Vijana Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo kwamba nitazungumzia moja ambalo na Mhe. Mkema alilizungumzia suala la fedha za mfuko wa JK na AK.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tumeanzisha hili kwa nia nzuri na wananchi wakalipokea lakini kwa masikitiko makubwa kwamba lengo la kuanzisha mfuko huu haukufikiwa, kwa sababu fedha zile ambazo zimetengwa hazikuwafikia wananchi ipasavyo. Mimi nasema hazikuwafikia wananchi ipasavyo kwa sababu wananchi wa Jimbo langu la Magomeni hakuna mwananchi hata mmoja aliyepata mkopo huo hadi leo hii tunazungumza. Zilitoka fomu katika shehia zangu mbili mara ya mwanzo hakuna hata mtu mmoja aliyepata na hivi karibuni zimetoka fomu nyengine katika shehia nyengine lakini hakuna hata mwananchi mmoja aliyeweza kufaidika na mkopo huo. Kwa hivyo, kwa kweli tuna masikitiko makubwa juu ya taratibu hizi ambazo zinakwenda juu ya mkopo huu. Sasa hivi tunapata taarifa kwamba fedha hizi zimekwisha.

Kwa hivyo, ni jambo la masikitiko na kama jambo lipo na limetendeka basi ni wajibu wetu tulizungumze, hatuna jengine la kufanya. Mhe. Mwenyekiti, sisi kama wawakilishi wa wananchi kazi yetu ni kuzungumza na kusema, utekelezaji ni wa serikali yenyewe, limetekelezwa ndivyo, halikutekelezwa haya. Lakini nataka nihakikishie kwamba zoezi zima la mfuko wa JK na AK halikwenda vizuri. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nitaanza na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii halafu nitakuja na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na kumalizia na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze kamati hii kwa kazi yake kubwa iliyofanya na kupitia wizara zake mbali mbali ili kujua na kutafiti na kupata habari zilizokuwa na matatizo katika mawizara haya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia nitaanzia kwenye ukurasa wa 32 kifungu cha 2.3 utekelezaji wa matumizi ya fedha. Mhe. Mwenyekiti, kuidhinishwa kwa fedha katika Wizara ya Afya shilingi bilioni 10,089,300,000/- kwa bajeti ya wizara hii. Kwa hivyo, utakuta mheshimiwa pamoja na hayo fedha hizo zimetoka kama bilioni 6,369,191,872/- kwa hivyo utakuta Mhe. Mwenyekiti, utoaji wa fedha kama hizi za bajeti ambazo zinakuwa hazikamiliki inakuwa inaleta mapungufu makubwa katika huduma mbali mbali za Wizara ya Afya.

Mara nyingi ndio huwa tunasema bila ya kujua hii bajeti kwamba kuna makero ya upungufu wa magodoro yaliyokuwa safi, vitanda vilivyokuwa vizima. Kwa hivyo, ukosefu wa bajeti hii kukamilia hayo ndio yanayojitokeza. Kwa hivyo, ningemuomba anayehusika na bajeti hii kwa wizara hii akaiangalia zaidi ili kukamilisha fedha zote za bajeti zinazotolewa au kama kuna uwezekano wa kuongeza zikaongezwa ili kupunguza hayo matatizo yanayojitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, kama inavyoeleweka baadhi ya watendaji wa Wizara ya Afya mara nyingi huwa wanatoka wanakwenda kufanya kazi katika nchi jirani. Mimi hili sitegemei kama ni kasoro ya bajeti sijui ni kitu gani kinachosababisha hivi. Kuna baadhi ya watendaji wengine huwa wastahamilivu wanafanya kazi kiuzalendo nitapenda kuwataja kuna Dk. Jidawi, Dk. Malik, Dk. Mwakwetu na baadhi ya wengine siwajui lakini huwa wanajitolea kwa dhati kufanya kazi kizalendo. Kwa kulingana na hili Mhe. Mwenyekiti, kama itaboreshwa hii bajeti nafikiri hata wengine wanaweza kuvutika kuhisi maslahi yao watayapata kikamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba wizara hii iangaliwe sana kwani ni wizara tegemezi kwa wananchi wetu zikiwemo na wizara nyengine kama Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kweli zinakuwa kipaumbele zaidi kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika ukurasa wa 34 kifungu cha 2.6.13. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikipongeze hiki kitengo cha ZAYEDESA kwa kuwepo kila eneo lenye utata kwa kushirikiana na AMD kutatua matatizo ikiwemo chumba cha wazazi katika Wilaya ya Micheweni. Mimi nawapongeza sana kwa sababu mara nyingi huwa nakisikia katika shughuli mbali mbali za kimaendeleo za ushirika huwa kinajitokeza kuwasaidia wananchi wetu kuhamasisha na kuwasaidia misaada tofauti ili vipate viende mbele vikundi vya kijamii. Kwa hivyo, kitengo hiki namuomba Mhe. Waziri kama kuna mipango yoyote ya kupatiwa wafadhili kiisaidie ili kiboreshwe zaidi kwa wana vikundi vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye kifungu cha 2.6.17 mswada wa marekebisho ya sheria ya madawa ya kulevya. Kama inavyoeleza katika maandishi kuwa mswada huu umeshapitishwa na umeshatiwa saini kwa hivyo kuna haja kitengo husika kiharakishe kufanikisha kazi na utendaji wa kitengo hiki ili kupunguza lile wimbi kubwa la vijana wetu ambao wanashiriki madawa ya kulevya na wengi wao kupoteza maisha na wengine kupoteza nguvu za kufanyia kazi.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri kitengo hiki kiangaliwe sana kwa sababu sasa hivi vijana wengi wameshakuwa na hali mbaya na wafanyakazi wetu wengine ambao walishiriki kwenye vitendo hivi tumekuwa hatuna wafanyakazi wenye uwezo wa kufanya kazi kwa nguvu zao. Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba kikaangaliwa sana ili kiweze kuboreshwa ili kuhakikishwa suala hili linapungua au linaondoka kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Afya kwa juhudi yake kubwa iliyochukua kwa kumpeleka kwenye matibabu nje ya nchi Bi. Riziki. Hii mara nyingi tulikuwa tukiilalamikia hapa Barazani kwa kuwa mfanyakazi huyu alikaa kipindi kirefu alikuwa akisumbuliwa na ugonjwa aliokuwa nao, kwa hivyo baada ya kupeleka malalamiko yetu na kelele zetu nyingi leo wizara hii imechukua juhudi ya kumsafirisha ili kwenda kupata matibabu. Kwa hivyo, kwa hili nawapongeza sana wizara hii na namuomba Mhe. Waziri aliangalie kwa kina hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 41 kifungu cha 3.5.1 Wizara ya Habari, Utamaduniu na Michezo. Kwa kuwa vifaa vya digital kwa ajili ya redio na televisheni na utangazaji vimeshawasili hapa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, kuna haja sasa hivi vitengo hivi kupewa mikakati ya dhati ili baada ya kwishakuvifunga vifaa hivyo matangazo vya vyombo vyetu yawe ya kuvutia na yawe yanakwenda vizuri. Kwa sababu sasa hivi utakuta baadhi ya wakati kama Sauti ya Tanzania Zanzibar huwa inakatisha matangazo yake ghafla hujui tatizo ni nini. Kwa hivyo, utakuta tofauti na baadhi ya vyombo vyengine vya binafsi wewe uwe wapi unaona habari mbali mbali katika televisheni . Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa vifaa hivyo vimeshakuwepo ningemuomba Mhe. Waziri vikafungwa vikaweza kutumika wananchi wetu wakafaidika na vyombo vyetu hivi.

Mhe. Mwenyekiti, kama inavyoeleweka Sauti ya Tanzania Zanzibar mara nyingi ikipata wasanii ikirikodi michezo huwa inafurahisha sana wananchi wetu wanapata kusikiliza. Mhe. Mwenyekiti, tunayo michezo mbali mbali ambayo inavutia ya kina Mashaka, Makombora hili linaleta burudani nzuri kwa wananchi kama wakisikia michezo yao. Ukija kwenye televisheni kuna michezo ya marehemu Dk. Ayoub hiyo nayo ni kivutio zaidi kuliko hata ile michezo ya Nigeria. Kwa hivyo, kama tutaimarisha vifaa hivi na studio zetu zikawa na michezo kama hiyo itakuwa na mvuto mzuri kwa watizamaji na kuleta faida kwa wageni wanaokuja katika nchi yetu. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri hapa akaliangalia vizuri zaidi ili tuwaka na vyombo vya habari vya kileo.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 45 kifungu cha 4.3.2 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Mwenyekiti, kipengele hiki kimezugumzia suala la kuvipatia viti na meza skuli za majimbo. Hili kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kuna upungufu mkubwa wa kupata meza na viti kwenye maskuli yetu ya majimbo mbali mbali. Imekuwa ni usumbufu kwa watoto wa sekondari ambao wanakaa chini, sio vizuri mtoto wa sekondari leo kuchukua busati akapeleka skuli kwa ajili ya kukalia darasani. Kwa hivyo, ni vyema ukarabati huu wa kupatiwa viti na meza maskuli yetu unahitajika.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kama kuna mipango mengine ya kuboresha meza hivi inakuwa vizuri kwa sababu baadhi ya maskuli mengi kuna yale madeski utakuta watoto wanayavunja kiholela. Kuna baadhi ya vijana wetu ambao hawapendi maadili mazuri huwa wanaingia baadhi ya maskuli na kuvunja madeski kwa makusudi, huwa wanatoa mbao za juu, wanatoa mbao za kukalia. Kwa hivyo, hili linasababisha kuwa na upungufu wa madeski juu ya jitihada yote wanaochukua viongozi wa maeneo wa kuweka ulinzi na kutisha lakini huwa wanashindwa.

Kwa hivyo, ningeiomba wizara hii kama kuna mbinu nyengine mbadala ili kubadilisha vikalio hivi vya maskuli waweze kubuni aina nyengine yoyote ili vifaa hivyo visiweze kuharibiwe kama ilivyo sasa hivi. Kama litakuwepo hilo namuomba Mhe. Waziri alitizame hili zaidi ili kama itakakuwepo fani hiyo ijaribu kufanya hivyo ili kuondosha upotevu wa meza hizi za skuli zinazopotea kila leo.

Nikija katika ukurasa wa 46.4.7 Uimarishaji wa Elimu ya Lazima Skuli. Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili la kuimarisha elimu ya lazima katika skuli zetu, sasa hivi kwa kweli kuna upungufu mkubwa wa wanafunzi wa darasa la kumi kwenda la kumi na moja, kuwa baadhi yao wengi katika masomo ya ziada huwa wanasomeshwa masomo ya sayansi.

Lakini ukienda katika skuli zao kuna upungufu wa walimu wa sayansi pamoja na vifaa vya kufundishia, mitihani inayokuja yanakuwemo masomo hayo. Kwa hivyo, utakuwa baadhi ya wanfunzi wale wachache kwenye madarasa wanaofaulu masomo ya sayansi, kwa hivyo, yakitoka matokeo kubakia skulini mwao kwa kuendelea na masomo hayo utakuta walimu hawana. Kuna skuli chache tu ndio utakuta wanafunzi wakiwemo 50 basi 10 au 20 wamefaulu masomo ya sayansi, lakini kutokana na upungufu wa walimu na vifaa hivyo wanakuwa wanashindwa kuendelea zaidi.

Je, Mhe. Waziri atakuwa na mpango gani kwa baadhi ya wanafunzi ambao wamefaulu masomo ya sayansi kuwatafutia madara ili kila skuli akachukua waliofaulu wale akawatengea madarasa maalum na kuwatafutia walimu wenye fani na vifaa ili kujiendeleza na masomo yale ya sayansi, ili waweze kujiweka tayari katika mitihani kwa masomo yale yanapokuja.

Kwa hivyo, hili ningemuomba Mhe. Waziri akaliangalia sana, kumekuwa na usumbufu mkubwa sana. Kuna wazazi wengi sasa hivi wanahangaika kwa kuona baadhi ya watoto wao skuli wanazosoma hakuna walimu na vifaa hivyo na wao wana fani ya sayansi.

Sasa hapa ningemuomba Mhe. Waziri afanye juhudi zake zote kama nilivyosema kuwatafutia madara kwa kuwakusanya wale ili na wao wapate masomo yao waliyoyachukua.

Mhe. Mwenyekiti, pia ningeomba aangalie zaidi maslahi ya walimu. Kwa kweli walimu wamesubiri kwa muda mrefu, sasa na wao wangeangaliwa zaidi ili waondokane na usumbufu wa kulalamika kila mara kuwa hawapati maslahi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mswada ripoti hii imeshazungumzwa na wajumbe wengi na wengine pia wanataka kuichangia, basi mimi niiunge mkono sina pingamizi nayo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii nikachangia kidogo katika ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyotangulia Mwenyekiti wa Kamati hii kutaja majina ya wajumbe na mimi akanitaja kuwa nimo katika kamati hii kwa hivyo, ni kweli nathibitisha kuwa kweli mimi ni mjumbe wa

kamati hii na yote yaliyoandikwa kwenye ripoti hii ni yetu. Sasa haitakuwa vyema kama sitazungumza mawili matatu yale ambayo ya kuishauri wizara au ya kutaka kujua.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianzie na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, nataka nianzie kwenye ukurasa wa 35. Kwenye ukurasa huo wa 35 kifungu 2.6.19 katika suala la kupeleka *Solar Power* Makoongwe. Hili leo asubuhi Mhe. Waziri kalisema alipokuwa akijibu swali la *solar power* katika vituo vya afya vya visiwa. Kasema kuwa hivi vifaa viko tayari vinasubiri nyumba tu zimalizike na zikimalizika basi tayari *solar power* itafungwa.

Kwa kweli mimi nashukuru kama hivi ndivyo ilivyo, na kwa sababu lililo baharini madamu maji yanajaa lisubiri ufukweni kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hili nalisubiri ufukweni tukijaaliwa kwa sababu maji karibu yatajaa, nyuma zitamalizika zile kujengwa na tutaliona jinsi gani litavyotekelezwa. Naamini kwa kazi nzuri anayoifanya Waziri wa Afya basi hili litakuwa na hapendi kusema uongo kama alivyosema mwenyewe asubuhi.

Lakini jambo jengine ninalotaka kidogo niligusie ni suala la kusomesha wafanyakazi. Suala hili lina pande mbili, lina kusomesha wafanyakazi waliokuwa tayari wamo kazini, lakini pia lina suala la kusomesha wafanyakazi wapya ambao wanatarajiwa wachukuliwe kazini. Lililoelezwa katika ripoti hii ni wafanyakazi wale waliomo kazini kupewa mafunzo zaidi.

Mimi nataka nizungumzie hili la pili ambalo halikuzungumzwa katika ripoti hii lile la wale watu wanaotayarishwa kuwa wafanyaka wa Wizara ya Afya baadae, katika chuo chetu cha Mbweni.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili kidogo lina utatanishi, kwa sababu kuna watu waliomaliza muda mrefu sasa na hawajapata ajira, ukiachilia mbali kuwa tuna upungufu mkubwa. Hili linawezekana ikawa ni tatizo la fedha kama tunavyoambiwa kila siku, lakini pia inawezekana kuwa bado kuna mambo ya hapa na pale hayajakaa vizuri. Lakini hasa lililonigusa zaidi ni kuwa mtu akimaliza mafunzo anatakiwa apatiwe vyeti vyake vya mafunzo. Sasa mpaka hivi karibuni sijui leo na jana, lakini mpaka hivi karibuni wahitimu wa chuo kile walikuwa vyeti vyao hawajavipata, sijui suala hili ni kitu gani kilichozuia vyeti vile wasipewe.

Kuna taarifa kuwa hata hawa waliokuwa wakipewa wakati ule wa sherehe basi hupewa kwa mkono wa kulia na wakanyang'anywa pale pale kwa mkono wa kushoto. Wakishapokea kuna pahala wakenda wakavipeleka. Sasa sipendi kusema kuwa hili ni kudanganya watu, kwa sababu watu wale wataona watu tayari wanafunzi wamepewa vyeti vyao, lakini wakiondoka pale hakuna mwenye cheti.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kama hivyo ndivyo inavyofanywa, basi kuna haja ya marekebisho, kuwa watu wakimaliza mafunzo yao basi wapewe vyeti vyao, serikali ina uwezo wa kuwaajiri iwaajiri, serikali haina uwezo wa kuwaajiri mtu tena atapie nafsi yake, akipata pahala pa kuajiriwa aweze kuajiriwa, kuliko mtu kumuweka katika kibafute hujui ndani mna ngapi mkononi zilizofumbatwa.

Himi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, ni moja katika mambo ambayo yalinigusa sana na nikafikiria ingekuwa vizuri likachukuliwa hatua za kufaa.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika ukurasa wa 36 kuna kulipwa fidia watu 355 walioumia mikarafuuni tangu mwaka 1999 mpaka 2008. Mhe. Mwenyekiti, suala hili kwa kweli linanisononesha, linaniumiza ndani ya nafsi yangu na laiti ningekuwa na uwezo japo kuikopesaha ningeikopesha serikali ikawalipa watu hawa. Kwa sababu gani?

Mhe. Mwenyekiti, watu hawa wamechuma karafuu wakaanguka ndani ya kutoka kwenye mikarafuu, kila mmoja kaumia na maumivu yake aliyoyapata. Karafuu walizozichuma kwa miaka hii yote tayari zimeshauzwa na zimeshatumiwa. Nadhani hizi karafuu zilizochumwa zikauzwa ilikuwa kitolewe hiki kidogo ambacho wanastahiki walipwe, lakini karafuu zimechumwa imekuwa yule mchumi mndu aliyemsema Mhe. Najma Khalfan Juma. Wakati wa kufyeka basi yeye ndiye anayewekwa mbele kufyeka, lakini wakati wa mafao yeye anawekwa kipembeni huko asije akachinja watu.

Kwa hivyo, hili Mhe. Mwenyekiti, nadhani kuna haja ya kulichukulia hatua za dharura badili ya kungoja mpaka tufike katika hatua za kawaida ambazo zinaonekana zitachelewa sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikikwita Mhe. Spika nichukulie tu hivyo hivyo, pengine ni dua hiyo nakuombea. Mhe. Mwenyekiti, hapa katika ukurasa wa 37 kuna suala la Mkoani *Abdalla Mzee Hospital* la *red cross* kutumiwa kama wauguzi. Nataka nimthibitishie Mhe. Waziri kuwa bado suala hili linaendelea, sasa sina hakika kama kuna hatua alizozichukua mpaka sasa au hakuna.

Niingie katika wizara nyengine Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Nataka nianzie kwenye ukurasa wa 40 ambako kuna mradi wa uchapishaji wa kamusi ya Kiswahili, sijui la Kiswahili au ya Kiswahili sina hakika. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kamusi hili lina umuhimu mkubwa sana hasa hivi sasa. Kwa sababu kuna makamusi yaliyokwishatayarishwa mengi na watu mbali mbali na vyombo mbali mbali, lakini sisi kama Wazanzibari, kama watu ambao lugha yetu ya kwanza ni Kiswahili, basi kamusi yetu tunaitarajia itakuwa nzuri kuliko kamusi zote zilizotangulia ambazo walioziandika wengi wao si lugha yao ya kwanza Kiswahili.

Kwa hivyo, suala hili la kamusi naomba lifikie pahali tukabidhiwe kamusi tujue kuwa sasa tuna pahala pa kuangalia tukihitaji kuangalia neno likoje na lina maana gani.

Nikitoka hapo nirukie katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, wizara yangu. Wizara yangu naanzia na ukurasa wa 45 katika suala la samani ambalo sitaki niliseme sana. Kwa sababu hata leo asubuhi niliuliza swali la nyongeza na Mhe. Waziri akanijibu akataka tushirikiane nimwambie ni skuli gani. Lakini hapa mimi sina haja ya kutafuta sana hizo skuli. Kwa sababu kuna skuli nakaanayo jirani sasa hivi ina darasa la tano, imejengwa mpya kabisa kwa ufadhili wa Hoteli ya Fundolagon.

Banda la kwanza lilipofikia wakati wa kumalizwa lilimalizwa na wizara, lakini bahati mbaya halikupatiwa samani. Banda la pili mwaka wa pili sasa, huu wa 2010 ni wa tatu, lilifikia sehemu ya kumalizwa na wizara miaka miwili nyuma lakini bado wizara haijalishughulikia hili banda. Si hivyo tu, yule mwalimu hana hata kiti cha kukalia na bahati mbaya mimi nyumbani kwangu sina viti angalau ningewaazima, mimi mwenyewe natandika chini nikikaa.

Mhe. Mwenyekiti, lile alilonilomba Mhe. Waziri asubihi kwenye swali lake naomba kwanza aanzie na hiyo baadae nitamtafutia na nyengine.

Nikitoka hapo katika ukurasa wa 46 katika uimarisha wa elimu ya msingi naona hili nishamwambia kabisa Mhe. Waziri kwa hivyo, najua atalichukulia hatua.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nikija ukurasa wa 55 katika wizara hii hii ya elimu, labda nigusie kidogo katika ziara yetu ya Dar es Salaam, lakini pia niunganishe na nililoliona jana kwenye televisheni. Suala zima la mafunzo ya ufundi stadio (*VETA*) tulitembelea tukaona mambo mbali mbali na tukashauri tulipokwenda kwenye kamati. Jana nikasema kumbe hii *VETA* ina matawi yake sehemu mbali mbali kule Tanzania Bara, ilioneshwa *VETA* Kigoma kwenye televisheni.

Sasa *VETA* Kigoma inaonekana mambo yake ni mazuri zaidi kuliko hiyo ya Dar es Salaam. Sasa nawaombea tu kamati hii watakaokuwa huko baadae wakaiangalie na *VETA* Kigoma tukijaaliwa, wawezeshwe wende wakaiangalie.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika suala la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi ambalo pia tulilitembelea Dar es Salaam. Najua na Zanzibar kuna Mfuko wa Mikopo wa Wanafunzi, sasa hapa nina kitu nataka nijuilishwe. Kuna mawasiliano gani kati ya vyombo hivi viwili vinavyofanya kazi moja? Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi Tanzania na Mfuko wa Mikopo wa Wanafunzi wa Zanzibar, kuna mawasiliano gani? Haitokezei mwanafunzi akakopeshwa kule akakopeshwa na huku, au kuna utaratibu gani unaofanywa kuhakikisha kuwa mtu anapata kukopa sehemu moja tu na hakopi sehemu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema haya mambo machache. Kwa kweli wizara hizi zinafanya kazi nzuri sana zote, pamoja na hiyo ya Wanawake na Watoto ambayo sikusema kitu, kwa sababu watu wengi wamezungumzia mfuko wa AK na JK. Mimi sitaki niutaje tena.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, linalojitokeza kadiri tunavyokwenda kuangalia shughuli za wizara hizi ni tatizo kwanza la ufinyu wa bajeti, lakini pili la upatikanaji mzuri wa fedha katika mawizara haya.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali kwa sababu wizara hizi zote zina umuhimu wake, kama Wizara ya Elimu tunaambiwa elimu ndio ufunguo wa maisha, Wizara ya Afya ndio inayofanya hayo maisha yapatikane na hao wanafunzi wasome, walimu waweze kusomesha na watu wengine waweze kufanya shughuli mbali mbali za taifa wakiwa katika hali ya uzima.

Wizara ya Wanawake na Watoto na Afira, watu hao wakishakuwa wazima, wakishasoma wanataka kuajiriwa, hawa ndio wenye mipango mbali mbali ya ajira na mambo mengine, ukiachilia ajira hizo za masomo, lakini kuna na ajira za vikundi mbali mbali, pia nazo zinahitajika zifanywe vizuri. Mwisho na Wizara ya Habari nayo ina habari, ina michezo, ina utamaduni, mambo ambayo yote nayo yana umuhimu wake na Wizara ya Elimu ndio niliyotangulia kuisema kuwa elimu ni ufunguo wa maisha.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba tu serikali wakati inapofanya ugavi wake wa hicho kinachopatikana au kinachotarajiwa kupatikana, basi wizara hizi ziangaliwe kwa jicho maalum ili ziweze kutekeleza yale mambo yote muhimu na tuweze kufaidika katika shughuli mbali mbali. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya dakika kumi ambayo umeniidhinisha. Na naomba nichangie moja kwa moja na nianze kwenye Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo ambayo yamezungumzwa na kamati nataka nitoe pongezi. Moja ni malipo ya fedha za wafanyakazi kwenye kambi za kipindupindu. Hoja hii mwaka jana ilikuwa ndio hoja yangu kubwa na mara hii nilidhamiria kwenye bajeti niwe mkali sana. lakini kama kamati imegundua kuwa watu wale wamelipwa napongeza na naishukuru sana wizara kwa jitihada hizi. Na kama kuna watu bado hawajalipwa naomba wamalizwe kabla ya bajeti nisije nikawa mkali tena.

Mhe. Mwenyekiti, jengine Afisi ya Mkemia Mkuu. Nimejaribu kutafuta sikuiona, ni miongoni mwa hoja yangu ya pili ambayo inanipa tabusana, kwamba afisi ile iimarishwe lakini zaidi Mkemia Mkuu aliyekuwepo athibitishwe na apewe maslahi yake. Hili nimekuwa nikilisema sana na kwa kweli sijaliona utekelezaji wake. Namuomba Mhe. Waziri afanye jitihada zake Mkemia Mkuu aliyepo athibitishwe na maslahi yake apewe.

Jengine ni changamoto moja ambayo kamati wao wamesema kuhusu maslahi ya wafanyakazi. Mhe. Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba wafanyakazi wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu, mshahara mdogo. Juzi nimesikia nchi moja huko nje madaktari waligoma kwa muda wa wiki nzima, serikali ikalazimika kuwatoa madaktari wa kijeshi kuwasambaza vituoni. Walikuwa wakidai nyongeza ya asilimia mia sita. Kwa sababu walikuwa wanapewa dola mia moja rais akatangaza kupewa dola mia sita haraka sana. Sasa tuone umuhimu wa wafanyakazi madaktari kwamba wamegoma hatimaye nyongeza yao imeongezwa kwa asilimia mia tano,

Mhe. Waziri nakuomba sana uhakikishe kwamba maslahi ya wafanyakazi wetu yanaongezwa na kuzingatiwa na hili ndio jambo pekee ambalo litapunguza uhaba wa wataalamu wetu.

Mhe. Mwenyekiti jengine ambalo ningepongeza ni ujenzi wa nyumba za madaktari hasa katika visiwa. Nikweli Shamiani nyumba imejengwa nzuri, Makoongwe ipo, sasa suala la kufunga *solar power* ni jambo la kuzingatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jambo ambalo linanisikitisha ni malipo ya watu walioanguka mikarafuu, nadhani sasa *ZSTC* sababu ya kutokuwalipa haipo. Kwa sababu deni lao la shilingi bilioni nne na Wizara ya Fedha lilimalizika. Kwa hivyo, tusingependa kusikia kwamba watu hao hawajalipwa hadi kufikia wakati wa

bajeti. Kwa sababu serikali pesa zao imewalipa hatuelewi kwa nini watu hawa wasilipwe pesa zao za kuanguka mikarafuu. Mhe. Mwenyekiti, hili kwa kweli tungeomba lisifike wakati wa bajeti watu hao walipwe.

Jengine ambalo ningechangia haraka harana ni matibabu ya watoto wagonjwa wa moyo Israel. Ningetaka Mhe. Waziri anifahamishe ni muda gani mtoto huyu huchukua hadi kupelekwa nchini Israel? Hivi karibuni mgonjwa kutoka jimboni kwangu mtoto mdogo aliletwa hapa na madaktari wakapendekeza kwamba, kwenye safari ya mwanzo kabisa mtoto huyu angepelekwa kwa sababu hali yake mbaya. Akatengezewa safari lakini hadi leo mpaka kufariki kwake hakupelekwa, huku tukiwaona watu wengine ambao walikuja baada yake wakapelekwa haraka kuliko yule.

Sasa ningependa kujua ni muda gani huchukua mgonjwa kama huyu kupelekwa nje? Na kwa nini maelekezo ya madaktari yalisema huyu apelekwe haraka na wakachukuliwa wengine kupelekwa kuliko yule ambaye madaktari walipendekeza.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni ugonjwa wa kiharusi ambao inaonekana kwamba Zanzibar hautibiki na badala yake wagonjwa huchukua fedha nyingi kupeleka nje. Tunaambiwa mgonjwa mmoja hugharimu zaidi ya shilingi milioni kumi na tano. Sasa ushauri wangu ni kwamba, tungejitayarisha kutafuta vifaa na wataalamu hapa Zanzibar ili kupunguza gharama ya fedha ambayo tunaipeleka nje.

Jengine ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kwamba Mhe. Waziri atufahamishe basi, bajeti mbili mfululizo tuliambiwa kwamba Wizara ya Elimu itajenga skuli za sekondari kila wilaya. Bahati nzuri Jimbo langu la Kiwani ndipo ambapo ilichaguliwa kujengwa ile sekondari moja ya wilaya, hatua hii imefikia wapi na kwa nini hatujaelezwa kwenye kamati hii.

Jengine ni ahadi za Wizara ya Elimu kwamba skuli nyingi zitapatiwa kompyuta, limetajwa hili zaidi ya mara nne kwamba Mwambe na Kiwani Sekondari watapatiwa kompyuta. Sasa ningetaka nijue ni lini suala hili litatekelezwa.
Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nipongeze tu, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa kuamua sasa kujiimarisha. Tangu juzi tulipokuwa na jambo muhimu la Mswada wa Sheria ya Kura ya Maoni walikuwa wakitoa *live* matangazo yale na kwa kweli huo ndio utawala bora na ndio wajibu wa vyombo vya habari. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nakushukuru kunipa nafasi hii kutoa maelezo machache kuhusu maswali ambayo yamejitokeza katika Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru mwenyekiti wa kamati hii pamoja na kamati yake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya wakati wa kamati hizi walipopita katika wizara zetu. Kwa kweli wametusaidia sana kwa kutupa ushauri na kutuelekeza na ninaamini kwamba maelekezo yao na ushauri utatuwezesha kufanya vizuri katika mwaka unaofuata.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wizara yangu imepata maswali na imepata maelekezo mbali mbali kama walivyoeleza wajumbe, na nianze tu na swali la Mhe. Haji Mkema Haji ambaye alizungumzia masuala ya Vyuo vya Amali. Tulisema kwamba kila mkoa tunatarajia kujenga Chuo cha Amali kimoja kama vile ambavyo tumevijenga sasa hivi Mkokotoni na Vitongoji.

Suala hili linadhaminiwa na Benki ya *ADB* na kwa bahati nzuri ni kwamba sasa hivi tuna utaratibu wa kuandaa mradi mpya baada ya kumalizika mradi ule ambao tayari umekwisha muda wake. Tunafanya mazungumzo na *ADB* ili kuona kwamba mradi mpya unaingia katika hatua ya utekelezaji.

Labda niseme tu kwamba sasa hivi hatua iliyofikiwa ni kuzungumza na *ADB* na kuandika *proposal* ya mradi huu na mara tu, tutakapokubaliana na *ADB* basi nadhani mradi huu utaanza kufanya kazi kama vile mwanzo. Napenda niwaeleze wajumbe kwamba *ADB* wamevutiwa sana na vituo vile ambavyo tumevijenga na vituo hivi wanaviita kama ni sampuli kwa nchi za Afrika.

Mhe. Mwenyekiti, siwezi kusema kwamba lini mradi huu utaanza, lakini niseme tu kwamba mara baada ya kukamilika makubaliano nadhani tutaanza utekelezaji wa mradi huu.

Kuhusu suala la magofu Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema mjumbe ni kweli kwamba tumekuwa tukiyatengeneza magofu na kuyatunza kwa lengo la kuendeleza utamaduni na historia yetu kwa vizazi vijavyo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda niwaeleze tu kwamba, wizara yangu tayari imeshachukua hatua mbali mbali ya kuyaendeleza magofu, lengo ni kuwashirikisha wananchi katika kushiriki katika miradi hii. Nakumbuka miradi mingi ambayo inaendeshwa ya magofu sasa hivi iko katika miradi ya *TASAF* ambayo lengo kubwa ni kuwashirikisha wananchi wenyewe kuona kwamba wanabuni miradi hii na kuweza kuiendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo liliopo katika miradi hii ni kwamba, Wizara ya Elimu ikishatengeneza ule mradi, lakini wale ambao wanahusika tena wanategemea moja kwa moja kila kitu kifanywe na Wizara ya Elimu. Nadhani tunachofanya sisi ni kuwajengea uwezo na kuwapa taaluma mbali mbali ya kuona kwamba wanaendeleza mradi ule. Tayari tumeshafanya kwa miradi ya Maruhubi pamoja na Mtoni, tumeshafundisha vijana kwa ajili ya kuendeleza miradi hii.

Kwa hivyo, nataka nimwambie mjumbe tu kwamba, ni kweli kuwa ukienda kwenye magofu haya waliokuwepo wengi hawawezi kutoa taarifa zile ambazo zinatakiwa na watalii. Lakini nadhani baada ya jitihada ambayo itafanywa na Wizara ya Elimu basi tatizo hili litapungua au litaondoka kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la viti na meza. Hili nadhani hata jana nilijibu swali kuhusu suala hili, na nikaeleza hatua mbali mbali ambazo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inachukua kuondoa tatizo hili.

Moja ambalo nililizungumza jana ni kwamba tayari hivi sasa tuna usambazaji wa viti na meza katika maskuli yetu na hatua mbali mbali tunazichukua kuona kwamba tatizo hili linaondoka kabisa.

Moja ya hatua ambayo niliielezea jana ni kwamba kila tunapojenga skuli sasa hivi ni kuona kwamba tunaweka hizo samani na kuondoa tatizo hili. Lakini pia jana nilieleza kwamba wizara sasa hivi ina utaratibu wa kutenga fedha za serikali kwa ajili ya kutengeneza viti hivi kwa maskuli yetu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nimjibu tu kwa sababu suala hili limeelezewa na watu wawili, Mhe. Mohamed Ali Salim (Mulla) nadhani jana aliniuliza swali kuhusu skuli ambazo hazina viti na meza ya mwalim. Nikamuahidi kwamba tushirikiane tuone kwamba tatizo hili tunalitatua.

Jana pia nilimueleza kwamba tayari tumechukua hatua ya kupeleka samani karibu 900 Pemba kwa ajili ya ugawaji katika maskuli hayo. Ninaamini kabisa viti hivi vitafika hata katika zile skuli ambazo hazina viti na meza ya mwalimu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu pendekezo la kwamba tutengeneze viti vya chuma nadhani hili tunalichukua. Kwa sababu tayari hatua kama hii imeshawahi kuchukuliwa huko nyuma basi tutaangalia kwa nini nyuma ilichukuliwa na baadae ikashindikana na sasa hivi tumerudi kwenye viti vya mbao.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nimueleze Mhe. Mwakilishi kwamba tutalichukua na kuweza kuona kwa nini nyuma tulifanya hivi na baadae tukageuza tukarejea kwenye viti vya mbao.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la upungufu wa walimu, nadhani pia nalo nimekuwa nikilielezea mara nyingi hapa Barazani wakati najibu maswali mbali mbali ambayo yameelezwa na wajumbe. Napenda niwaambie wajumbe kwamba tuna mradi mkubwa wa *World Bank* ambao tunatarajia kujenga skuli 20. Lakini katika mpango huo wa *World Bank* pia tunao mpango wa kufundisha walimu wakiwemo walimu wa somo la sayansi. Lakini vile vile tuna mpango wa kununua vifaa mbali mbali vya somo la sayansi.

Kwa hivyo, tatizo hili nadhani litaweza kupungua wakati tutakapoweza kutekeleza mradi huu wa World Bank ambayo pia leo nadhani nilijibu swali lake kuhusu hatua ambazo zimefikiwa katika mradi huu ambao sasa hivi tunaufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu maslahi ya walimu nalo hili pia tayari wizara imeshachukua hatua ya kuweza kuona kwamba walimu wanapata maslahi mazuri kadri inavyowezekana. Tayari tumeshayapitia upya maslahi hayo na *scheme of service* tayari imeshatengenezwa kwa ajili ya walimu hao na imeshapelekwa serikalini kwa ajili ya utekelezaji. Ninaamini kabisa tatizo hili la maslahi ya walimu litapungua mara tu wakati tutakapotekeleza *scheme* mpya ya utumishi.

Mhe. Mwenyekiti, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba katika *scheme of service* hii ya walimu hakutakuwa na tofauti kubwa baina ya walimu wa Bara na walimu wa hapa visiwani. Ninaamini kwamba lile tatizo la uhamaji wa walimu kutoka Zanzibar kwenda Bara litapungua kwa kiasi kikubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Mhe. Mohamed Ali Salim moja tayari nimeshalielezea na katika skuli hiyo ambayo ameitaja haina kiti cha mwalimu wala meza, basi katika hizi samani 900 ninahakikisha kwamba na skuli yako itapata.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Bodi ya Mikopo. Ameuliza Mhe. Mwakilishi kwamba kuna mawasiliano gani baina ya Bodi ya Mikopo ya Tanzania na ile ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nimjulishe tu kwamba katika Bodi ya Mikopo ya Tanzania na Bodi ya Mikopo ya Zanzibar ni vitu viwili tofauti. Lakini lengo ni moja kuwasaidia wanafunzi wetu kuweza kupata mikopo kwa ajili ya masomo ya juu. Mahusiano yaliyokuwepo ni kwamba kuna wajumbe ambao wanaingia katika Bodi ya Mikopo ya Tanzania ambao pia ni wajumbe wa Bodi ya Mikopo ya Zanzibar. Kwa hivyo, mawasiliano yaliyokuwepo kwamba tunaunganishwa na wajumbe ambao wanaoingia katika Bodi hiyo ya Mikopo ya Tanzania na hutupa taarifa kwamba nani na nani ambaye amepata mkopo huu.
Inawezekana na imeshatokezea kwamba kuna baadhi ya wanafunzi wanapata mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Tanzania lakini wakati huo huo walipata mkopo kutoka Bodi ya Zanzibar. Nadhani suala hili tayari tumeshalirekebisha na kuona kwamba halitokei tena. Kinachotakiwa ni kwamba mwanafunzi achukue mkopo katika bodi moja tu. Kama anaamua kuchukua Bodi ya Mikopo ya Tanzania basi achukue huko na kama anaamua kuchukua Bodi ya Mikopo ya Zanzibar basi achukue hapa.

Tunachokifanya ni kwamba wenzetu wa Tanzania mara nyengine wanakuwa hawawachukui vijana wetu wote hapa Zanzibar. Sisi kama Bodi ya Mikopo ya Zanzibar basi huwa tunaangalia nani na nani amekosa katika Bodi ya Mikopo ya Tanzania ili kuweza kumuingiza katika Bodi yetu ya Mikopo ya Zanzibar.

Kwa hivyo, namhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba hicho kinafanyika na tumejirekebisha, lile kosa ambalo lilifanyika tayari sasa hivi limesharekebishwa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Mhe. Hija Hassan Hija kuhusu skuli za sekondari za wilaya. Nadhani na hili leo nililizungumza wakati najibu swali. Tulisema kwamba tutajenga skuli 20 Zanzibar kila wilaya itapata skuli moja ya kisasa kabisa zikiwemo huduma muhimu za dakhalia. Nilieleza katika jibu langu nililojibu leo kwamba tayari tumeshafungua zabuni za washauri na baadae tunatarajia kupata wajenzi kwa ajili ya kuendelea na mradi huu.

Tatizo lililokuwepo ni kwamba kulikuwa na ukwamishaji kuhusu *World Bank* lakini tayari tumeshazungumza nao na tatizo limeshatatuka na tunaamini kwamba hatua zile ambazo zinapitiwa zitaweza kufikia mwisho na tunaweza kutekeleza mradi huu kabla ya mwaka 2009/2010 kama nilivyojibu kwenye swali.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ahadi ya kompyuta. Ni kweli kwamba kumekuwepo na ahadi mbali mbali za Mhe. Waziri kuhusu kuzipatia kompyuta skuli mbali mbali ambazo amepitia.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nimhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba ahadi hizi zitaweza kutekelezwa pale ambapo wizara itapata uwezo wa kuweza kulifanya hilo.

Nadhani Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wangu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni hayo ambayo yalijitokeza na napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba haya ambayo tunayazungumza hapa kwa kweli tunayafanyia kazi na tutaendelea kuyatekeleza kadri hali itakavyoruhusu. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru wewe binafsi, namshukuru Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa kazi nzuri ambayo ameifanya.

Mhe. Mwenyekitia: Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii fanya kazi yako na kazi ya Waziri wa Kazi, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu. Pia natoa pongezi zangu za dhati kwa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ikiwa wewe pia ni mjumbe wa kamati hiyo, wakiwemo Mwenyekiti Mhe. Ali Suleiman Ali, Makamo Mwenyekiti Mhe. Ame Ussi Juma, Mhe. Mohamed Ali Salim (Mulla), Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Haji Faki Shaali, Hii kamati kwa kweli ina vigogo hasa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tunafarijika na tunafaidika sana na kamati hii. Nyinyi mkiondoka sisi tunajipanga. Mmetuambia tutie lifti, lifti mpya Dk. Mohammed Saleh Jiddawi ameshatia sahihi itatiwa pale, mmetuambia tupeleke *ambulance* na mafuta, *ambulance* lipo la Pemba linapelekwa na mafuta yamekwenda Pemba mtapata hamna tatizo. Mmeniambia *x-ray* tayari zimeshafika hapa za Pemba zitapelekwa. Kila mnachotushauri sisi tunachukua hatua wala hatudharau. Kwa kweli maendeleo yetu ya wizara tunayojivunia basi sehemu kubwa inachangiwa na Kamati hii ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nakuja moja kwa moja kwa Mhe. Haji Mkema Haji kuhusu mambo ya saratani. Mhe. Mwenyekiti, kuna nyanja tatu katika mambo ya saratani na mambo mawili tunayatekeleza Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kuna mambo yanayohitaji *surgical treatment*, *chemotherapy* na *radiotherapy*.

Sasa katika mambo haya ya saratani *(cancer)* mambo ya kufanyia upasuaji, mambo ya matibabu ya madawa sisi tunayafanya pale wizarani, tuna madaktari bingwa wanayafanya mambo haya bila ya matatizo yoyote. Lakini mambo ya *radiotherapy* (mionzi) haya yanafanyika *Ocean Road Hospital* hatuna uwezo hapa. Kwa sababu haya mambo ya *radio active material* inabidi yawekwe pahala maalum na tahadhari kubwa sana zinachukuliwa. Sasa haya tunayafanya *Ocean Road.*

Sisi tuna mashirikiano mazuri sana na Kitengo cha *Ocean Road.* Tunapeleka vijana wetu watoto wa kike wanasomea kule ikisha wanakuja hapa *Mnazimmoja Hospital* wanafanyia uchunguzi mapema *cancer* ya kizazi. Wale wagonjwa wanaohitaji mionzi sisi hapa *Mnazimmoja Hospital* tunawa-*refer* na kuwapeleka Muhimbili.

Kwa ufupi kuna baadhi ya mambo tunayafanya hapa hapa kama ya saratani za matiti au saratani za kizazi ambazo zinahitajiwa kuondoshwa mapema pamoja na matibabu madogo madogo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ulaji wa chakula tunajitahidi sana hospitali ya Mnazimmoja na hospitali nyenginezo vyakula tunapeleka wagonjwa wetu wanalishwa mara tatu kwa mujibu wa uwezo tunaopata.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu madeni sasa hivi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hatuna madeni, madeni yaliyokuwepo ni madeni ya zamani. Hayo tumeyapeleka Wizara ya Fedha tunatumai wenyewe watachukua hatua za kuwalipa madeni hao wanaotudai. Lakini kwa sasa hivi kipindi hichi madeni wizara yetu hatuyakaribishi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salmin Awadh Salmin alizungumzia kuhusu nyumba za wazee kuzifanya kuwa mradi. Sisi tumeshapeleka maombi haya Wizara ya Fedha tunangojea majibu yao kama wamekubali kuufanya mradi na kutoa fedha, basi sisi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hatuna pingamizi.

Mhe. Mwenyekiti, Ali Denge Makame yeye ametuombea kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ipewe fedha nyingi kutoka Wizara ya Fedha tunalikaribisha hilo. Pia amezungumza kuhusu *ZAYEDEDA* na *AMD* ujenzi wa nyumba za wazazi Micheweni. Hivi juzi tulikuwa Micheweni na jiwe la msingi limewekwa

na Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania. Kazi ya ujenzi wa nyumba ya wazazi Micheweni imeshaanza na tunatarajiia karibu itamalizika na watu wa Micheweni watajifungulia katika jengo jipya la kisasa lenye vyombo vya kisasa. Tunawaambia tu uzazi wa mpangilio ufanyike lakini wanaozaa wasiwe na wasi wasi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mgonjwa Bi Riziki Selele apelekwe Mioti. Mhe. Mwenyekiti, mgonjwa Bi Riziki ameshapelekwa Mioti amesharudi amefanyiwa dawa yake vizuri na kule daktari amesema apelekwe mara ya pili, tarehe 5 mwezi huu anakwenda tena Mioti kufanyiwa dawa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohamed Ali Salim (Mulla) ametaka kujua je, *solar power* Makoongwe na anaingojea kwa hamu kubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, hospitali ya Wete, Chake Chake, Mkoani, Mwembeladu na *Mental Hospital* ndio tumepeleka *solar power*. Hivi vituo vya afya tunatafutia fedha na uwezo wa kupeleka *solar power*. Hususan sehemu za visiwa tutajitahidi tukifuzu kutafuta fedha hizo na huko kote kutapata *solar power*.

Lakini napenda si ahadi kwamba tutapeleka huko. Kwa sababu katika mradi wa *ADB solar power* kupeleka visiwani hakuna, hayo ni jukumu la Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kutafuta fedha na kupelekwa. Lakini lengo letu tutapeleka kwa sababu tunataka kufanikisha jambo hilo na tutafanikiwa.

Kusomesha wafanyakazi kwa nini tunazuia vyeti vyao hatuwapi. Utaratibu uliokuwepo Chuo cha Afya Mbweni mwanafunzi akimaliza basi baada ya miaka miwili ndio hupewa cheti chake. Huu utaratibu uliokuwepo toka zamani, sasa kama turekebishe utaratibu huo tutachukua ushauri na tutazungumza wizarani tuliangalie hili jambo. Lakini desturi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii anayemaliza Chuo cha Afya Mbweni basi muda wa miaka miwili anaambiwa kidogo hiki cheti chako tunakizuia baada ya miaka miwili wanapewa. Kama tubadilishe ushauri unatupa tumeuchukua tutaufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, walioanguka mikarafuu sisi tunafanya makisio tu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii lakini wanaolipa ni *ZSTC*, sisi tunafanya makisio tunasema makisio yake ni haya, kwa hivyo wahusika wanakusikia.

Kuhusu *Red Cross* wanafanya kazi kama wauguzi, sisi haturuhusu hilo. *Red Cross* wanafanya kazi kama orderly, mambo ya usafi, beba hichi, fanya hivi basi, lakini sio kazi ambayo hawakusomea. Wakifanya kazi za uuguzi ni lazima wasomee, kama watafanya hilo ni kosa, kwa hivyo kazi zao ni orderly tu pale, wafanye mambo ya usafi, kufyagia, kukosha basi.

Mhe. Hija Hassan Hija fedha za kipindupindu. Sisi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tunachokijua kwamba wafanyakazi wetu wote tumeshawalipa fedha za kipindupindu. Siku hizi hakuna madeni, siku hizi tunaita sabuni. Watu wanaoshiriki katika mradi wa kipindupindu tunaomba fedha tunapewa, tunafungua kambi na tunawalipa kama sabuni au chakula. Lakini hakuna malipo ya ziada ya kipindupindu.

Kuhusu Mkemia Mkuu athibitishwe na kupewa maslahi yake hili tunalishughulikia. Je, watoto wanaopelekwa Israel muda gani huchukua hata mwengine anafariki.

Mhe. Mwenyekiti, watoto wanaopelekwa Israel wanakuja madaktari wenyewe kutoka Israel hapa na vyombo vyao na zana zao. Wanafanya kazi kwa kushirikiana na wafanyakazi wetu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Wanawapima halafu wanawaweka kwa makundi, kundi hili liende tarehe hii, kundi hili likirudi linakwenda kundi hili. Kwa hivyo, wanawapanga wao wenyewe madaktari wanaotoka Israel kwa kushirikiana na madaktari wetu. Wanapanga kwa mujibu wa maradhi wanavyoyaona.

Sisi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hatuingii kwa chochote, tiketi wanatoa wao, chakula wanatoa wao, matibabu wanatoa wao na kila kitu, Serikali ya Israel inafanya wenyewe mambo haya. Kwa hivyo, sisi wizara tunachokifanya madaktari wetu wa hospitali ya Mnazimmoja wanashirikiana na madaktari kutoka Israel.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya haya sasa naomba niende kwenye Wizara ya Kazi, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto kama Kaimu Waziri. Mhe. Mwenyekiti, pia tunaipongeza kamati kwa michango yao mizuri sana, Mwenyekiti, Makamo Mwenyekiti na Wajumbe wote.

Suala kubwa hapa ni pesa za AK na JK, limezungumzwa na Mhe. Haji Mkema Haji, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Mohamed Ali Salim na waheshimiwa wote.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli mfuko haujawafikia wananchi wote sababu ziko nyingi sana zikiwemo kuchelewa kutolewa mkopo huo. Lakini sasa hivi wizara imejipanga vizuri kwa kushirikiana na Benki ya Watu wa Zanzibar, ili mikopo hiyo iweze kufika wilaya zote za Unguja na Pemba. Majimbo yote kama Magomeni na mengineyo tunatarajia yatafaidika na mfuko huu wa AK na JK.

Jumla ya wananchi 545 wamepatiwa mkopo kwa Unguja na Pemba. Bado tunaendelea na michakato na wengi ninahakika watafaidika na mfuko huo. Haya ndio majibu niliyopatiwa na maofisa wangu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri haya masuala ya Wizara ya Kazi, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto ni vizuri wale Waheshimiwa Wajumbe ambao wamesema majimbo yao watu wao hawajapata kabisa, basi mngekutana mkayafafanua mkayamaliza.

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kujibu maswali yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mhe. Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wake kwa kutengeneza taarifa hii ambayo imekidhi haja. Pia wajumbe hawa walipata fursa ya kutembelea katika maeneo ya wizara yangu na kwa asilimia kubwa sana waliridhika kwa sababu mimi mwenyewe nilishiriki katika majumuisho na wakatupongeza sana. Kwa yale machache ambayo waliyoyaona wametushauri na *inshaallah* tutayafanyia kazi katika bajeti hii inayokuja ili tuyamalize.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo kuna suala hapa la kwa nini kituo hichi cha elimu ya wanahabari hakisomeshi *Media Law* na *Constitution Law*. Mhe. Mwenyekiti, kituo kinasomesha *Media Law* katika *syllabus* yake katika ngazi ya cheti na ngazi ya diploma. Kituo hakisomeshi *Constitutional Law per say* lakini katika *syllabus* yake kuna somo la *Constitution* ambalo kila mshiriki anatakiwa alipasi. Kwa hivyo, kwenye suala la *Constitution* inasomeshwa, lakini kwenye *Constitution Law* ndio huko hakusomeshwi.

Lakini ushauri wa wajumbe kwamba kuna haja ya kusomesha huko, tutalichukua shauri hilo. Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe taarifa kwamba chuo chetu kina upungufu mkubwa sana wa walimu na wafanyakazi. Tumeomba nafasi tatu za wafanyakazi akiwemo *registrar* na tumeomba pia nafasi tatu za walimu. Tungezipata nafasi hizo za walimu na za *administration* chuo kwa kweli kingekuwa kimekamilika na tungekuwa tuna nafasi nzuri sana ya kwenda kuomba usajili wa kudumu.

Sasa bado tunakwenda mbio kuiomba Idara ya Utumishi Serikalini kutusaidia kutupatia kibali cha kuwaajiri hao, pesa zipo kwenye bajeti. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nitashukuru sana kama wewe mwenyewe binafsi na yeyote atakayekuwa na nafasi ya kutusaidia kuzungumza na utumishi utusaidie. Pesa tunazo kwenye bajeti zipo tunahitaji watu sita, watu watatu *administration* na watu watatu walimu. Sasa hivi tunatumia *part time teachers* na wengi wao ni hawa wafanyakazi, lakini kwa kweli hatuwezi kupata usajili wa kudumu kwa kutegemea nguvu hizo. Sasa tunataka usajili ili chuo chetu *certificate* na *diploma* tutakazozitoa ziwe zinakubalika.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la vyombo vya kufanyia kazi kama tunavyo au hatuna, kama hatuna basi tuna haja ya kuvitafuta. Mhe. Mwenyekiti, vyombo tunavyo kwa kiasi. Tumenunua hivi karibuni kompyuta tano za *digital*, ukiongezea na zile zilizokuwepo kwa hivyo tuna kompyuta nane. Hazijatosha bado lakini zinakidhi haja kwa kiwango kikubwa sana.

Tuna *photocopier* tumenunua hivi karibuni nayo ni ya *digital* aina ya *cannon.* Zile kompyuta hivi karibuni zitaunganishwa na *internet* ili twende katika huo mtandao wa kisasa. Hivi sasa *internet* imeunganishwa lakini kwa matumizi ya ofisi, baadae tutaiunganisha mpaka kwenye *library* ili wanachuo waweze kufanya *reference* zao kwa urahisi.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia *UNESCO* na mashirika mengine tuna vitabu si vingi vya kutosha lakini tuna vitabu vipya. Tunategemea kuendelea na kuwaomba wenzetu wengine wa kimataifa watupatie vitabu zaidi ili *library* yetu sasa iweze kujaa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salmin Awadh Salmin alizungumzia suala la kuliboresha gazeti letu, kuongeza maslahi ya wafanyakazi na ikiwezekana kujenga nyumba hasa ya Gazeti la Zanzibar Leo. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salmin ameyajua haya kwa sababu yeye ni Mjumbe wa Bodi ya Shirika la Magazeti ya Serikali. Tulimpeleka huko kwa kujua uwezo wake na taaluma yake ya kufuatilia mambo pale penye kasoro.

Tunakubali kwamba gazeti letu ni jipya linahitaji kuendelezwa na kwa kipindi cha bajeti hii inayomalizikia hatukuweza kuomba fedha ya kukidhi haja ya muundo huu wa shirika. Tumejitahidi serikali kwa kushirikiana na bodi tumekuwa tukizungumza mara kwa mara mbona hatuoni mabadiliko. Jibu linakuja pale pale kwamba pesa mlizotupa ni kidogo. Tukasema basi hamuwezi angalau wiki mara moja mkatoa gazeti la rangi, huu wito wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukaukamilisha.

Tunashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu wamelizungumza wame-*appreciate* kwamba tuna gazeti sasa angalau linatoka siku ya Ijumaa zuri la rangi. Tungeweza kulitoa kila siku tukatanua wigo wa kuyauza magazeti yetu tungefanya hivyo. Lakini *inshaallah* kwenye bajeti ijayo na wawakilishi watanisaidia kuitetea hiyo bajeti ili tupate pesa za kununua mitambo ya *colour separation*, kuanzisha magazeti ya rangi kila siku na ikiwezekana kujenga jengo letu. Lakini kwa hali iliyopo sasa kwa shirika letu halina matatizo ya makaazi ya jengo letu kwa sababu nafasi nzuri wanazo. Ni kweli kabisa tungepata jengo letu ingekuwa ni vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nilizungumze hili ili Mhe. Salmin Awadh Salmin alisikie na akatusaidie wakati wa kuzungumza katika bodi. Bodi ya Shirika la Magazeti ya Serikali mpaka sasa hivi haijawasilisha wizarani *strategic plan* ya gazeti, haijawasilisha *scheme of service* ya shirika lake na haijawasilisha *project proposal* iliyokamilika. Namuomba Mhe. Salmin kama ni mjumbe atusaidie kuhimiza katika haya ili tukiingia katika muhula mpya wa bajeti tuweze kutekeleza hayo ya kulidumisha gazeti letu kwa kufuata utaratibu huu wa kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Denge Makame alitushauri tutumie vizuri mitambo yetu ya *digital* tuliyokwishainunua ili matangazo yetu yafike mbali na kadhalika. Napenda kumueleza Profesa kwamba mitambo ya *digital* tuliyoinunua ni zaidi ya kusaidia hapa tulipo na zaidi kwenye *camera* na vifaa vidogo vidogo vya kurekodia. Hiyo ndio ilikuwa awamu ya mwanzo ya kukiondosha chombo chetu kutoka *analogue* kwenda katika *digital*, lakini hiyo labda ni asilimia 5 mpaka 7 ya kuelekea huko.

Mhe. Mwenyekiti, chini ya mradi wa NDRI wa kusamehe madeni, waliosamehewa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo na sisi tuna kasma yetu. Tumeomba dola milioni 2.5 kununua vifaa vingi sana vya kubadilisha mitambo yetu.

Kwa hivyo, Mhe. Ali Denge Makame, tukishavipata vifaa hivyo, pesa tunazo. Kwa hivyo tukivipata vifaa hivyo sasa suala lake litakuwa limekuja kwa wakati mzuri na jibu litapatikana. Tumeshaanza kusomesha watu wetu wengi tu na mitambo yetu ikishamalizika watukuwa na uwezo mkubwa sana wa kuiendesha.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohamed Ali Salim amezungumzia kuhusu kamusi na zaidi alizungumzia kwenye ushauri kwamba tutengeneze kamusi bora, zuri, lenye hadhi na litakaloweza kuwa kama ni *reference point* ya Waswahili wote watakaotaka kufanya *reference*.

Mhe. Mohamed Ali Salim anaelewa, kwa sababu yeye ni mjumbe wa kamati yetu ya Bodi ya Kiswahili na anaelewa tulipofika na tunavyokwenda. Juzi nililetewa maandishi yale ya mbele ili kuweka saini, ni kuthibitisha kwamba kazi imeshafika mbali sana.

Tunaomba radhi kwa nini tumechelewa. Kwa sababu kamusi tunalotaka tulitowe ni hili ambalo Mhe. Mohamed Ali Salim amelizungumza. Kwa sababu sisi ndio tunaozungumza Kiswahili fasaha, sisi ndio tunaoandika Kiswahili fasaha na kamusi hili litawasaidia watu wetu wa habari na wao kukitumia Kiswahili fasaha wakati wakitoa taarifa zao.

Kwa hivyo, katika taarifa hii kubwa kwenye sehemu ya 3.8 pale mwisho. Taarifa ilikuwa inaelezea au inatushauri kwamba tuondoshe matatizo yaliopo kati ya ZFA na serikali. Mhe. Mwenyekiti, nataka nithibitishe kwamba matatizo yale sasa ni hadithi au ni historia, kupitia mashirikiano makubwa yaliopo kati ya vyombo vyetu chombo cha habari na chombo cha michezo. Wizara mbili hizi zimekutana mara nyingi na zikikutana zinapitia masuala yote ya maendeleo na ya matatizo.

Katika kikao cha pili kabla ya kikao tulichokimaliza juzi, kwanza tulimaliza suala la matatizo ya ZFA na TFF, tukaizindua tena ile kamati ya pamoja ya kushauriana na Mhe. Hafidh Ali akapewa tena nafasi yake ya kuwa Mwenyekiti wa hiyo kamati. Nimepata habari hiyo kamati imeshakutana mara tatu na wamezungumzia zaidi suala hilo la mashirikiano na kufanya kazi kwa pamoja. Ni muda mrefu sasa hatujasikia kwenye magazeti kwamba kuna matatizo kati ya ZFA na TFF tunashukuru.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni nimesoma kwenye gazeti la Zanzibar Leo na magazeti ya mwananchi kwamba tatizo la CHANETA NA CHANEZA limeshamalizika, wameshakutana na wametayarisha *memorandum of understanding* na wametia na sahihi. Kwa hivyo, hiyo ndio faida ya waheshimiwa hata kama hawaongozi serikali au wizara za Muungano, lakini kama wizara zinafanana kikazi na kazi zake ni muhimu basi tunapokutana tunazungumza mazungumzo mazito, mazuri na tunapata ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu, na kufanya *summary* ndogo sana kwa wizara zetu nne ambazo Waheshimiwa Mawaziri wetu wametoa maelekezo au ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo na Naibu wake kwa kazi zao nzuri, pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wote wanaohusika katika wizara hizi yaani wafanyakazi wote kwa jumla.

Halikadhalika Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu kama yupo, pamoja na Wakurugenzi, madaktari na wafanyakazi wote kwa jumla. Vile vile Mhe. Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wake, Maafisa Wadhamini wote wa Pemba katika wizara zetu hizi.

Pia Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Naibu Waziri wake, Katibu, Manaibu Katibu, Wakurugenzi, Makamishna, Walimu na wafanyakazi wote wa wizara hizi. Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali ya muda wetu tuliokuwanao, basi sitosema mengi zaidi ya kuwashukuru kwa dhati kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niwapongeze kuanzia Waheshimiwa Mawaziri wenyewe, Manaibu wao, Makatibu, Wakurugenzi, wafanyakazi wote wa wizara hizi nne na Maafisa wetu Wadhamini tunawapa asilimia 100 wametushughulikia vizuri sana wakatu tulipokuwa Pemba, pamoja na wenzetu wa Tanzania Bara kwa kushirikiana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Mkurugenzi wa Vijana, Mkurugenzi wa Wizara ya Afya. Halikadhalika Maalim Jeketu kwa kazi nzuri ambazo tulishirikiana nao huko Tanzania Bara na mafanikio tuliyoyapata ndio matunda yake yapo hapa.

Kwa muhutasari Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kayaelezea. Mojawapo ni makubaliano ya CHANEZA na CHANETA. Lakini sio hayo tu, kuna faida kubwa lakini kwa

vile muda hatuna nitawapa wapenda kandanda katika nchi yetu. Ile *league* ya Muungano ambayo tulikuwa tunaililia kutafuta vipaji kwa timu zetu za Tanzania basi itarudiwa kwa muda mfupi ujao, baada ya makubaliano mazuri ya Mhe. Naibu Waziri Kiongozi wetu na Waziri wa Habari wa huko Tanzania Bara George Mkuchika.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo narudisha tena kikao hiki kuwashukuru wajumbe wote wa Baraza hili tukufu kwa kazi nzuri na mashirikiano mazuri waliotupa katika kuchangia kamati yetu. Kwa wale waliokuwa hawakupata bahati ya kuchangia basi pia wamechangia, maana wamekaa kimya na kusikiliza kwa sababu kila wizara inagusa taasisi mbali mbali katika majimbo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nakushukuru na ninawashukuruni sana wajumbe kwa kunisikiliza, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale ambao wanakubaliana na ripoti hiyo wanyanyuwe mikono juu. Wasiokubaliana. Waliokubali wameshinda. Ahsantes sana.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na afya njema na kunipa uwezo wa kuweza kusimama mbele ya Baraza lako hii tukufu, kuwasilisha ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2009/2010, kwa wizara zetu Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 104 (c) cha kanuni mpya za Baraza la Wawakilishi na majukumu yake yametajwa katika kfungu cha 109 kama ifuatavyo:-

Kwanza wajumbe wa kamati yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kamati hii imeundwa kutokana na wajumbe kumi, wakiwemo makatibu wawili. Wajumbe wenyewe ni:

1. Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu - Mwenyekiti
2. Mhe. Hamad Masoud Hamad - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Kamal Basha Pandu - Mjumbe
4. Mhe. Zakiya Omar Juma - Mjumbe
5. Mhe. Ame Ussi Juma - Mjumbe
6. Mhe. Subeti Khamis Faki - Mjumbe
7. Mhe. Asha Moh'd Hilal - Mjumbe
8. Mhe. Ali Denge Makame - Mjumbe
9. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe
10. Mhe. Omar Ali Jadi - Mjumbe
11. Nd. Othman Ali Othman - Katibu
12. Nd. Rabia Juma Shaaban - Katibu

MAJUKUMU YA KAMATI

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilikuwa na majukumu yafuatayo:

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya mwaka uliotangulia.
b) Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa Barazani.
c) Kufuatilia mapato na utekelezaji wa miradi ya Wananchi liyochini ya Wizara husika.
d) Kuchambua Mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya wizara husika ya mapato na matumizi ya kila Mwaka.

e) Kushughulikia jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.
f) Kufikiria miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika
g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji na ahadi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa maka 2009/2010 ilifuatilia utekelezaji sera na mipango kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa Bajeti, kwa Wizara za Mawasiliano na Uchukuzi na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilitumia wiki sita (Unguja wiki tatu, Pemba wiki mbili na Dar-es-salaam wiki moja) na siku nne kamati ilikwenda Tanga kwa ajili ya kuangalia maendeleo ya umeme unaotoka Tanga kwenda Pemba. Kwa ujumla Kamati iliridhika kwa kazi ilizozitembelea kwa Taasisi zinazohusika.

Mhe. Mwenyekiti napenda kuchukua nafasi hii adhimu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao ambayo yamewezesha kufanya kazi zetu katika hali ya ufanisi mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa malengo ya kazi za kamati, Kamati imepata nafasi ya kutembelea taasisi za Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, taasisi za Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Taasisi zilizo chini ya Serikali ya Muungano ambazo ni: Shirika la Posta, Kampuni ya simu (TTCL), Mamlaka ya Hali ya Hewa, Mamlaka ya Usafiri wa Anga, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Kampuni ya Simu ya Zantel- Dar-es-salaam na Kampuni ya ORYX iliyoko Dar-es-salaam.

WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI IDARA YA UJENZI NA UTUNZAJI WA BARABARA

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ilipotembelea na kukagua barabara za Mazizini hadi Fumba, Mshelishelini hadi Pwani Mchangani, Wete-Konde, Wete-Chake, Wete-Gando, Mtambile-Mwambe, Mtambile-Kangani, Mzingani-Wambaa, Kenya-Chambani, Tundauwa Pujini, na Barabara za Jozani, Ukongoroni, Charawe, ambazo barabara hizi zinajengwa kwa msaada wa wafadhili mbali mbali na wajenzi tofauti pamoja na mchango wa serikali unaotokana na mfuko wa barabara.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati iliridhishwa na kazi zilizofanywa na zinazoendelea kufanywa na UUB. Kamati yangu imeelezwa kuwa kuna mpango mkuu ambao unazihusisha baadhi ya barabara hizi ambao unalenga hadi mwaka 2025, na kutokana na kazi hizo Idara inahitaji wataalam ili kushirikiana na waliopo kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Kamati inaelezwa kwamba kwa hivi sasa lami imeshafika nchini na baadhi ya barabara zitatengenezwa kama barabara ya Kinazini – Bububu.
Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipotembelea barabara za Jozani, Ukongoroni, Michamvi iliridhishwa na kazi zinazoendelea za kuzisafisha barabara hizo, kuweka kifusi ili kuweza kupitika vizuri zaidi, na baadae itatiwa lami kutokana na kuridhika kwa Mfuko wa Barabara kutokana na kazi zinazofanywa ambazo ni kilomita 17.3, kwa awamu ya kwanza kazi iligharimu Shs. Milioni 75 na awamu ya pili itagharimu shillingi milioni 70.

IDARA YA ANGA

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Anga jukumu lake ni kushughulikia na kusimamia maendeleo ya usafiri wa Anga Zanzibar, pamoja na uendeshaji wa viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba. Kamati ilipata nafasi ya kutembelea katika viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba, na kuona hali halisi ya viwanja hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipotembelea kiwanja cha ndege cha Pemba ilisisitiza hoja ya kiwanja hicho kuwa na taa ili ndege ziwe na uwezo wa kutua katika mazingira yote, na kushauri suala la uzio liendelee kutafutiwa ufumbuzi kutokana na hatari ya wanyama kupita katika njia ya kurukia na kutulia ndege na kupatikana jenereta la akiba. Kamati imeridhishwa na hatua ya matengenezo ya jengo la abiria. Kiwanja cha ndege cha Pemba kimetengewa shilingi milioni 12,000,000, na ADB kwa ajili ya jenereta la akiba.

Mhe. Mwenyekiti, Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Zanzibar hivi sasa kimo katika matengenezo makubwa ya njia ya kutulia na kurukia ndege. Kamati ilifanikiwa kwenda kuona kazi hizo zinavyoendelea

na kuridhika na matengenezo ya kazi hizo. Mategemeo ya kamati ni kumalizika kwa muda wa kazi hiyo kama mkataba unavyoelekeza. Kamati ilioneshwa ramani ya jengo la kufikia abiria ambalo litajengwa na Kampuni ya BEIJING CONSTRUCTION ENGINEERING CO.LTD kutoka China. Kamati imeridhishwa matayarisho ya kazi hiyo ambayo ni muhimu na itaondosha malalamiko ya abiria wakati wanapotaka kusafiri.

IDARA YA USAFIRI NA LESENI

Mhe. Mwenyekiti, Jukumu la Idara ya Usafiri na Leseni ni kusimamia usalama wa watumiaji wote wa barabara, jukumu hilo linahusisha kazi za ukaguzi wa vyombo vya moto, usimamizi wa mafunzo ya udereva, upasishaji wa madereva na walimu wa skuli za udereva na kudhibiti utoaji huduma za usafirishaji abiria na mizigo kwa njia ya barabara na kuyafanyia matengenezo magari ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipotembelea Idara ya Usafiri na Leseni imeridhishwa na utaratibu wa kazi zinavyoendeshwa katika Idara hii, na kushauri Idara hii kupewa fedha kutokana na mahitaji yao ili kukamilisha malengo waliojiwekea kutokana na umuhimu wa Idara yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilitembelea karakana kuu na kuangalia utendaji wa kazi wa sehemu hii, na kushauri magari yote ya serikali kupelekwa kwa ajili ya matengenezo ili kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi, na wafanyakazi wa hapo wapewe mafunzo yanayostahiki ili waweze kufanya kazi kwa ari zaidi na kuongezwa vifaa vya kazi katika karakana hiyo.

MASHIRIKA YALIYOCHINI YA WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI

a) SHIRIKA LA BANDARI

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bandari kwa mwaka 2009/2010 limepewa Jukumu la kutoa huduma za uingizaji na utoaji meli katika Bandari za Unguja na Pemba, uangalizi wa alama za kuongozea meli (minara na maboya) uteremshaji na upakiaji wa bidhaa kwenye meli, kuhifadhi mizigo inayoingia bandarini pamoja na kufanya matengenezo madogo madogo ya vyombo vya baharini kwa kutumia chelezo kilichopo Karakana kuu ya Malindi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilitembelea Shirika la Bandari la Unguja na Pemba na kuangalia kazi mbali mbali zinazofanywa na Shirika hilo. Kwa ujumla kamati imeridhishwa na kazi za Shirika hilo kwa kupata maelezo ya utendaji kazi wa zana nzito ambao umerahisisha kazi ya gati ya Malindi kwa upande wa utiaji wa sakafu, na kamati kutembelea Kisiwa cha Chumbe kwa ajili ya kuangalia mnara huo ambao teknolojia ya gesi itabadilishwa na kutumika ya "s*olar*" katika minara yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Pemba kamati ilitembelea Bandari za Mkoani, Wete na Wesha na kuridhika hatua za uendeshaji wa bandari hizo, na kuelezwa kwamba suala la gati ya Mkoani kudidimia litapatiwa ufumbuzi kwa kufanywa matengenezo yatakayoondoa hali hiyo, na kuhitaji vifaa ili kuwa na sifa zinazohitajika kuwa ya kimataifa. Kamati imeridhishwa na mabanda ya kufikia abiria kwa Bandari za Mkoani na Wete ambazo zimewapunguzia usumbufu wananchi waliokuwa wanaupata.

SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Meli lina jukumu la kuendesha meli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na kutoa huduma za uwakala wa meli za kigeni zinazoingia katika Bandari za Zanzibar. Shirika la Meli linaendesha Meli tatu za MT Ukombozi, MV Maendeleo, na MV Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ilipotembelea Shirika hili ilipata maelezo ya kazi yanayohusiana na utendaji kazi wa Shirika hili, hususan meli zetu pamoja na changamoto inayozikabili. Kamati imeshauri meli ya MV Mapinduzi iuzwe na kuweza kununuliwa meli nyengine mpya.

Mhe. Mwenyekiti, Meli ya MV Maendeleo mpaka hivi sasa iko chelezoni, na baadhi ya wajumbe wa kamati walikwenda kuiona na kuandika ripoti kuhusu meli hiyo. Matumaini ya kamati kwamba meli hiyo ikisharudi na baada ya matengenezo makubwa itapunguza tatizo la usafiri wa Pemba ambalo limejitokeza hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipata nafasi ya kuonana na wamiliki wa vyombo wote na kuzungumza nao pamoja na kutoa pole kwa wamiliki wa MV Serengeti kutokana na ajali iliyotokea. Kamati imewashauri wenye vyombo kuhakikisha usalama wa abiria kutokana na matatizo yanayojitokeza wakati wa kusafiri na kufuata taratibu za vitambulisho kwa abiria.

TAASISI ZILIZO CHINI YA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO

(a) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ni kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mamlaka ya mawasiliano Tanzania Na. 12 ya 2003 na sheria za sekta yaani Sheria ya Utangazaji Na. 6 ya 1993 na Sheria ya Mawasiliano Na. 18 ya 1993, Kutoa leseni na pia kufuta inapobidi kwa kuzingatia ubora wa utoaji huduma za Mawasiliano, Posta na Utangazaji, Kusimamia bei ya huduma za utangazaji na mawasiliano pale ambapo hakuna ushindani, Kushughulikia malalamiko na kusuluhisha migogoro ndani ya sekta, Kushirikiana na wadhibiti wa mawasiliano katika nchi nyengine ili kuandaa mikakati itakayosaidia kuboresha utoaji huduma nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ilitembelea Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania iliyoko Zanzibar na Dar-es-salaam, na kuridhishwa na maendeleo ya taasisi hii hususan majengo ambayo ni mapya na yana mazingira mazuri ya utendaji wa kazi. Kamati imeshauri kuongezwa wajumbe katika Bodi pamoja na kutengwa kwa nafasi za masomo kwa Wazanzibari na kujengwa jengo la mamlaka huko Pemba.

(b) Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka imejiwekea malengo kuyatekeleza ifikapo juni 2010, kwa kutoa huduma bora na za uhakika za hali ya hewa, kuajiri wafanyakazi wa kutosha, kutoa mafunzo na kuhakikisha matumizi ya nyenzo mbali mbali yanafanyika kama ilivyopangwa, kupatikana kwa vifaa na mitambo ya kisasa ya hali ya hewa, huduma bora za utafiti zinafanyika na matokea yake kupelekwa vituoni ili kuongeza tija.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea mamlaka hii yenye ofisi yake iliyoko Zanzibar na Dar-es-salaam, na kupata maelezo yanayohusiana na mamlaka hii ikiwa pamoja na kutoa taarifa za utabiri wa hali ya hewa, na kuwapelekea walengwa ili nao wazisambaza habari hizi kwa lengo la kuepusha maafa kwa wahusika. Kamati imeridhishwa na utendaji wa kazi wa mamlaka hii, kuanzia katika bodi yake, pamoja na utendaji wake wa kazi na kushauri suala la kukaimu wadhifa litadutiwe ufumbuzi kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(c) Shirika la Posta Tanzania (TPC)

Mhe. Mwenyekiti, Majukumu ya Shirika la Posta ni kutoa huduma za posta ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kusambaza huduma za msingi za posta nchini kote, kukidhi mahitaji muhimu ya mawasiliano ya jamii, kutoa huduma mbalimbali za uwakala na huduma zingine zinazohitajika na jamii kupitia mtandao wa posta nchini ambazo zitaimarisha biashara za Shirika la Posta Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipotembelea Shirika la Posta lenye makao makuu yake huko Dar-es-salaam na kuridhishwa na kazi zake. Kamati inashauri kuendelelea kubuni mbinu mpya ili kuweza kujiendeleza, na kuendelea kutoa huduma zake mpaka vijijini kwani huko ndiko kwenye wananchi wengi. Kamati ilishauri kutolewa elimu kwa wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi ili waweze kuwaelimisha wananchi wanaowaongeza.

(d) Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)

Mhe. Mwenyekiti, Kampuni ya Simu Tanzania ina jukumu la kutoa huduma za msingi za simu nchini (*Basic Telephone services*), kutunza na kupanua mtandao wa huduma za mawasiliano ya simu nchini pamoja na kutoa huduma ambazo si za msingi (*non-basic*).

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipotembelea kampuni ya simu Tanzania, imeelezwa matatizo yaliyojitokeza wakati wa ubinafsishaji wa kampuni hii, na tatizo lililojitokeza la kupungua kutoa huduma hiyo kumilikiwa na wageni. Kamati imeelezwa kwamba kwa sasa uongozi wa kampuni hii ni watanzania wenyewe na wanachukua kila jitihada kuhakikisha kampuni inarudi katika utendaji wa kuridhisha. Kamati imeshauri itoe promosheni kwa wateja ili waongezeke, na kuelezwa kwamba wataalamu wa kampuni hiyo watapelekwa China kwenda kujifunza.

(e) Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA)

Mhe. Mwenyekiti, Malengo ya Mamlaka ya Usafi wa Anga Tanzania ni kusafirisha kwa ndege (*air transport*) kwa abiria, kwenye viwanja vya ndege zinajumuisha matumizi ya miundombinu ya urukaji na utuwaji, huduma kwa abiria, mizigo, mafuta ya ndege na chakula cha kwenye ndege na urukaji ikiwa ni pamoja na uongozaji ndege, mawasiliano kwa ajili ya urukaji, mitambo yaani *navigation surveillance*.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ilipotembelea Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania ilioko uwanja wa ndege wa kimataifa wa Dar es Salaam na kuona jengo jipya la mamlaka hiyo. Kamati imeridhika na utendaji wa kazi na uwajibikaji wa mamlaka hiyo. Kamati imeelezwa kwamba ili mamlaka iweze kufanya kazi yake kikamilifu ni muhimu kwa serikali zote mbili zisaidie, ili kuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yake iliyopewa.

KAMPUNI YA SIMU YA ZANTEL

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ilipotembelea Kampuni ya Simu ya Zantel iliyoko Dar-es-salaam na kuelezwa kwamba wameajiri wafanyakazi 686 wa muda ambao ni Wazanzibar. Kamati imeelezwa kampuni inatumia teknolojia ya GSM na CDMA na kama kuna aina mbali mbali za motisha kwa wateja kama, kuongea shilingi moja kwa sekunde na nyenginezo.
Kamati imeelezwa kwamba kwa hivi sasa wana wateja 1,400,000/- lengo lao ifikapo mwaka 2011 kuwa na wateja wasiopungua 2,000,000. Mwaka 2015 wamekusudia kuwa wa kwanza au wa pili kwa kutoa huduma bora nchini.

WIZARA YA MAJI, UJENZI NISHATI NA ARDHI NA MAMLAKA YA MAJI

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji imejipangia kutekeleza miradi ya maji kwa mwaka 2009/2010 ya usambazaji wa maji vijijini, uhuishaji na upanuzi wa shughuli za maji mijini, kuijengea uwezo mamlaka ya maji, usambazaji wa maji safi na mazingira na kazi za kawaida na kazi za kawaida za matengenezo ya mabomba na pampu za maji.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ilitembelea mamlaka ya maji iliridhishwa na kazi zinazofanywa na Mamlaka hiyo kwa upande wa Unguja na Pemba na kuipongeza mamlaka katika uendeshaji wa kazi zake, na hasa kwa kupunguza bei ya maji kutoka Shs. 4000 hadi Shs. 2000.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilitembelea Miradi ya Maji ya Mfenesini Bumbini, Kangagani, Njuguni, Kigongoni, Ziwani, Jumbi, Kizimkazi, Mkoa wa Mjini Magharibi unaofadhiliwa na Japan na sehemu zenye matatizo ya kupatikana maji za Michenzani na Makadara. Mategemeo ya kamati ni kwamba kazi hizi zitamalizika kwa wakati uliopangwa, ili wananchi waepukane na matatizo ya kutafuta maji.

IDARA YA NISHATI NA MADINI - ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2009/2010 Idara ya Nishati na Madini imepanga kukamilisha kazi zote zilizobakia katika kuandaa sera hiyo, kuendeleza jitihada za kutafuta nishati mbadala na kuwafikishia elimu

ya Umeme wa Jua wananchi wa maeneo ya mashamba na Visiwa vya Unguja na Pemba. Vile vile kushiriki kikamilifu katika masuala yote ya Nishati ya Jumuia ya Afrika Mashariki, kuendelea kusimamia upatikanaji wa. mafuta ya *Diesel*, *Petrol*, *Kerosene* nakadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeipongeza Idara kupitia Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa kupitishwa Sera ya Nishati, ambayo itakayosaidia nchi yetu kuwa na uwezo wa kuunda Shirika la Mafuta la Zanzibar, baada ya kupitishwa mswada katika Baraza lako Tukufu, na Zanzibar kufaidika na nishati hii ya mafuta baada ya kupatikana *(Makofi)*.

Kamati ilitembelea kampuni zote za mafuta zilizoko hapa Zanzibar wakati wa kipindi cha kukosekana kwa Umeme na kuridhika na jitihada zilizochukuliwa na kampuni hizo, kuhakikisha kwamba nishati hii ya mafuta inapatikana. Kampuni zenyewe ni hizi zifuatazo:-

1. *Zanzibar Petroeum*,
2. *United Petroleum* na
3. *GAPCO*.

Vile vile kamati ilitembelea uwanja wa ndege kuangalia Kampuni ya *British Petroleum* na kuridhika na kazi zake pamoja na kwenda Mwangapwani kuangalia sehemu ambayo inajengwa, kwa ajili ya kuweka na kupatikana kwa mafuta, meli kutoka nje zitakuwa zinaleta mafuta Zanzibar na mafuta hayo yatauzwa kimataifa *(Makofi)*.

IDARA YA UJENZI

Idara ya Ujenzi kwa Mwaka 2009/2010 imejipangia kutekeleza na kusimamia na kudhibiti ipasavyo shughuli zote zinazohusu sekta ya ujenzi kwa kuimarisha Bodi ya Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo pamoja na Bodi ya Makandarasi sambamba na kuunda kanuni zitazoratibu na kudhibiti ujenzi nchini. Vile vile kuanza harakati za kushughulikia zaidi kazi za ushauri na usimamizi wa ujenzi kuliko kushughulikia na fani nyenginezo za ujenzi, ikiwemo ukandarasi na kumaliza kabisa na baadaye kukabidhi Serikalini Jengo la Nyumba za Maendeleo Mpapa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilipotembelea Idara ya Ujenzi na kupata maelezo yanayohusiana na maendeleo ya Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo za Michenzani, ambazo kimsingi zimeshamalizika na zinasubiri utaratibu wa kuzigawa kwa mwenyewe. Kwa hivyo, wenye haki ya kupata nyumba hizo hususan kwa wale waliovunjiwa nyumba zao kupisha ujenzi wa Nyumba za maendeleo na wale wenye matatizo ya nyumba za kukaa.

Kamati ilipata maelezo yanayohusu Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo Mpapa na kueleza tatizo ni umalizaji wa nyumba hasa upatikanaji wa fedha, ambazo zinaingizwa kidogo na muda umekuwa mkubwa kiasi ambacho vifaa vya ujenzi kila siku vinapanda bei. Kamati imeshauri serikali iingizie idara fedha kwa wakati muafaka, ili iweze kumaliza jengo hilo la Mpapa na kuomba kamati kushughulikia suala la Idara ya Ujenzi kupewa majengo ya serikali, kwa ajili ya kuimarisha Idara ya Ujenzi.

IDARA YA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAAZI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Idara ya Nyumba inakusudia kutekeleza mambo ya kulipa fidia wale wote waliovunjiwa nyumba zao kupisha ujenzi wa nyumba za maendeleo, Kuzifanyia matengenezo Nyumba za Serikali Unguja na Pemba, Kuzidisha juhudi za ukusanyaji mapato na kodi za nyumba.

Pia Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba itaendelea kupokea, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri yatayowasilishwa, kuendelea kuandaa Sheria ya '*Condominium'* na kufanyia marekebisho Sheria ya Kudhibiti Kodi za Nyumba, kuandaa utaratibu mzuri wa baadhi ya Nyumba za Serikali na kusimamia zoezi hilo kwa mujibu wa miongozo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilipotembelea Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi na kuelezwa utaratibu uliowekwa kwa Nyumba za Maendeleo za Michenzani, kuwalipa fidia wale ambao waliovunjiwa nyumba

zao, kwa ajili ya kupisha ujenzi wa nyumba za maendeleo na utaratibu wa uuzaji wa Nyumba za Vijiji kuuziwa wale ambao wanaishi kwa wakati huu.

Kamati inaiunga mkono Bodi iliyoundwa ya Kudhibiti Kodi, ili iweze kufanya kazi vizuri na kuweka kiwango cha malipo ya kodi kwa nyumba hizo. Ili idara iwe na uwezo wa kuzifanyia matengenezo ya nyumba hizo na kuyashughulikia makaro, ambayo katika nyumba nyengine yako katika hali mbaya, pamoja na matengenezo ya nyumba hizo.

MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI MJI MKONGWE

Katika mwaka 2009/2010 mamlaka ilikusudia kuendeleza shughuli za Mradi wa Kuukuza na Kuutambulisha Mji Mkongwe unaohifadhiwa na Shirika la *SIDA*, hasa kipengele cha kufanya mapitio ya uwezo wa mamlaka, kutekeleza Maazimio ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*), yanayoagizwa kwa tathmini ya athari za kimazingira na kijamii (*environmental and social impact assessment*) katika eneo la Malindi baada ya ujenzi wa bandari mpya.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilitembelea Mamlaka ya Uendelezaji na Utunzaji Mji Mkongwe na kupata maelezo yanayohusiana na mamlaka hiyo, pia kupata nafasi ya kutembelea Bustani ya Forodhani, na kuona maendeleo ya bustani hiyo na hali ya kuridhisha ya utunzwaji wa bustani hiyo. Vile vile kamati imeshauri kuwa juhudi ziendelee za ujenzi wa ukuta wa ukingo wa maji unaoendelea hadi katika Taasisi ya Elimu ya Bahari iliyoko karibu na Bandari ya Malindi.

Suala la Kuhifadhi na Kuendeleza Mji Mkongwe linasisitizwa sana na kamati na kushauri mamlaka kusaidiwa katika hali zote, ili lengo lililokusudiwa liweze kupatikana. Hii inatokana na baadhi ya wenye nyumba kujenga kinyume na utaratibu unavyotakiwa. Vile vile kamati inapongeza kupitishwa Sheria ya Kufuta Sheria ya 1994, ili watakaopinga utaratibu wa ujenzi unaotakiwa wachukuliwe hatua.

IDARA YA UTAWALA WA ARDHI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Utawala wa Ardhi katika mwaka 2009/2010 ilikusudia kutekeleza malengo ya kuendelea Kusimamia Mapitio ya Sera ya Ardhi, pamoja na Mapitio ya Sheria ya Ardhi, kuendelea kulinda mustakabali wa eka zisizotumika kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa.

Kutokana na hali hiyo, na kuona lengo hili linafanikiwa idara itaendelea na uhakiki wa matumizi ya eka tatu, kuendelea kusimamia maeneo ya uwekezaji, ili kuhakikisha kwamba mapato yanakusanywa ipasavyo na hakuna migogoro ya ardhi inayojitokeza. Vile vile kusimamia mikataba ya ukodishaji kwa kuhakikisha kwamba, wawekezaji wanaendeleza shughuli zao kwa mujibu wa makubaliano ya mikataba hiyo na taratibu walizopewa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi imeelezwa kwamba utaratibu wa zoezi la kuzihakiki eka tatu linaendelea vizuri. Kamati ilishauri maeneo yaliyokwisha fanyiwa uhakiki yadhibitiwe na kuendelea na kazi hiyo katika eneo jengine, ili lengo la kupewa eka wananchi libakie pale pale kwa nia ya kujiendeleza. Kamati imeishauri idara kusimamia maeneo ya uwekezaji kwa kushirikiana na taasisi nyengine katika kuondoa matatizo yanayojitokeza katika maeneo hayo.

Suala la Mapitio ya Sheria ya Ardhi ni muhimu kutokana na migogoro ya ardhi inavyojitokeza hususan katika maeneo ya kitalii. Kamati inashauri idara kuendelea kutafuta njia bora za kusuluhihsa wananchi katika maeneo yanayohusika na matatizo, ili kuweza kupatikana muafaka.

IDARA YA ARDHI NA USAJILI

Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Idara ya Usajili na Ardhi ina malengo ya kuendelea kubadilisha hati za zamani na kuwapatia wananchi hati mpya. Pia kuendelea na utaratibu wa kuweka kumbukumbu za ardhi kwa njia ya kisasa, kuendelea na mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya Zanzibar, kuimarisha udhibiti wa umiliki wa matumizi endelevu ya ardhi na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaovamia ardhi.

Hivyo, Mahakama ya Ardhi itaendelea kuimarisha ufanisi zaidi kwa kutekeleza kazi zake pamoja na Afisi ya Mrajis na Bodi ya Uhaulishaji Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilitembela na kupata maelezo kuhusu idara hii. Kamati imeridhishwa na kazi za idara zinazofanya pamoja na usajili wa ardhi. Vile vile kamati ilishauri kutafutwa wataalamu wa fani ya ardhi, kutokana na upungufu mkubwa wa wataalamu waliopo na wanafunzi waliochukuliwa kusomeshwa, kwa ajili ya kuajiriwa katika idara hii, malipo yao yameshindikana na kuamua baada ya kumaliza masomo yao wende kwenye taasisi nyengine.

Suala la Ardhi ni la umuhimu kwa nchi yoyote. Hivyo, kamati inapongeza idara kupitia wizara kwa kuundwa Mahakama ya Ardhi, ambayo itasaidia kupunguza matatizo ya ardhi yaliyopo kwa muda mrefu, kwa kuongezewa mahakimu kila mkoa kwa lengo la kuwarahisishia wananchi wanaofuwatilia huduma na kesi zao kuhukumiwa mapema iwezekanavyo *(Makofi)*.

IDARA YA UPIMAJI NA MIPANGO MIJI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Upimaji na Mipango Miji kwa mwaka 2009/2010, ilikusudia kuendelea na kazi ya ukamilishaji wa Ramani za Visiwa vya Unguja na Pemba, kuendelea kupima viwanja 2,000 vya makaazi Unguja na Pemba, kadri tatizo la upatikanaji wa maeneo na ulipaji wa fidia ya ardhi litalopatiwa ufumbuzi.

Vile vile kuendelea kuufanyia Mpango wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Ardhi Nchini na utayarishaji wa ramani za matumizi ya ardhi, katika vijiji vya ukanda wa pwani kwa kushirikiana na Mradi wa *MACEMP*. Pia kuendelea na kazi ya upimaji wa mipaka ya mikoa na wilaya nchini, kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ pamoja na Mradi wa *MACEMP* na kuendelea na kazi ya udhibiti ujenzi kwa kushirikiana na taasisi nyengine za serikali.

Kamati ilipotembelea Idara ya Upimaji na Mipango Miji, ili kupata maelezo kuhusu kazi za idara hii. Hata hivyo, kamati ilipata fursa ya kwenda kuangalia eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya mwekezaji mzalendo huko Mwangapwani kwa lengo la kujengwa Chelezo, ambacho kitakuwa na uwezo sawa na kile cha Mombasa Kenya baada ya kumalizika. Kamati imeridhisha na hatua hii iliyofikiwa *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imesisitiza utoaji wa viwanja uzingatie miundombinu, na maeneo ya viwanja wapewe wawekezaji, ili wajenge nyumba za ghorofa na kuuziwa wananchi, kwa ajili kuweza kuikinga ardhi itumike sehemu ndogo na nyengine iweze kuwanufaisha wakulima. Aidha kamati imetaka kuchukuliwa hatua wananchi waliojenga bila kibali na waliojenga katika vianzio vya maji, ili kulinda mazingira.

SHIRIKA LA UMEME

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010 shirika limepanga kutekeleza Miradi wa Nyongeze ya Awamu ya Nne na usambazaji wa umeme vijijini, kupeleka umeme Pemba kutoka Tanga, Mradi wa kuendeleza ufungaji wa mita za TUKUZA "*prepaid*". Pia Mradi wa Uimarishaji wa Shirika Kifedha (*Financial Turn Arround*). Mradi wa Ujenzi wa njia ya pili kutoka Ubungo hadi Mtoni, Unguja.

Kamati ilitembelea Shirika la Umeme Zanzibar na kupata maelezo ya miradi, ambayo shirika imejiwekea malengo. Pia kamati ilipata fursa ya kutembelea Mtoni kwa ajili ya kuangalia usambazaji wa umeme unaotoka Fumba.

Vile vile kamati ilitembelea Kituo cha Fumba na kupata maelezo ya kina kuhusu matatizo yaliyojitokeza mpaka ukakosekana Umeme katika kisiwa cha Unguja kuanzia tarehe 10 Disemba 2009 hadi ulipopatikana. Tatizo hilo lilichukua takribani miezi mitatu na matengenezo yaliyofanywa na wataalamu kutoka Uingereza, pia na matengenezo kama hayo yalifanyika katika kituo cha Ras Kiromoni, ambayo kamati ilikwenda kuyangalia na kushauri kufanyiwa masawazisho ya mara kwa mara.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilikwenda Tanga kuangalia kazi za utekelezaji wa Ujenzi wa Laini Kubwa ya "33KV O/H *line*" kutoka Majani Mapana hadi Mnyanjani na kuelekea Pemba ambayo laini ina urefu wa

kilomita 9. Ulazaji wa umeme ulifanyika tarehe 10/12/2009 kwa ujumla kazi imekwenda vizuri. Tatizo lililojitokeza ambalo kamati ililikuta ni kwamba zinatakiwa kuhamishwa nguzo, pia kamati ilikutana na wahusika na kutaka suala hili lirekebishwe ili kazi iendelee kama ilivyopangwa.

KAMPUNI YA MAFUTA *ORYX*

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilipokuwa Dar-es-Salaam ilipata nafasi ya kutembelea Kampuni ya Mafuta ya *ORYX* na kupata maelezo ya kina. Kwa kweli kampuni hii ni ya kimataifa na ina uwezo wa kusafirisha mafuta nchi nzima na nchi za jirani, kampuni ina mashirikiano makubwa na Tanzania na mwaka 2006 serikali ilondoa kodi kwa upande wa gesi.

Kamati imeelezwa kwamba *ORYX* ina mpango wa kuanzisha mikopo kwa wafanyakazi ili waweze kutumia gesi ipasavyo, ambayo haina madhara na wala haiharibu mazingira na gharama zitapunguzwa, ili mtu yoyote aweze kununua.

Nifaraja kuona kwamba kampuni hii imekubali kuwafanyia semina Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeridhika na utendaji kazi wa kampuni hii, kwani ni kampuni pekee ambayo serikali inanunua mafuta mazito ya *IDO* kupeleka Pemba, kwa ajili ya jenereta za kuendesha umeme na kuridhika na huduma zao.

MAJUMUISHO YA KAMATI

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi imeridhika na kazi za taasisi ilizozitembelea kwa lengo la kuangalia utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2009/2010. Taasisi hizo ni Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi.

Vile vile kamati ilizitembelea taasisi zilizo chini ya Serikali ya Muungano nazo ni Mamlaka ya Hali ya Hewa, Mamlaka ya Usafiri wa Anga, Mamlaka ya Mawasiliano, Kampuni ya Simu (*TTCL*), Shirika la Posta, Kampuni ya Simu ya *Zantel* na Kampuni ya Mafuta ya *ORYX*.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imezitaka taasisi zilizo katika Taasisi za Umma, kuendelea kufanya kazi kwa kubuni mbinu mpya na kushindana kwa biashara, ili wafikie malengo walivyojiwekea. Vile vile kutumia utaalamu katika kazi zao, ili kufanya kwa uhakika kuomba wafadhili na kujitokeza ndani na nje ya nchi.

MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti, yafuatayo ni mapendekezo yetu kwa serikali:-

1. Kamati imependekeza kufanywa Idara ya Anga na Shirika la Bandari kuwa Mamlaka, hii kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi na tija kwa wafanyakazi;

2. Kamati imependekeza magari yote ya serikali yenye namba ya SMZ kupelekwa Karakana Kuu, kwa ajili ya matengenezo ili kupuka matumizi mabaya ya fedha. Suala hili mara nyingi tunalisemea, lakini hakuna hatua yoyote inayochukuliwa na serikali. Kwa hivyo, tunamuomba Mdhibiti Mkuu na yeyote mwenye kushughulikia mali za umma, basi suala hili lipewe kipaumbele na hii ni amri itekelezwe *(Makofi)*;

3. Kamati imependekeza suala la kupatiwa elimu wafanyakazi lipewe umuhimu, ili kuweza kufanya kazi vizuri kwa mujibu wa fani zao;
4. Kamati imependekeza kwa Mfuko wa Barabara kugharamia matengenezo ya vipuri vya zana zinazotumika katika matengenezo ya barabara;

5. Kamati inashauri suala la Usafiri wa Baharini lipewe kipaumbele kwa kununuliwa Meli Mpya za Serikali zitakazohudumia abiria kwa kuepuka usumbufu uliopoo hivi sasa ambao umekithiri;

6. Kamati imependekeza kwa serikali kuangalia sehemu muhimu zaidi kwa kuajiri wafanyakazi kwa lengo la kuongeza wataalamu;

7. Kamati imependekeza kufanyiwa matengenezo ya masawazisho ya mara kwa mara kwa waya wa umeme unaotoka Fumba kwenda Ras-Kiromoni *(Makofi)*;

8. Kamati inapendekeza kwamba yawekwe maeneo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za ghorofa kwa lengo la kupunguza matumizi mabaya ya ardhi;

9. Kamati inapendekeza kuendelea kuchukua jitihada za makusudi za kulinda Mji Mkongwe, ili ubaki katika haiba yake pamoja na kuwa Urithi wa wa Kimataifa na

10. Kamati imependekeza kushirikiana na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zenye kufanyakazi zinazofanana na zile za Serikali ya Muungano, ili kubadilishana ujuzi na uzoefu *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza hili la Wawakilishi pamoja na mimi mwenyewe binafsi nakushukuruni sana na naomba kuwasilisha *(Makofi)*.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuchangia Ripoti ya Kamati ya Mawasilinao na Ujenzi ambayo inazijumuisha wizara mbili nazo ni Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi pamoja na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwa ajili ya kuendeleza kazi mbali mbali za kamati hii.

Nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Uchukuzi, Makamo Mwenyekiti, Wajumbe wote wa Kamati, Waheshimiwa Mawaziri wa wizara hizi, Manaibu Waziri wao, Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote wa wizara hizi kwa pamoja nawapongeza sana *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze Kamati yetu hii ya Mawasiliano na Ujenzi hasa nikizingatia kwamba chimbuko la mafanikio ni mimi niliyesimama hapa ambaye naitwa Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) ambaye ndiye nilikuwa Mwenyekiti niliyepita kabla huyu ambaye yupo, malezi yangu mema yaliyobakia yanaendelezwa *(Kicheko/Makofi)*.

Kwa kweli kila mtu hujivunia kile alichokipanda. Kwa mfano, ukipanda muhogo vizuri basi utavuna mazao mazuri na kuona mafanikio yake. Kwa hivyo, hii nasema ni changamoto iliyotokana na kamati yangu uliyopita na kilichobakia ni urithi ambao unaendelezwa na Mwenyekiti wa kamati hii ambaye alikuwa ni mjumbe wakati huo, nawapongeza sana *(Makofi)*.

Kutokana na hali ya nchi kiasi miezi mitatu huko nyuma iliyopita nchi yetu ilikuwa katika giza. Lakini nachukua fursa hii adhimu kuipongeza Serikali yetu ya Zanzibar kwa juhudi kubwa ilizochukua za kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma muhimu.

Kwanza nilipongeze Shirika la Umeme kwa juhudi kubwa iliyokuwa ikifanya na kutoa taarifa mbali mbali za maendeleo tena kwa ukweli na uwazi, yaani bila ya kuficha. Kwa mfano, hali iko hivi na vile mpaka tumefanikiwa. Kwa hivyo, nawapongeza sana kuanzia Meneja wa Shirika pamoja na watendaji wake wote.

Kwa sababu wakati unapofanyakazi na ukiwa muwazi, yaani huna kificho basi kazi yako itakuwa laini na wala haina manung,uniko, haidhuru kwamba lengo lako ufikie pahala fulani na kushindikana, lakini bado Meneja hakuwa na hofu ya kusema na kusema bila ya kuogopa. Kwa hiyo, nampongeza Mzalendo kijana wetu huyu pamoja na watendaji wake wote kwa kutoa taarifa hizo sahihi ambazo wananchi wetu walizipokea siku hadi siku.

Vile vile katika hili niunganishe kuishukuru serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ambapo kwa asilimia mia moja umefanyakazi nzuri sana ya kuunganisha taarifa inayotolewa katika Shirika la Umeme kuhusiana na harakati zetu za kila siku zilizokuwa zikiendelea.

Kwa kweli ninawapongeza sana kwa juhudi yao hiyo, ninamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie Meneja wetu huyu kwa uwezo wake pamoja na ujasiri wake, basi Mwenyezi Mungu *Inshaallah* amlipe mema na aendelee kufanyakazi zake kwa ufanisi zaidi pamoja na watendaji wake wote.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya tatizo hili ambalo lilitokea hali ya mazingira ilibadilika katika nchi yetu na watu walikuwa wanakwenda mbio kila pembe kwa ajili ya kutafuta maji. Lakini naishukuru serikali kupitia Mamlaka ya Maji, kwa kweli walifanyakazi kubwa sana ya kujitolea.

Suala hili linaonesha kwamba mwananchi anapoambiwa alipie basi huwa kina faida yake baadaye. Kwa mfano, ukiambiwa skuli mwanafunzi achangie shilingi 3,000/- kwa mwaka basi wazee wachangie, kwa sababu faida yake yale masomo anayoendelea nayo baadaye atayaona.

Kwa hivyo, mamlaka ilijibana na wala haina kitu, yaani hakuna malipo yoyote kwa mwezi, lakini kile walichokuwa nacho pamoja na kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali waliongezea, ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaondokana na shida ya kupata maji safi na salama. Kwa mfano, leo wanachukua *generator* kutoka sehemu moja kwenda nyengine na kesho pahala pengine, magari ya maji kupelekwa katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza Mamlaka ya Maji Zanzibar, Wizara ya Maji, Ujenzi Nishati na pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kazi kubwa iliyofanywa ya kuhakikisha kwamba tatizo limetokea katika nchi, yaani sawa na vita. Kwa kweli nchi inapoingia vitani na Mwenyezi Mungu atuepushie na wala tusiingie vitani, isipokuwa tuwe katika hali ya amani na utulivu maisha yetu yote, inakuwa hakuna mkubwa wa mdogo.

Kwa mfano, tutizame Vita vya Kagera wakati vilipotokea, mimi niliyesimama hapa nilikuwa mwanajeshi Mhe. Mwenyekiti tena nikiringa, pia Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu, Mhe. Kamal Basha Pandu, Mhe. Salmin Awadh Salmin, yaani wengi tuliopo hapa tulikuwa wanajeshi, lakini tulikuwa *standby*, yaani vita vinapiganwa huko na sisi tuko tayari wakati wote na ilikuwa unapewa ilani moja tu unapewa ruhusa ukalale kwako, maana mwanajeshi unatakiwa umuondoe mawazo umuweke katika raha.

Kwa hivyo, vita vipo Kagera lakini kama vipo hapa Zanzibar, unaambiwa unapotoka nyumbani kwako asubuhi unaaga kabisa maana tumekula kiapo, kwamba popote katika nchi hii au nje ya mipaka ya nchi hii nitapigana bila ya kuogopa. Kwa maana hiyo, ulikuwa ukifika kwenye kikosi chako siku hiyo ukikuta kwenye orodha, maana inakuja orodha kutoka juu, yaani fulani na fulani jiandaeni basi hurudi tena nyumbani, kile kimekuwa ni kiapo ambacho kinakubalika.

Mhe. Mwenyekiti, hivi vita vilivyotokea vya kukosa umeme ni sawa na vita vya nchi. Serikali kwa nguvu zake zote ilisema pamoja na athari iliyotokea basi wananchi wetu wapate kidogo angalau hiki na kile kwa ajili ya kuondoa yale matatizo yaliyojitokeza. Kwa hivyo, naipongeza Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa kazi yao nzuri waliyoifanya.

Kwa kweli tatizo letu kubwa Waswahili tunayo tabia ya kutokusema ukweli. Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili ni baya sana ambalo linaturejesha nyuma baada ya kwenda mbele. Kwa mfano, fulani amefanya vizuri basi msifu amefanya vizuri na fulani amefanya kosa basi mwambia amefanya kosa na arudie kwa njia fulani kwa ajili ya kufuta makosa yake, lakini hatuna tabia hiyo.

Kwa hivyo, mimi kwa kuwa msafi katika nafsi yangu, basi nawasifu sana wenzetu hawa kwa kazi kubwa walizozifanya Shirika la Umeme pamoja na Mamlaka ya Maji kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuhakikisha kwamba fedha zinatolewa huduma ya maji inapatikana pamoja na mambo mengine. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza serikali kupitia Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka nilizungumze hapa ni kuhusu Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, nayo naipongeza sana kwa hatua ambazo zinaonekana hivi sasa. Kwa kweli tukitaka tusitake ikiwa unazo radhi za wazee na mwenyewe mkweli, basi yale mafanikio niliyoyasema hapa ndiyo yaliyokuja *(Makofi)*.

Nilishuhudia katika mkataba wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege, pia nilishiriki katika utiaji saini kuhusu Ujenzi wa Bandari au Gati yetu Mpya ya Malindi. Vile vile nilishuhudia katika utiaji wa saini wa ujenzi wa barabara mbali mbali pamoja na Mhe. Machano Othman Said wakati huo alikuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, mwenyewe Mhe. *Brigadier* Adam Mwakanjuki alikuwepo ambaye ndiye Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, pamoja na kazi nyengine nyingi ambazo nimezishuhudia, basi matunda yake leo yale pale yanaliwa.

Kwa hivyo, barabara zetu hivi sasa zimo kwenye harakati nzuri za kuwaendeleza wananchi wetu na kuondoa adha, yaani mazao kutoka kijijini kwa usumbufu, basi sasa wamekuwa wakitembea bila ya matatizo yoyote. Kutokana na hali hiyo tunaipongeza serikali kupitia UUB.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni vyema nikakuomba wewe mwenyewe pamoja na Wajumbe wote waliopo hapa tukiacha kampuni za *MECCO, S.S. MEHTA* na nyenginezo. Lakini ile Idara yetu ya UUB inafanyakazi nzuri sana, inajenga barabara kwa uwezo wa kileo tena inayo kila uwezo wa kushindana na makampuni ya nje. Isipokuwa kutokana na sheria za kilimwengu hatuwezi kuingia kwenye *tender* kwa sababu tumo serikalini na tukipewa tunaweza tena kuliko hao wengine.

Lakini sitaki kuzitoa makosa baadhi ya barabara. Kwa mfano, kuna barabara ambazo zimejengwa na UUB na baadhi ya barabara ambazo zimejengwa na makampuni mengine ambayo sitakikujataja, kwa kweli naweza kusema kwamba yetu ni nzuri mara mia moja zaidi tena yenye ubora wa kiwango kuliko za wenzetu hao waliotoka nje na kuja kutujengea barabara hapa. Kwa hivyo, nawapongeza Mkurugenzi pamoja na watendaji wake, wanafanyakazi nzuri na wanajitahidi kwa hali na mali, ili kuhakikisha kwamba mafanikio yanapatikana *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, tukiacha barabara ya Uwanja wa Ndege ya Mazizini. Lakini nataka ukipata nafasi basi utembelee barabara hii ya Mtoni kuna sehemu wanaifanyia ukarabati mzuri sana. Mwenzangu Mhe. Hasnuu Moh'd Haji aliniambia sijaona, yaani ile raha yake kwa kile kipande ambacho kimeanza kuwekwa lami, barabara ya Bububu kuanzia Mtoni kuja Kinazini tukikiangalie kile kipange kichotengenezwa utadhani wametengeneza *MECCO*, kwa sababu hii ni kampuni nzuri.

MECCO Mhe. Mwenyekti na lazima utembee kwa sababu wewe ni Mwenyekiti wa Baraza, wakati mwengine linapoulizwa swali basi tayari umeshapita. Kwa mfano, mimi napenda sana kufuatilia mambo ya maendeleo *(Kicheko/Makofi)*.

Kwa hiyo, nakuhakikishia kwamba njia ya Amani – Dunga hivi sasa jinsi Kampuni ya *MECCO* ilivyoila, maana kama hujenda siku nyingi basi mlima wa Koani huujui na utauliza uko wapi, yaani mlima umeliwa wote. Lakini barabara ile wanatoa kifusi cha zamani chote na kuweka kifusi kipya kabisa *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, naweza kusema njia aliyosema Mhe. Waziri wa (AR) Mawasiliano na Uchukuzi, kwamba kuna njia zinazoishi miaka 5, au 7 ama 10. Lakini hii naweza kusema Mwenyezi Mungu akitufikisha hata miaka 30 panapouhai, basi inaweza kufika, kwa sababu ni njia imara tena ya uhakika. Kwa hivyo, huo ndio utawala bora tena ndio njia zetu za kuhakikisha kwamba tunatafuta viwango ambavyo vinakubalika kimataifa, nawapongeza sana wenzetu *(Makofi)*.

Vile vile kuna tatizo jengine ambalo nalo tuliseme kuhusiana na Shirika la Bandari Zanzibar. Kwa kweli shirika hili nalo limepiga hatua kubwa sana, hivi sasa tunavyokwenda mbio katika bandari zetu mbali mbali tukianzia Bandari ya Malindi, Mkoani, Wesha, Wete basi unakuta mabadiliko ya kimandari, tena ni bandari za kisasa, kwa sababu huduma zote zipo pale.

Kwa mfano, ukitaka kupumzika *VIP*, ukihitaji chai kwenye *restaurant*, yaani ukitaka chochote basi unapata na hata ukisema leo unalala hapo, basi utalala bila ya hofu. Kutokana na hali hiyo, wanapongeza Shirika la Bandari kwa kazi nzuri wanayoifanya *(Makofi)*.

Lakini kwa kuokoa muda nazipongeza kampuni zetu za simu. Kampuni hizi zinafanyakazi nzuri za kuunganisha jamii, kusaidia wanyonge, kwa sababu kuna *offer* fulani inapoingia basi wananchi wetu wanafaidika. Kwa mfano, hivi sasa kuna *offer* inayosema 'Chomoka na Vespa' pamoja na mengineo.

Jambo la mwisho, kwa kuwa muda hamna nasikitika. Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali kwa dhati kabisa kupitia Wizara ya Mawasiliano pamoja na serikali kuu, kwamba nchi yetu ni visiwa tunahitaji kuwa na meli za serikali. Kwa mfano, tunazo sherehe zetu Bara au Pemba ama tunazo karafuu zetu, yaani tunayo mambo mengi. Nadhani hii ni aibu kuwa tunashindwa kupata angalau meli moja ya kileo au mbili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe kwa kuwa unaiomba serikali ipate meli na mimi ni Mjumbe wa Bodi ya Shirika la Meli, basi dakika tano nitakupa jioni *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti *(Makofi)*.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona sasa hivi kupata nafasi ya kumalizia dakika tano zilizobakia.

Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo yote niliyoyaeleza nililigusa Shirika la Meli Zanzibar. Nimesema katika dunia yetu visiwa vya Zanzibar vimezungukwa na bahari na hakuna njia yoyote ya mkato utakapokwenda Pemba njia inayotumiwa na asilimia 90 ya wasafiri wetu hutumia meli au boti nyengine na wengine wenye uwezo wao wa kuamini bahari hutumia ngalawa au madau. Lakini usafiri wa salama ni meli ili upate uhakika wa safari yako.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ikiwa wewe ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Meli pia ni mmoja kuhakikisha kwamba haya mambo ninayoyazungumza yanatekelezeka basi namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa kuangalia jografia ya nchi yetu na kwa kuangalia umuhimu wa wananchi wetu wa Unguja wetu wa Unguja na Pemba wanategemea wapate usafiri wa uhakika wa meli. Kama serikali itapata meli kubwa iliyokuwa nzuri tusitafute meli ya kwenda mbio tu tupate hata meli ya kwenda kidogo kwa sababu usafiri wa kutoka Unguja kwenda Pemba unatumia watu na mizigo. Kwa hivyo, ipatikane meli nzuri ambayo itaondoa usumbufu kwa wananchi wetu kuondoa utata huu uliokuwepo wa usafiri ambao hauna uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, huko nyuma tunakotoka wakati wa MV. Mapinduzi na MV. Maendeleo zinafanyakazi asilimia kubwa ya wananchi walikuwa na imani kutoka siku fulani mpaka siku fulani nitakwenda safari yangu bila ya matatizo. Lakini leo mheshimiwa usafiri wetu umekuwa wa kubahatisha kwa sababu nataka kusema kuwa wa kubahatisha wenye vyombo binafsi wana maamuzi yao. Kwa hivyo, naiomba serikali kwa kuliona hili na kulipa umuhimu naiomba Wizara ya Fedha na Uchumi ifanye taratibu zake zozote zinazowezekana ili Shirika la Meli lipate meli za kuwahudumia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengi huwa yanafanyika ya sherehe mbali mbali mara Pemba mara Unguja huwa watu wa Pemba wanataka kuja Unguja na Waunguja waende Pemba. Mhe. Mwenyekiti, wakiwa na vyombo vya uhakika basi kila kitu kitakuwa kizuri zaidi bila ya matatizo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hili naliomba kwa moyo mkunjufu na naamini Mhe. Waziri kwa kuwa wafadhili wengi wanakuja hili atalitafutia njia la kulitumbukiza pahala popote hata ikiwa kwa mkopo lakini zipatikane meli kama mbili ambazo zitasaidia wananchi wetu wa Unguja na Pemba kuondokana na utata wa usafiri ambao hauna uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka nilizungumzie ni kuwapongeza wenzetu wa tasisi inayoshughulikia na ukaguzi wa meli. Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba kwa kipindi hiki tulichokuwa nacho wenzetu hawa wamo katika harakati nzuri za kufanya kazi na kuhakikisha wanakwenda kutokana na kiwango ambacho kinatakiwa katika meli zetu ili twende salama. Pia ningeshauri kama kuna chombo hakina uhakika wa usalama ni bora kizuiliwe kwani bora kinga kuliko tiba kwa sababu

tutakapokizuia chombo ambacho hakina uhakika ni bora kuliko kuja kung'ojea ushahidi wa kuja kuharibikiwa mbele.

Mhe. Mwenyekiti, naamini wananchi wetu watiifu na wananchi wetu wanapenda vyombo vyao lakini wakati mwengine anakuwa hana budi imemtokea dharura ya kusafiri na chombo kilichopo hakina uhakika basi chombo kama hicho kinaweza kikahatarisha usalama wa wananchi wetu. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri hili aliangalie na aweze kuwaangalia wananchi katika maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba hivi sasa makampuni ya mafuta Zanzibar yanaongezeka, si vibaya Shirika la Meli likapatiwa meli ya kisasa ambayo itakidhi haja hasa tukiangalia kuwa mara kwa mara hutokea matatizo ya ukosefu wa meli kufika hapa kwa wakati na wananchi wetu wakakosa huduma hiyo muhimu na bila ya huduma hiyo harakati za maisha huwa zinapungua. Mhe. Mwenyekiti, naamini mafuta ni nyenzo muhimu sana na nyenzo hii ikikosekana siku moja basi harakati za vyombo watu huwa wanahangaika hapa na pale na ulanguzi wa mafuta huwa unajitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile umenipa dakika tano naheshimu sana muda ulionipa lakini nakushukuru kwa dhati kuona kuwa hili shirika nililoligusa linawahudumia Wazanzibari wote tukitaka tusitake. Hili ni moja katika kuwapunguzia umasikini wananchi wetu. Kwa hivyo, ombi langu la mwisho kabisa naiomba tena serikali kuliangalia hili kwa faida ya wananchi wetu. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii nikapata kutoa michango yangu juu ya ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mambo makubwa nina mambo kama mawili matatu tu.

Mhe. Mwenyekiti, eneo moja ambalo ningeomba kulizungumzia ni suala la miradi ya barabara. Tumeona miradi kadhaa ambayo imekusudiwa kutekelezwa na malengo mbali mbali, lakini jambo ambalo nataka kulizungumzia ni suala la ujenzi wa barabara ya Magomeni-Sogea. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, suala la umaliziaji wa barabara ya Magomeni-Sogea linanisononesha sana na kwa sababu wizara au serikali imefanya jambo zuri la kutengeneza ile barabara kwani kila mmoja akiona anaona ni nzuri na inapendeza. Lakini sasa uzuri wake umeshaanza kupotea. Kwa nini Mhe. Mwenyekiti, nikasema hivyo?

Mhe. Mwenyekiti, barabara sasa hivi inahatarisha maisha ya watu na inahatarisha maisha ya watu kwa jambo mimi naweza nikalisema ni dogo kabisa na ambalo tayari tumeshakubaliana kwamba barabara ile ikamilishwe. Wananchi wamekuwa wakilalamika kwenye mawio juu ya athari ya barabara ile na hatari zinawapata. Juzi hata kwenye maelezo baada ya habari yamezungumzwa, wamethubutu hata kusema bora barabara yetu ya mwanzo kuliko hii ya sasa hivi. Hivi ndio vilio vya wananchi wa Jimbo la Magomeni juu ya barabara ile. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, sijui tena aseme nani, kwa sababu mimi nimeshasema sana,wananchi wana lalamika lakini hakuna utekelezaji wa jambo lolote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kusema kwamba serikali hii ni ya wananchi na sisi sote ni watumishi wa watu na ni wajibu wetu tusikilize wananchi wanataka nini na wanasema nini. Tunapokuwa hatuwasikilizi maana yake hatuwatendei haki, na hili sio jambo zuri na kwa sababu uwezo wa kutengeneza jambo lile upo na kama mnakumbuka Mhe. Waziri katika bajeti iliyopita alitoa ahadi hapa kwamba atavitengeneza vikuta vile katika kota ya mwanzo ya bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, kesho kutwa tunaingia bajeti nyengine hakuna chochote kilichofanyika. Sijui tuseme ni kitu gani kinachoendelea na wakati tunashuhudia mambo mengi yanaendelea kufanyika. Mhe. Mwenyekiti, mimi nashindwa kuelewa dhamira ya jambo hili kwa sababu niliwahi kwenda mimi kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano kuzungumza nae kuhusu jambo hili akaniambia kwamba tunakusudia kuitengeneza baada ya kumalizika vikuta vya barabara ya Kiembesamaki, lakini hadi hii leo hakuna lolote linaloendelea. Hili ni jambo la kusikitisha sana na ni jambo ambalo linatia aibu kwamba kila wakati tunazungumza jambo hilo hilo na utekelezaji wake haupo. Mwisho Katibu Mk

Kwa hivyo, inakuwaje hali inakuwa kama hivi, tuseme kwa lugha gani ili wenzetu watuelewe, barabara ya Magomeni ina matatizo inasababisha vifo, inasababisha hatari, leo mwaka mzima suala la kuweka vikuta

linashindikana. Kwa hivyo, nimeamua niseme tena na Mhe. Waziri ananisikia na watendaji wake wananisikia, lakini nasema natoa tahadhari bajeti ijao nakusudia kuondosha shilingi katika kifungu cha Idara ya Barabara, na sitorudisha shilingi. Mhe. Mwenyekiti, najua bajeti itapitishwa lakini itapitishwa kwa kura, lakini nitakuwa nimeshaonesha ule uchungu wangu juu ya jambo lile na wananchi watasikia. Nakusudia kuondosha shilingi ya kifungu cha Idara ya Barabara katika bajeti ijao na sitorudisha. Hilo moja.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kuhusu suala la la barabara ya Benjamin William Mkapa ambayo tulipata taarifa kwamba tayari fedha zake zipo, Rais Jakaya Mrisho Kikwete ameshawasilisha serikalini lakini inaonekana bado utekelezaji wa jambo hilo haujaanza. Sasa tungetaka kufahamu tu suala hili likoje kwa sababu wakati mwengine tunakuwa na matatizo ya fedha, lakini hata fedha zinapokuwepo pia inakuwa tatizo. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka tupate maelezo juu ya maendeleo ya ujenzi ule, na kwa sababu tuna wasi wasi kwamba fedha kila zinapokaa zinapungua thamani yake na barabara nayo haiko katika hali nzuri, iko katika hali ya hatari, fedha zipo lakini utekelezaji nao unakuwa mgumu. Kwa hivyo, tunataka kujua tatizo nini wakati fedha zipo.

Mhe. Mwenyekiti, niondoke kwenye Idara ya Barabara nije katika Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi. Mhe. Mwenyekiti, wakati wa ujenzi wa Afisi ya Makao Makuu ya Shirika la Posta na Simu Kijangwani wakati ule kuna baadhi ya wananchi pale walivunjiwa nyumba zao. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuvunjiwa nyumba kuna baadhi ya wananchi wa pale walipewa pesa kufidiwa zile nyumba zao, lakini kuna baadhi ya wananchi walipewa nyumba nyengine katika nyumba za maendeleo za Michenzani. Wale waliopewa nyumba za Michenzani hadi leo hawana uthibitisho wowote unaothibitisha kwamba zile nyumba ni mali yao na ni nyumba mbadala badala ya zile zilizovunjwa pale. Waliovunjiwa pale wamejaribu kufuatilia katika taasisi mbali mbali lakini hakuna kumbukumbu yoyote inayothibitisha hivyo inaonekana ni watu tu wamepewa nyumba kaeni hapa maana yake hawana uthibitisho wa kumiliki nyumba zile.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi ningetaka kujua nini tatizo na kama kwa wakati ule hakukuwa na utaratibu wa kutoa hatimiliki juu ya nyumba zile basi serikali iwe na utaratibu wa kuwapa hatimiliki, kwa sababu nyumba zile hawakupewa kama ruzuku au sadaka kama wengine. Wao walipewa nyumba zile baada ya kuvunjiwa nyumba zao kwa sababu mle katika nyumba za Maendeleo kuna watu wamepewa tu. Lakini hawa waliovunjiwa maana yake wamepewa nyumba kwa sababu wamevunjiwa nyumba. Kwa hivyo, serikali lazima iwape hatimiliki za nyumba zile ili kuthibitisha kwamba nyumba zile ni mali yao tofauti na wengine. Mhe. Mwenyekiti, hilo linaonekana halikufanyika kwa hiyo Mhe. Waziri anayehusika na masuala ya majengo hebu atupe ufafanuzi na atupe maelezo juu ya nyumba zile.

Mhe. Mwenyekiti, ni suala la Mamlaka ya Maji. Mamlaka ya Maji sasa hivi inasimamia mradi wa maji wa Mkoa wa Mjini Magharibi lakini kwa bahati mbaya sana maendeleo ya mradi ule kwa kweli hayajaturidhisha pamoja na kwamba awamu ya mwanzo tayari na sasa hivi wako katika awamu ya pili, lakini bado maendeleo hayajaridhisha. Katika maeneo ya Sogea yaliyoko katika Jimbo la Magomeni kuna tatizo la maji kwa asilimia mia moja, hakuna hata tone la maji linalopatikana kwa muda wote, kabla ya umeme kuzimwa na hata baada ya umeme kuwashwa. Wananchi wa maeneo yale wamekuwa wakihangaika kutafuta maji kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana kwamba bado katika karne hii katika Mkoa wa Mjini Magharibi watu wanahangaika na vidoo vya maji kwenda huku na huku kwa kweli sio jambo la kufurahisha ni jambo la kusikitisha sana.

Kwa hivyo, naiomba Idara ya Maji kwa makusudi ishughulikie matatizo ya maji katika eneo la Sogea ambalo liko katika Wilaya ya Mjini Jimbo la Magomeni kuna matatizo makubwa, wananchi wanapata tabu sana ya maji, huku wananchi wengine wa visiwa hivi hivi wakifaidika na maji usiku na mchana, lakini wananchi wa Sogea walioko katika visiwa hivi hivi wanasumbuka na maji usiku na mchana badala ya kuhangaikia mambo mengine wao wanahangaikia maji. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri hili alielewe kwamba wananchi wa Sogea hawana maji kwa asilimia mia moja tofauti na maeneo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa kweli mchango wangu ni huo nimejaribu kuchukua yale maeneo ambayo kwa kweli yanakuwa yananikera, niwaambie Mawaziri kwamba haya ni mambo ambayo yanakera na yanasononesha wananchi ili wachukue hatua ya kuyatatua. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi kutia barka ripoti ya wenzetu ya Kamati ya Ujenzi na Mawasiliano nawapongeza kwa kazi nzuri kwa sababu kamati hii imepewa wizara mbili tu lakini ni wizara kubwa sana yenye maeneo makubwa sana, pia wameweza kutuletea ripoti nzuri na sisi tumebakia kutia minofu mle ambamo wenzetu wamefanya mapungufu. Mapungufu yaliomo sio kama wameshindwa kwa sababu ya muda hawakupata nafasi kutembelea maeneo yote ambayo yalistahiki wayapitie na wayaandikie ripoti. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tutatumia muda huu sisi tuliowahi kupita kwenye maeneo mengine ambayo wenzetu wa kamati walifanya kazi kwa niaba yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi niushukuru uongozi wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi hasa kwa lile tukio la hivi karibuni la kukatika kwa umeme katika kisiwa chetu cha Unguja jinsi walivyolikabili tatizo lile kwa kushirikiana na sisi wananchi na hivi sasa tunapata umeme kama kawaida. Najua kazi ilikuwa nzito, kubwa na iliyopoteza muda, sisi tumeshiriki kwa upande mwengine kutulia, lakini mafundi wenzetu usiku na mchana walifanya kazi hii, vyombo vya fedha vilihangaika huku na kule kutafuta fedha kununua vipuri na kuwapatia maposho na wataalamu walikuwa wakishughulikia kurekebisha mitambo yetu ili umeme urejee. Kwa hivyo, lazima tuwashukuru na Mhe. Waziri awape pongezi mafundi wetu kwa jitihada zao kubwa walizozifanya, wametumia na uzalendo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kweli sasa hivi umeme umerudi vizuri tu na hivi sasa visiwa vyetu vinangara hasa ukiwa kwenye ndege usiku unaweza kuuliza hapa ni Hawai au ni wapi. Kwa kweli visiwa vyetu vinapendeza kutokana na umeme kuenea sehemu zetu, lakini juu ya kazi hiyo nzuri napenda kuiambia serikali kwamba kuna baadhi ya maeneo umeme huu hawajapata mpaka leo kwa hivyo wajitahidi. Mhe. Mwenyekiti, kijiji cha Jumbi bado mpaka leo hawajapata umeme, sehemu za Mkorogo, Pongwe, Mizingani bado umeme hawajapata katika eneo la Koani kijiji cha Manyame hawajapata umeme. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri katika hili ijitahidi kwa sababu hii ni ahadi ambaye anamaliza muda wake alisema atahakikisha sehemu zote zinapata umeme, wananchi washindwe wenyewe kuvuta katika nguzo kutia katika nyumba. Nafikiri hivi sasa wapige hatua zaidi ili kukamilisha kumnawisha uso kiongozi wetu ambaye anamaliza muda wake kwa kipindi hiki.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Nyumba nayo imefanya kazi vizuri, niwapongeze mafundi na hasa kuchukua hatua ya kiporo cha awamu ya mwanzo majengo ambayo yalikuwa yamekwama kwa muda mwingi hayakufikiriwa. Mhe. Mwenyekiti, nyumba zile hivi sasa zimekaa kama manuwari ya Kijerumani ambazo zilikuwa zikifanya kazi wakati huo wa vita, majumba yamependeza na makubwa. Katika Mkoa wetu tulikuwa na magofu kama yale sehemu ye Mpapa na hivi sasa nayo yanashughulikiwa. Mhe. Mwenyekiti, mimi naipongeza idara hii kwa kuona wananchi wanapata maisha bora ikiwa yuko mjini au kijijini. Kwa hivyo, hivi sasa Mpapa nao wanalala kwenye nyumba za ghorofa pamoja na Gamba na kwengineko. Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ni adimu kwa mnyonge kulala kwenye ghorofa lakini sasa hivi yameshakuwa ni mazoea mjini na vijijini watu wanalala kwenye maghorofa.

Mhe. Mwenyekiti, pia naipongeza serikali kuweka Bodi ya Nyumba, lakini kuna mapungufu makubwa. Mhe. Mwenyekiti, nasikitika sana kuona Afisi ya Bodi ya Nyumba hairidhishi. Wiki iliyopita nimemkuta Hakimu anafanya kazi kwenye gari yake, mafaili anapelekewa pale, nikamuuliza vipi au ndio masika zinavuja akasema hapana mle ndani hamna kiti cha kukalia mimi, mchafu hairidhishi kwa hiyo nimeona kazi zangu nifanye hivi hivi. Isipokuwa kwenye vikao vya bodi kuna ukumbi ndio anakwenda humo, lakini afisi yake hasa haipo. Jana mimi nikasema hebu nende, kweli nimekwenda nimeona aliyonambia ni kweli hata zile faili za kesi zimewekwa ziko chini hakuna hata *shelf.*

Kwa hivyo, hapa pana mapungufu kwa sababu bodi ile ni sawa sawa na Mahakama lazima iwe na hadhi na zile document ni vitu muhimu lazima kuwe na mahala maalum. Pia na yule Hakimu anataka muda kama ni afisi yake aweze kufanya kazi zake. Kwa hivyo, mheshimiwa naiomba wizara ishughulikie afisi ile ili Hakimu yule aliyepewa kazi pale awe na mazingira mazuri ya kuweza kufanya kazi na mtu yeyote anayekwenda pale ajue kwamba hii ni afisi ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nakuja katika Mamlaka ya Maji hawa mimi nataka niwape pongezi kwamba wanajitahidi sana kutupatia maji kwa sababu kwa takwimu wanazotupa kila siku ni kwamba kiwango cha uzalishaji wa maji kinakua lakini maji hayatoshi. Hapa sasa hivi nimemsikia Mhe. Salmin hivi sasa

akizungumza suala la maji. Ni kwamba kiwango hakitoshi kwa sababu na sisi kila siku tunakua wingi wetu unakuwa mkubwa kuliko uzalishaji wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, sio kama idara haitowi maji lakini speed ya uzalishaji maji imepitwa na uzalishaji wa watu. Kwa hivyo, nafikiri ni kwamba uzazi wa mpango uende taratibu ili tufuate maagizo ya wataalamu wetu ili mambo yetu yaende sambamba, angalau *speed* ya uzalishaji wa majina, uzalishaji wetu uwe sambamba ili kile kitu kinachozalishwa kiweze kukidhi wale watu tuliomo, la si hivyo tutakuwa na matatizo. Kwa sababu kila tukiwa wengi nchi itazidi kuwa masikini hata tukajitahidi vipi kuzalisha au kuinua uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo hayo maji mengine yanayopatikana baadhi ya sehemu hayafiki vizuri kutokana na matatizo ya kitaalamu. Kwa mfano, mitambo ya Unguja Ukuu inayotakiwa kupeleka maji mpaka Uzi sasa hivi haina uwezo, watu wa Ng'ambwa hawapati maji na walikuwa wakipata maji kama kawaida. Vijiji vidogo vidogo vya Bungi, Kikungwi havipati maji.

Sasa nafikiri Mhe. Mwenyekiti, wizara ishughulikie, mle mwahala ambamo mmeshawekwa miundombinu wataalamu wetu wahusika watumie mbinu zao ili maji yale yaweze kupatikana. Kwa sababu bado kwa takwimu ziliopo maji yaliyomo zisiwani mwetu kwenye ardhi ni mengi sana na tunaweza kutumia sisi bila ya matatizo. Lakini tatizo sasa ni uzalishaji wetu speed yetu imekuwa ndogo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tujitahidi na katika jimbo langue neo la Tunguu pamoja na Mji mpya kuna matatizo hayo ya maji.

Lakini pia tuna mji mpya wa Tunguu, mimi nina wazo jipya Mhe. Mwenyekiti, kwa serikali na nilitoa katika hotuba ya bajeti lakini naona nitumie nafasi hii. Ili tupate mji mzuri mpya wa Tunguu basi lazima tuweke mamlaka, zitasimamia ujenzi na kuelekeza namna gani kama wenzetu walivyoamua mji wa Dodoma wajenge, wameweka mamlaka ya *CDA*, lakini sisi pale wanakatiwa viwanja kila mmoja anataka ajenge lililobakia sasa hivi ni watu wanafanya biashara, unakatiwa kiwanja kesho wanauza, ujenzi hawendi unakwenda pole pole, halafu kuna viwango viwanja vya *plan* vinataka gharama lakini mtu wa kawaida atataka mle mle.

Kwa hivyo nafikiri lile lengo la kuwa na mji wa kisasa pale halitofikiwa, lazima serikali ifikirie kuweka chombo kama hiki cha mamlaka kama kweli tunataka kufanya mji mdogo wa kisasa ili twende na wakati. Mji Mkongwe tushafanya mamlaka kwa nini mji mpya hatuwezi kufanya mamlaka? tukaweza kubuni mambo mbali mbali, majengo na hivi sasa kuna vyuo vikuu, nyumba za viongozi wakubwa, numba ya Mkuu wa Mkoa, Makamo wa Rais. Kwa hivyo, lazima hivi sasa kama mji ule tunataka uwe mzuri basi Mhe. Mwenyekiti, serikali ifikirie kuweka mamlaka ya kusimamia upimaji, usimamizi, ili uwe mji wa kisasa kabisa.

Lakini hata hivyo, ili matayarisho hayo ya wale ambao wameshapata viwanja basi huduma za maji zianze kupelekwa ili waweze kushughulikia ujenzi, la si hivyo viwanja vitawashinda.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Nishati. Mafuta, zinakuja meli hapa lakini kunakuwa na kero linaudhi. Upungufu wa mafuta wa mara kwa mara unaudhi Mhe. Mwenyekiti, na hapa kampuni kubwa iliyopewa dhamana ni *GAPCO*. Ninavyojua Mheshimiwa na wewe ulikuwa wizara hii inayoshughulika na nishati tangu zamani, kila mwaka nakumbua mimi kulikuwa na sheli *BP, CALTEX*. Serikali ilikuwa inatiliana mkataba na kampuni moja wapo ambayo ni dhamana kwa kuhakikisha hapa nchini hapana upungufu wa mafuta.

Sasa nitaomba Mhe. Mwenyekiti, waziri anambie, kampuni gani hasa ameipa dhamana ya kuhakikisha hii nchi yetu haikosi mafuta. Kusema biashara huru ndio mambo hayo yanafikia hapa, ikiwa utaratibu huu tumeuacha wa kuichagua kampuni moja serikali ikaingianayo mkataba kuhakikisha mafuta yanapatikana nchini, tukasema tu biashara hii huru ndio tatizo hili tunalipata. Bei zinapandishwa kiholela.

Hivi sasa mafuta Mhe. Mwenyekiti, yameshapandishwa, mafuta sasa shilingi 1,650 sijui, bila ya kutoa taarifa wala tangazo. Unakwenda hapa unasikia bei shilingi 1,800 hakuna tangazo. Basi Mhe. Mwenyekiti, nasema mambo haya ya mafuta tusiyafanyie mchezo, kwa sababu ni muhimu sana kwa viwanda vyetu, maisha ya kila siku, kwa magari yetu. Kwa hivyo, lipo tatizo juu ya mafuta. Na kama ipo kampuni iliyopewa dhamana hiyo na kwa kipindi fulani tumepata matatizo basi serikali lazima ifidiwe hasara

waliyoipata wananchi. Sasa kwa niaba ya wananchi na serikali ilipwe fidia na kampuni hiyo, ambao kwa muda mwingi imepoteza tulikuwa hatuna mafuta katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla baada ya hayo mimi niipongeze sana Wiara hii ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa kazi za kila siku. Baada ya michango hiyo ambayo nimeitoa, sasa niende katika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye usafiri wa baharini, wawekezaji kutuletea mameli malbusi kunaudhi. Serikali kusema wawekezaji wetu hawana uwezo basi bora kama hakuna wafanye ubia, Machano, Mkema, Mati tushirikiane lakini tulete kitu cha uhakika, sasa tuna makampuni tele ya meli lakini kazi yao kuleta meli mbovu siku mbili utasikia imewaka, imefanya nini, namna gani jamani nchi hii? Huu si utaratibu Mhe. Waziri kiserikali, ustaarabu wa biashara ubia, kama mtu hawezi pesa zake kidogo amwite kaka Nassor Mazrui hebu njoo, samahani ee, Sheikh Abubakar njoo, mnaunga mnafanya ubia, kampuni sio lazima uwe peke yako, lakini mnafanya biashara ya uhakika ambayo wananchi wanaifurahia. Lakini kuweka utitiri wa wafanyabiashara ambao wanaweka huduma mbovu Mhe. Mwenyekiti, huu haukubaliki. Kwa sababu usafiri huu unahatarisha maisha ya watu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi bado kwa nitakuwa siridhiki kwa wawekezaji kuleta meli mbovu halafu tukaambiwa wawekezaji tunao pesa zao ndogo, aa, wao binadamu wana akili. Biashara si lazima kuuza pekeyako na kila chombo kikiwa na usafiri cha uhakika na kizuri watu watapenda na abiria mtapata wengi na kupata tija. Kwa hivyo, nafikiri suala hili lifikiriwe na waelezwe hasa wafanyabiashara. Wananchi hawapendi kupandishwa vyombo vibovu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine huduma za barabara. Nashukuru watu wa Idara ya Barabara na mtandao mzima wa barabara na miradi iliyopo kweli miradi mingi, mahitaji mengi yanatakiwa kwa wakati mmoja, hata zana tumezizidi. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, tuwashukuru, kazi zinakwenda vizuri lakini pia na maneno mazuri wanayotupa tuwaridhie kwa sababu maneno mazuri humtoa nyoka pangoni.

Mimi nilikuwa bado nina njia zangu mbaya nyingi hazijatimia lakini maneno tunayopewa na serikali yananiridhisha. Kwa hivyo, nashhukuru, sijapata barabara ya Pongwe/Jumbi wala ya Cheju/Ungujaukuu, lakini maneno ninayopewa na serikali yananiridhisha na mimi naweza kupata angalau jawabu ya kuwaambia wananchi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri juu ya kuwa naridhika lakini mjitahidi hizo barabara zangu mnitizamie ili wananchi waridhike kwa vitendo juu ya mambo haya.

Jengine katika idara hii ya barabara naomba utunzaji wa barabara hasa pale Miembe Mingi, Bungi. Hatari nyingi zimetokezea, wengine wakatia itikadi kwa sababu msikiti mbovu umeanguka, watu wanajenga msikiti, lakini bado barabara mbovu nayo tuna hakika itaendelea kuto aulinzi.

Niliwahi kumueleza Mhe. Waziri akanambia hakuna mashimo barabara laini kama ngisi si kweli, barabara ya Bungi imekaa kama mgongo wa kasa, sio ngisi. Barabara ya Bungi, Miembe Mingi kama mgongo wa kasa, Mhe. Mwenyekiti kesho unaweza kwenda ufuatane na Mhe. Waziri ukapite uione ishachoka.

Baya zaidi Mhe. Mwenyekiti, misingi ya maji wananchi wanaibomoa, wanachukua udongo kupeleka mahotelini kuuza lakini hakuna mchungaji. Hili linatisha na maji ni sumu ya barabara, kutuama maji kwenye barabara hata akaijenga nani mwaka mmoja itakuwa mbovu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, pia uchukuaji wa udongo nao usimamiwe, huu unapuuzwa na ndio unaosababisha barabara zetu mara kwa mara zinaharibika na kuleta mipasuko.

Jengine nakwenda kwenye bandari yetu hiyo ndogo ya kupandia vyombo vidogo vidogo. Kwa ujumla niwashukuru Sirika la Bandari kujenga sehemu za kuhifadhia abiria pale Wete jengo zuri sana, Mkoani safi kabisa, sasa nataka na pale Mkokotoni wajenge vile vile kama ni bandari kwa kiasi cha watu wanaokuja. Ingawa tunazungumza kwamba bado hapajakuwa na abiria wa kwenda na kurudi, lakini abiria wanakuja na wanapokewa pale, basi hao wa *emergency* ndio pawe na nyumba kwa abiria, wale ambao wameruhusiwa angalau kuweza kufikia pale.

Lakini Malindi kwenye gati yetu ya kupandia abiria kwa vyombo vinavyokwenda kwa kasi pana matatizo. Matatizo ya kwanza sehemu ya abiria kungojea safari zao hapana na hapatoshi. Lakini hata viongozi pia wanataka kukaa nao vile vile sehemu yao hapana.

Wenzetu Dar es Salaam pale sijui kampuni gani pana kisehemu japo kidogo lakini tunaridhika, unafika pale *VIP* mheshimiwa, mwenginewe, unakwenda mgeni unapata chai, maji unapata kunywa, unakwenda msalani unajisaidia, lakini pale jumla jamala hujui mheshimiwa, mchukuzi, hujui nani, kwa kweli haparidhishi.

Hata hivyo, pale nje zogo liliopo niiulize hasa serikali, hivyo Mamlaka ya Bandari au Shirika la Bandari na Baraza la Manispaa lina mkataba gani? Kwa sababu watu wa Baraza la Mji pale wanapafanya fujo mlangoni, gari ya *taxi* ikileta abiria pale wao weshafika, dereva akiteremka kumpa mzigo wake gari ishafungwa mnyororo anamwambia ume-*park.* Sasa kweli utakwenda pale abiria wengine watu wazima afungue mlango tu ampe mzigo wake asiteremke? Wameona wapi mambo haya? Akiteremka anaambiwa dereva ume-*park* linalita mnyonyoro gari alipe shilingi 18 elfu.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili lazima wawekewe maeneo Baraza la Mji na watu wa Bandari kwa huduma mbali mbali, la si hivyo wanachafua utaratibu mzima pale wa usafiri.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk wamemfanyia, Mhe. Ali Abdalla Ali, ukifika pale lazima dereva ateremke akufungulie mlango, kama mheshimiwa begi lako akupe lakini akiteremka tu dereva anaambiwa ume-*park* kwa sababu huko kwenye sukani. Mimi sijapata kuona mambo haya. Na kwa nini Idara ya Mawasiliano inawaachia, mamlaka gani mliowapa wale pale, wanakuchafulieni bwana, halafu wameweka mistari mpaka chini ya mlango uki-*park* gari wanachukua pesa. Lazima pale penye geti watakuja abiria wengi kuingia na kutoka lazima watu na madereva wa *tax* wawe na eneo lao la kujidai, lakini wanavizia, *Wallahi Laadhim* huwa wanavizia, akiteremka dereva anatoa mzigo kwenye buti yeye keshatia mnyonyoro halafu anakimbia.

Mhe. Mwenyekiti, kama waziri hajaona naomba aende hivi hivi jioni atawakuta. Kwa hivyo, hili bwana hatulifahamu vizuri. Lakini pia tumefikia kuwa na utaratibu wa kujenga *parking* mle. Lakini hivi sasa nasikiri gati ya zile meli ndogo ambazo zilikuwa zikitumia Forodha Mchanga zitakuwa zikitumia pale pale. Hivyo wakati huo huo sehemu tuliyovunja banda wakati tutapoweka *park* ya magari patakuwaje?

Kwa sababu ile meli inapoteremsha vitu vikubwa halafu pale unakwenda kuweka *park* ya magari kama tunavyoambiwa, mimi nafikiri hili ni tatizo na sijafahamu hasa. Mambo mawili, hivi sasa mradi ule wa kufanya gati ya meli ya kasa na meli nyenginezo zile, unaendelea, lakini wakati huo huo tunaelezwa kuwa banda lililokuwa *port marine*, Shirika la Meli likiuzwa tiketi litafanywa *park* ya magari. Mimi bado sijafahamu kwa eneo lile ninavyoliona, kwa sababu naliona machoni, hapatoshi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hapa nitapenda nipate maelezo ya kutosha ili na mimi niweze kuelewa.

Sasa nimalie na Idara ya Ardhi. Mhe. Mwenyekiti, nilisahau jambo moja katika idara hii, siku zote idara hii inawapa watu viwanja kwa wale watu wanaohitaji. Lakini nina masikitiko, mimi nimepewa kiwanja Matemwe japo ninakaa Kikungwi, lakini nimeridhika kwa sababu mimi haja yangu pa kuishi na mtu anaweza kuishi pahala popote kwa mujibu wa katiba. Lakini mpaka leo sijakabidhiwa, naambiwa watu wa Matemwe hawataki sijui inakuwaje, sisi mbona Tunguu pamepimwa na tumewaachia watu wamepewa wa huko huko Matemwe.

Watu wa Matemwe kina Mhe. Ame Mati Wadi nina hakika tumewapa, kwa nini leo mimi Haji Mkema Haji nipewa kiwanja Matemwe mpaka leo sikabidhiwi naambiwa watu wa Matemwe hawataki inakuwaje serikali inashindwa kusimamia hili?

Hili Mhe. Mwenyekiti, naomba nijibiwe. Huu mwaka wa pili nimeshapewa warka wangu kanionesheni naambiwa aa watu wana ugomvi kule kwa sababu wenyewe wamesema hivi. Wamehamishwa watu na walikuwa wakiishi na nyumba zao, lakini serikali imeweza kuzungumza nao ondokeni hapa kaeni pale au

na wewe tunakupa hapa. Hapa atakaa Mhe. Machano Othman Said, hapa Mhe. Abubakari Khamis na wamekaa, leo Matemwe tunahangaishwa mwaka wa pili viwanja hatujapewa kwa nini? (*Kicheko*)

Suala hili Mhe. Mwenyekiti, ni zito naomba nijibiwe. Baada ya hayo nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa tuna ripoti hii ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, ripoti za wizara mbili. Tunatarajia leo leo tuzungumze Ripoti ya *PAC* ili Jumamosi tuzungumze Katiba na Utawala Bora na kufunga Baraza mapema kabla ya saa saba au saa saba. Sasa tukiendelea na utaratibu huu sitaki ku-*bulldoze* kwa sababu ile siku ya semina niliambiwa nina *bulldoze* aa, natoa ushauri tu, tuendelee mpaka Jumapili, lakini tujaribu kuchangia ripoti tusirudie yale kwa yale kwa sababu bado kuna watu kama sita hivi wamebakia sasa kazi kwetu.

Ikiwa tutaendelea hivi basi tutaendelea, Kamati ya *PAC* itasomwa Jumamosi kama mpaka jioni Jumamosi haya. Sasa tuweke wazi tuelewane tufuate muda na mengine tuweke kwenye bajeti. Kwa sababu sasa naona tunachangia bajeti, tuchangie ripoti tutoe maelezo lakini tuchunge muda ili tuweze kumaliza hili na tuingie kwenye Kamati ya *PAC* na tuchangie. Kwa hivyo, niliona niweke wazi hayo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakushukuru na nimekuelwa mantiki yako kwamba tupunguze muda.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja niende kwenye ripoti hii na kwanza niipongeze Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kamati ambayo mimi nilikuwa nimo na niliipenda sana. Kamati hii kwa kweli ndio inayosaidia maisha ya watu wa Zanzibar. Kwa hivyo, nichangie kwanza kwenye Idara ya Barabara na moja kwa moja niende kwenye ujenzi wa barabara za Kusini Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa na kilio kwa watu wote wa Kusini Pemba kwamba tuna hali ngumu ya barabara, lakini nashukuru uongozi wa Mhe. Rais Karume ulikubali kilio chetu na kututafutia mfadhili na wakatupatia miradi sita ya barabara ya Kusini Pemba. Mimi nilijenga hoja kwamba hatuwezi kujenga barabara ya Kusini Pemba bila ya kuanza barabara ya Matmbile/Mwambe. Kwa sababu ndiko kwenye mahitajio yote ya ujenzi wa barabara kama vile kifusi, mawe na mambo mengine. Nashukuru pia serikali ilisikia kilio changu na barabara ya Mtambile/Mwambe ilianza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hatua hiyo nataka niipongeze serikali na nimpongeze Mhe. Waziri kwa kukubali kilio cha watu wa Mwambe. Lakini pamoja na uzuri huo hakuna uzuri usio kasoro, nimesema kwamba nisisubiri ushahidi wa kinyamwezi. Wenzangu wa Bumbwini na Dunga walipokuwa wakiambiwa barabara *Prismo* walikuwa wanafanya masihara. Kwa hivyo, mimi nimetishika nimesema kwamba niseme mwanzo yasije yakatokezea yale ya Bumbwini na Dunga.

Mimi kama Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani nilikuwa nikifuatilia ujenzi wa barabara ya Mtambile/Mwambe na kupata maelezo kwa wataalamu wa ujenzi, lakini kwa ufupi kasi inayokwenda nimetilia wasi wasi kwamba yale ya Bumbwini yanaweza yakatokezea Mwambe.

Barabara hizi sita zimepewa miaka mitatu, Mtambile/Mwambe, Mtambile/Kangani na Wambaa ni mwaka mmoja na nunsu. Hadi sasa barabara ya Mwambe tumetumia takriban miezi tisa. Najiuliza barabara mbili za Wambaa na Kangani miezi mingapi zitatumia ili mwaka mmoja na nusu tuweze kumaliza barabara hizi?

Mhe. Mwenyekiti, nimefanya utafiti na kuuliza maswali nimegundua kwamba kwanza kuna uchache wa vifaa, doza moja hilo limegeuka kama kinu cha mganga, linatembea barabara zote tatu za Wilaya ya Mkoani. Asubuhi utaliona kwenye gari linaelekea Kangani, saa saba liko kwenye gari linaelekea Mjimbini na saa kumi linaelekea Mwambe na Wambaa. Ni tatizo, ikiwa doza moja hilo ndio ujenzi wa barabara sita za Kusini Pemba basi miaka mitatu ile iliyopangwa itaongezwa tena na mitatu na mitatu na mitatu hatuwezi kumaliza ujenzi wa barabara hizi. Kwa hivyo, vifaa vya ujenzi wa barabara hizi ni vichache na lazima Mhe. Waziri hili aliangalie upya.

Lakini pia nimegundua kwamba kuna ucheleweshwaji wa makusudi wa barabara hizi, kwa nini nikasema hivyo? Kwa sababu mimi sioni mantiki kwamba wafanyakazi wanafika kwenye *site* lakini wanashindwa na kupata kokoto kwa sababu ziko Vitongoji. Ukiuliza unaambiwa gari hazina mafuta, mimi sielewi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi huna cha kunambia kwamba barabara imekwamba kwa sababu magari ya kuchukulia kokoto Vitongoji hayana mafuta. Nadhani kuna mbinu makusudi ya kucheleweshe baadae ilaumiwe serikali kumbe pengine kuna mkono wa kuwadekeza wasimamizi kwa makusudi. Na haya ndio madhara ambayo *Prismo* yalimkuta na hatimaye akatuharibia.

Kwa hivyo, kwa sababu mradi fedha zipo, sioni mantiki kwa nini kokoto kutoka Vitongoji zishindwe kuchukuliwa kwa sababu ya ukosefu wa mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka nipate ufafanuzi ni teknolojia mpya ambayo katika barabara ile tunaitumia na kuhusu *labor power*. Niliuliza nikaambiwa kwamba kila mita 50 wanatakiwa wafanye watu 35, lakini hivi sasa wanaregeza *base* kwa mita 30. Kwa nini, kwa sababu ya ukosefu wa vyuma, sio madoza ni vyuma ambavyo vimetengenezwa Tanga vipo pengine na Dar es Salaam vipo. Kwa hivyo, ukimwambia mtu kwamba vyuma havipatikani jambo la kununua pengine Tanga mimi Mhe. Mwenyekiti, sioni mantiki. Kwa hivyo, nadhani ni usimamizi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningetaka Mhe. Waziri anifahamishe nilipata kuambiwa nilipotembelea kwamba wafanyakazi walitakiwa walipwe shilingi elfu moja ya Kenya kwa mujibu wa mkataba, lakini leo wanalipwa shilingi elfu tano ya Tanzania. Sasa je, kama shilingi elfu moja ya Kenya maana yake ni shilingi elfu 12, ikiwa leo walipwe shilingi elfu tano ningetaka kujua kuna tatizo gani la upungufu huo.

Jengine ambalo ningezungumza ni barabara ya Magomeni aliyozungumza Mhe. Salmin Awadh ambayo sasa inaitwa mwanandani. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Wazanzibari wanapotea sana, nasaha zangu hapa Mhe. Waziri afanye busara barabara ile baada ya kuitwa mwanandani kesho iitwe pepo kwa maslahi, sasa ijengewe vile vikuta vilivyokusudiwa ili tupunguze maafa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningelisema hapa ni kuhusu Idara ya Anga kwamba tumependekeza kamati kuwa ifanywe mamlaka na mimi naunga mkono. Kwa sababu sisi tunaamini kwamba ikiwa ni mamlaka basi mapato na uendeshaji mzuri utaimarika.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bandari ni shirika ambalo linaongoza kwa sifa, lakini linaingia dosari ndogo sana. dosari yake ni kwamba Gati ya Mkoani hivi leo kwa kweli ni aibu, kwanza sifa yote ile ya Shirika la Bandari inaharibiwa na kutuwama kwa maji pale Gatini Mkoani. Sasa ikiwa hatuwezi kujazia pale basi angalau tutafute wafanyakazi wapige deki. Kwa sababu huko kupiga deki ni gharama ndogo, lakini leo ukifika pale masika haya ni maji juu gati nzima karibu ya magotini ni aibu. Kwa hivyo, ule uzuri wa Shirika la Bandari nadhani hapa utakuwa unaondoka na Mhe. Waziri nadhani hili gharama yake ni ndogo sana. kufuta maji yale ni gharama ndogo na kama haiwezekani basi angalau kwa dharura tungeweka mchanga kwanza ili maji yale yasituame.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni Afisi ya Mrajis wa Meli. Nilisema kwamba kuna tatizo ambalo Mhe. Waziri leo asubuhi amenijibu lakini sikuridhika la tiketi ambazo zinauzwa kwa njia ya ulanguzi. Mhe. Mwenyekiti, imekuwa ni kawaida kwa wananchi wa Zanzibar kununua tiketi kwa njia za ulanguzi. Tiketi ya boti shilingi elfu 20 baada ya masaa mawili kuuzwa basi watu huwa wananunua shilingi 35 – 40. Nina hakika wafanyaji wa biashara hii wanajulikana, sasa nchi hii tumepitisha sheria ya fedha chafu, sasa ikiwa sheria tumepitisha juzi na watu wanajipatia kipato kwa tiketi za ulanguzi ni hatari kubwa.

Sasa ushauri wangu mimi serikali itangaze rasmi kwamba mwananchi atakayeuziwa tiketi ile ya ulanguzi basi mtu huyo apelekwe polisi na tuweze kuzuia uhalifu huu. Vyenginevyo kama hilo gumu mimi nitaamini kwamba hii ni biashara ambayo watu wanaijua na kwa kweli itakuwa serikali wanachangia kuwepo pale.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ningesema ni kwamba tusisubiri mengine Mwenyezi Mungu akatuhukumia. Wawakilishi humu walikuwa wakilalamika sana kwamba jamani Meli ya Serengeti mbovu mna saruji,

lakini juzi serikali ilivyokuwa ikitetea kama kwamba ile meli ni mpya imetoka leo kiwandani, hatimaye Mwenyezi Mungu amehukumu na watu wakapumzika. Lakini tusiwe na tabia hii, wawakilishi wakisema jambo maana yake hapo pahali pana madhara, si wataalamu sote lakini jambo linaonekana na tusisubiri kwa Mwenyezi Mungu mpaka achukue hatua ya kutuhukumia.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni Meli ya MV. Maendeleo. Kamati wamesema kwamba walikwenda wakaiona na wameandika ripoti, ingawa ripoti hiyo hatujaiona lakini ningetaka kujua meli hii lini itakuja hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka kwenye maeneo hayo sasa niende kwenye barabara ya Mwambe ambayo Mhe. Waziri nilimuandikia barua ili tuokoane kwa sababu ni kipindi cha uchaguzi. Mhe. Mwenyekiti, sina lugha nitakayoielewa ikiwa sikupata ziara ya Mhe. Waziri na akaona uharibifu ambao Mwambe umefanyika baada ya ujenzi wa barabara ya Mtambile/Mwambe. Nyumba nne zimezama kwa sababu ya kukusanya kifusi kwa nia njema tu cha kujengea barabara, lakini kumbe ilikuwa ni njia ya maji na maji yametuama nyumba zimeingia maji.

Nimeripoti Pemba mara tatu sijapata msaada, nakuomba twende ili tuokoane mimi na wewe tuwakilishwe mwakani.

Jengine ambalo ningeliomba ni barabara ya Mgagadu/Kiwani, leo asubuhi bahati mbaya tumepata msiba wa sheikh kule, lakini watu kutoka Chake Chake, Mkoani, Pujini na sehemu nyengine wamelazimika kuweka magari yao Mgagadu na kwenda Kiwani kwa miguu kwa sababu barabara imekatika. Sasa hadi naingia humu saa kumi na moja napiga simu naambiwa juhudi ya wizara haijapita. Naomba sana, sana sehemu ile ifukiwe kwa dharura ili magari yende Kiwani kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa Kiwani.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niache suala hilo niende kwenye Wizara ya Maji na kwa kweli sina mengi isipokuwa niwasifu tu, kwa juhudi zao na waendelee kufanya bidii hizo na kwamba Shirika la Umeme wasibweteke. Tukio ambalo lilitokea la miezi mitatu kukosa umeme Wazanzibari wakawa kimya, ni heshima kubwa kwa Shirika la Umeme. Na sikwamba tulikuwa hatuoni matatizo, lakini tulithamini juhudi zenu na tulijua kwamba hili suala ni la bahati mbaya.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, wananchi wa Msengele waliomba serikalini kupelekewa huduma ya umeme na Mhe. Naibu Waziri namshukuru sana alikuwa mstari wa mbele kutusaidia suala hili. Hadi sasa wananchi hao wamekwisha kuwasilisha shilingi milioni nne taslimu kwa ajili ya mchango wao wa nguzo. Ningeomba Mhe. Waziri unambie huduma ile ili Warabu wale wanipatie kura itakamilika lini.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa baada ya kuwashwa huduma ya umeme hivi karibuni, eneo la Kianga daraja la kwanza bahati mbaya hakuna duhuma ya umeme na sababu hatujui. Sasa ningeomba Mhe. Waziri ujue hilo kwamba watu wa Kianga Daraja la Kwanza mpaka maeneo ya Dole kule hawapati huduma ya umeme kwa sababu kuna hitilafu pengine ya transfoma au waya sehemu fulani. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba ufuatilie hilo ili kuwapatia maslahi wananchi hao.

Mhe. Mwenyekiti nashukuru.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuchangia Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya mwaka 2009/2010. Mhe. Mwenyekiti, mimi sichambui wizara kwa wizara nitazungumza kwa jumla kila wizara itachukua linalomhusu.

Kwa hivyo, katika taarifa hii ukurasa wa 60 pana Idara ya Leseni, hapa nilikuwa nataka nipate maelezo tu kwamba katika Sheria ya Mawasiliano imesema kwamba madereva wote sasa hivi watapata leseni kupitia skuli maalum zinazotambulika. Unasoma katika skuli hizo halafu unapatiwa leseni baada ya kufanyiwa majaribio yote na kupasi. Lakini bado naona njiani wamo watu binafsi wanafundishana mtu na ndugu yake, mtu na mkewe, mtu na mwanawe. Sasa je, Mhe. Waziri watu kama hawa ambao wanaonekana wanavunja utaratibu hakuna sheria inayoweza kuwakamata.

Lakini la pili hivi sasa njia nyingi zimeanza kufungua gari zake. Utakuta kuna gari kuanzia *Spice* hapa, kuna Mbuzini, kuna kwetu Kama, Mwachealale na nyengine zinataka kufunguliwa kwendea Uwandani, kwenda Zingwezingwe. Nilikuwa nataka niulize je, kama kuna mtu anataka kufungua njia anafanya utaratibu gani. Ningeomba na hili Mhe. Waziri pia akanipatia ufafanuzi.

Halafu ukurasa wa 62 Shirika la Bandari niwapongeze kama walivyopongeza wenzangu. Nilikuwa na mazonge mengi hapo lakini Mhe. Haji Mkema Haji kayamaliza nimebakia na mawili. Moja serikali kupitia shirika inapowaachia biashara kupeleka kwa watu binafsi hutegemea kwamba wananchi wapate manufaa na urahisi zaidi. Lakini kadri hivi sasa meli zetu wafanyabiashara wakileta badala ya kupungua bei lakini bado inamkandamiza abiria.

Hapo hapo mwenzangu aliyemalizia kazungumza kwamba pia wanauziwa tiketi za ulanguzi. Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia wizara na shirika kwamba na hili lizingatiwe kwa manufaa ya wananchi wetu kwa sababu wengi wao ni wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kubwa zaidi ambalo nadhani na wenyewe watalisema kwamba hivi sasa meli madhubuti hasa ya kwenda kisiwa cha Pemba haipo. Watu waliitegemea Serengeti imeshawaka moto, MV Mapinduzi imekufa, MV Maendeleo imekufa. Sasa tunaomba pia serikali iangalie kwa sababu meli nyengine kwenda Pemba unaweza ukaingia usiku wa leo ukalala kucha, ukapiga na kutwa, ukafika siku ya pili. Sasa ile kwanza ni usumbufu, ndani ya meli joto, watoto, chakula chenyewe haba mle. Ningeiomba serikali na hili wakalitazama wakatafuta mwekezaji akaleta meli ya uhakika ikaweza kuondosha kilio cha Pemba.

Mimi sikai Pemba lakini nimeoa kuna wanangu kule, wakwe zangu, sasa siku ninayotaka kwenda Pemba sasa hivi nakwenda kwa ndege na ndege ni gharama kubwa kwenda na watoto na kila kitu. Sasa naiomba serikali kupitia wafanyabiashara tutafute meli ya uhakika kama MV Mapinduzi ama MV Maendeleo ama kubwa zaidi ya zile ili kuweza kuondosha tatizo hili la safari za Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije ukurasa wa 69 Taarifa ya Maendeleo ya Mradi wa Maji Mkoa wa Mjini Magharibi. Mhe. Mwenyekiti, nichukue awamu ya pili niiishukuru serikali na wizara kwamba sisi majimbo matatu Bumbwini, Mfenesini na Kitope tumefanyiwa mradi na tayari tunashukuru umeshachimba visima vitatu, umeshajenga tangi unamalizia na sasa hivi tayari tumeanza utaratibu wa mabomba.

Kwa hivyo, tunashukuru kwa hatua iliyofika na tunaomba bado serikali ifanye jitihada ili mradi huu uweze kukamilika. Tunawapongeza sana kwa hatua waliyofikia na wananchi wamenituma nitoe salamu hizo kwa serikali pamoja na wizara inayohusika. Tunashukuru sana na tunaahidi kwamba tutashirikiana mpaka mradi uweze kukamilika.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kwenye taarifa hii nije ukurasa wa 74 Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe. Mhe. Mwenyekiti, juzi hapa tulipata kama semina juu ya mji wetu huu. Kwanza mji wetu umebahatika kuwa Mji wa Urithi wa Kimataifa. Lakini kwa hali tunayokwenda tumekuwa tuko hatarini kwa sababu ule mji tunaugeuza sasa hivi hauwi tena Mji Mkongwe tunataka tuufanye labda mji mpya. Miji mipya tunajenga Michenzani upo na sasa hivi tuko Tunguu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana serikali kupitia wizara inayohusika kwamba hili suala tusilichezee lazima tuweke jitihada bado mji wetu utambulikane kitaifa kwa sababu tunapata misaada mbali mbali na tunapata kuheshimika katika dunia. Sasa tukenda mpaka tukafutwa katika hifadhi ya miji mikongwe ya dunia kwanza itakuwa tumepoteza nafasi hiyo na kitu ukipoteza hakirudi tena. Sasa nasisitiza kwamba hili lizingatiwe, biashara zote ambazo hazielekei kuwekwa Mji Mkongwe ziondoke kwa sababu maeneo ya kufanya biashara hizo yapo.
Kwa mfano, vinyago watu wakauze kwenye mahoteli Kiwengwa, Matemwe, Nungwi na kwengineko. Masuala mengine yote ambayo hayastahiki kule basi tungeomba kisheria likaondoshwa na sheria imeshapita ili tuweze kuulinda mji wetu na sisi tupate hadhi katika ulimwengu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika mchango wangu kwenye taarifa hii nije ukurasa wa 77 unaozungumzia juu ya mradi wa awamu ya pili ya umeme kutoka Ras Kiromoni kuja kwetu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu tulipoelezwa hapo mwanzo na hata taarifa inasema kwamba utaanza au kumalizika mwaka 2013. Tuliwahi kusema katika muda tuliokuwa tumepata matatizo kwamba muda huo ni mkubwa sana na tukaomba serikali izungumze na hao wanaotaka kutusaidia ili angalau wapunguze muda na tukasikia kazi hiyo serikali wameifanya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri kama ni kweli leo tupate taarifa rasmi kwamba hawa wenzetu kutoka 2013 wameshusha mpaka wapi, 2011 Disemba, 2012 ama wamebaki kule kule. Kama wamebaki kule kule je, dharura imechukuliwaje. Labda majenereta ya dharura yapo na tayari yanafungwa ama yameshanunuliwa. Sasa hili pia tupate taarifa ili tuweze kuwajulisha wananchi wetu tuwe na kitu cha uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa sababu umenambia kuna watu wengi na umenipa kwa heshima nije ukurasa wa 80, hapa inazungumziwa Idara ya Utawala wa Ardhi lakini hasa haja yangu sehemu inayozungumzia Usimamizi wa Ardhi za Eka. Humu taarifa imesema kwamba tayari hivi sasa wanahakiki eka katika maeneo mbali mbali. Ilikuwa Kianga, Dole, Bumbwisudi, Kizimbani, kwangu mimi Mbuzini, Chuini na Mfenesini.

Lengo na dhamira mimi hasa sikupata kufahamu, sasa naomba wizara inielekeze kwamba hizi eka wakishakuhakiki wajue kwamba bado zinadhibitiwa na wale wale waliopewa hapo mwanzo, ama wanataka wajue ngapi zimebaki. Kwa sababu nyingi watu wameshauza na zimeshamalizika watu wameshajenga. Sasa je, wakihakiki kubwa hasa tatizo lao wanataka wapate nini kwamba zipo, ama waliovunja utaratibu wa eka achukuliwe hatua, ama kitu gani. Naomba nipate ufafanuzi juu ya uhakiki huu lengo lake ni kitu gani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba nitoe nafasi kwa wenzangu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia jioni hii. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kuniweka hai mpaka sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nawashukuru sana Wanakamati, Mawaziri wa Wizara zote hizi mbili pamoja na Makatibu, Wakurugenzi na watendaji wao kwa jumla kwa kuwa wasikivu wazuri kutokana na kamati inavyowafahamisha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwenye Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuna mambo ambayo kidogo ningeomba ufafanuzi na kuna mambo mengine ambayo nitoe ushauri wangu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nishukuru sana kupata barabara nzuri katika jimbo langu hasa barabara hii mpya ya juzi iliyounganisha kuanzia Mchangani hadi Kilombero/Pangeni mpaka kufikia Kinyasini.

Lakini pamoja na uzuri huo kuna mambo ambayo yanahitaji kusaidiwa wananchi wangu hasa wale ambao wamevunjiwa mpaka hivi leo hawajapata fedha zao. Lakini ukifuatilia unaambiwa bado Wizara ya Fedha haijawatilia pesa. Kwa bahati nzuri Dk. Mwinyihaji Makame yupo ananisikia kilio hichi, ninavyomjua mimi ni mtu ambaye msikivu na mtekelezaji wa mara moja. Kwa hivyo, nina imani kesho huenda akawatilia cheki hiyo na kuweza kutusaidia. Dk. Mwinyihaji tuokoe.

Nikiendelea katika barabara zile za ndani kwa kweli nishukuru sana na hasa pongezi zaidi ziende kwa Mkurugenzi pamoja na mtendaji wake, kuna kijana ambaye ni mzuri sana na tungemuombea tu wizara imtazame kwa kumpa taaluma zaidi. Kwa sababu leo watu wengi walisifu jinsi ambavyo barabara zile za Kinazini pale hapana mtaalam kutoka nje, ni kijana wetu hapa hapa akiwa msimamizi wake Mkurugenzi. Huyu mtoto nae Mhe. Waziri muongezeeni taaluma zaidi kutokana na hizi kazi nzuri anazofanya.

Mhe. Mwenyekiti, kuna daraja lile la ndani katika hizi barabara zetu za ndani kwenye majimbo ya Kitope na Kinduni limeshafanya gharama kubwa ambazo si chini ya milioni 9 walizotupa Mfuko wa Barabara. Lakini kwa kweli kwa mvua hizi kama hatukuwahi basi ile barabara zile fedha zote zitapotea kabisa tutakuwa tunaanza kwa alif kwa ujiti. Hiyo si vizuri kusema ukweli na hali ambayo sasa hivi inachimbika.

Mhe. Mwenyekiti, *akal minal kalil* ningemuomba Mkurugenzi atusaidie japo gari nne ili kuokoa hapa mwanzo, ukiingia tu pale Kinduni kwenda kupata hilo daraja hali iko mbaya sana.

Lakini pamoja na hayo, najua Mkurugenzi msikivu kesho atanipelekea kifusi. Namshukuru sana kutokana na hilo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mwenzangu Mhe. Ali Abdalla Ali alizungumzia mambo ya leseni lakini mimi sitozungumzia leseni zaidi. Kuna hatari sasa hivi wakati wowote inaweza ikatutokezea na *inshaallah* Mwenyezi Mungu aiepushe. Kuna haya magari yanayobeba makontena yanakwenda mbio na wakati mbaya. Tungejaribu kutafuta utaratibu kama wenzetu kule Bara magari kama yale yanaanzia usiku. Lakini hata hivyo, kule Bara wanapenya maana yake juzi kuna gari moja kubwa limeua vibaya vibaya, limeangukia gari dogo limefinya watu, ukiambiwa binadamu walikuwemo humu huwezi kuamini.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja niliingia kwenye msingi bila ya kutaka kwa ajili ya kuokoa maisha yangu. Alipita jamaa anaelekea Mwanakwerekwe na gari lile refu na kontena kapakia nyuma kwa mwendo wa kasi. Kwa kweli ni hatari kubwa sana tuwahi mapema kabla ajali kutufikia.

Mhe. Mwenyekiti, halafu ukija katika hizi barabara zetu za Kaskazini, madaraja yale yanaua, makaburi kusema ukweli, kama hatukutafuta utaratibu mzuri basi yataendelea kuua. Mimi napendekeza kuwa tungeweka matuta, kwa nini tunaona tabu kuweka matuta. Wenzetu kule Bara katika madaraja karibu ya kufikia daraja wanaweka tuta linawasaidia sana. Lakini sisi hapa utaambiwa kuna usalama wa viongozi, kule ndio hatari zaidi kwa viongozi kuliko hapa.

Hili ningeliomba tuwahi mapema kwa sababu kila leo, hebu katazame zile *fence* za yale madaraja, ukiambiwa palikuwa na *concrete* huwezi kuamini, ukiambiwa kulikuwa na vyuma vikubwa basi huwezi kuamini. Kila leo ajali ukikosa asubuhi basi jioni. Namuomba Mhe. Waziri aliangalie suala hili kwa upeo kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutangaza rasmi kuwa makampuni yaje hapa ili kuwaokoa zaidi wananchi wetu na umaskini kwa kuwapatia ajira. Lakini hili suala kwa taarifa fupi nimsifu Mhe. Waziri Kiongozi amelifanyia kazi hapa na pale na jitihada nzuri imeonesha neema yake.

Kuna hii Kampuni ya Mabaharia hapo *DONOUS*, hii baada ya mwenyewe Waziri Kiongozi kuichukulia nguvu basin a wizara ilikuwa ijiingize kichwa na miguu kwa ujumla, halafu baadae ndio Waziri Kiongozi mwenyewe amalize kazi. Lakini utakuta Waziri Kiongozi kaifanya kazi sasa huku bado tunaiacha. Hii kwa kweli imetusaidia, hivi sasa kwa haraka vijana wetu wa Zanzibar si chini ya mia nne na wapo kwenye maji wanaleta neema *PBZ*, kila mwezi wanalipa dola 1,500. Sasa hii raha.

Lakini kuna mambo mengine inabidi lazima serikali isaidie. Leo tunatumia Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam, sasa hivi kuna *member* elfu moja wamo katika orodha wanaotaka kwenda Dar es Salaam kusoma. Sasa tutazame sheria zetu, pamoja na kuwa hatumo kwenye member ya *IMO* lakini ziko taratibu zinaweza zikatusaidia.

Tukisema kuwa cheti chetu kitakuwa hakikubaliki kwa mujibu wa sheria ya dunia sawa. Lakini je, tukisema tuwachukue walimu tukawaleta hapa ili wakaweza kuwafanyia *training* vijana wetu, halafu baada ya mitihani kufanya wao wakatufanyia hao hao wa Bara, lakini tukapunguza *cost*. Kwa sababu kama kule ikiwa ni laki mbili mpaka laki tatu, basi wao tungewauliza nyinyi walimu watatu tukulipeni kiasi gani kwa kuja hapa, ili tukapunguza ile *cost* ambayo hawa wananchi wetu wengine ni maskini za Mungu hawana jamaa kule.

Kwa kweli hii kampuni ni nzuri na ni ya uhakika kabisa, tena inajitangazia sifa nzuri tu Zanzibar kwa sababu tunajulikana *world* iko Zanzibar. Sasa mimi ningeiomba serikali hili suala tulipe nguvu kabisa. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri yupo ananisikiliza na hili suala tulichukulie, pamoja na kuwa uwezo wa kusajili kampuni ile ya chuo upo hapa, lakini cheti chako kitaishia Chumbe. Sasa sisi hatutaki kiishie

Chumbe, tunataka kivuke maji kabisa na huko watu watutambue. Kwa hivyo, naiomba serikali iweze kutusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, nakaribia mwisho naingia katika Mamlaka ya Maji. Mhe. Mwenyekiti, niwasifu ndugu zangu hawa wa Mamlaka ya Maji kutokana na jitihada zao nzuri sana na hasa wakati ule wa tabu ya umeme. Kwa kweli wakurugenzi hawa wawili wa Fedha na Mkurugenzi Mkuu wamefanya kazi vizuri sana. Walikuwa wao hawana usingizi saa zote wanafanya kazi kwa kusikiliza wananchi wapi jenereta limeharibika. Sisi viongozi ni mashahidi tulikuwa tukifuatilia kwenye majimbo yetu wapi jenereta halifiki na ukisema tu tatizo gani pale pale wanalitatua.

Halafu la pili niwashukuru sana wamedhibiti hata huu mgao wa mafuta, hakukuwa na mgao wa kubabaisha. Ukiambiwa kituo chako lita mia, basi hakikisha lita mia zinafika pale na anahakikisha kuwa zimefanya kazi kwa mujibu wa siku ulizowekewa pale. Hili mimi nawasifu sana na Mwenyezi Mungu ndie atakayewapa fungu. Kwa sababu unaambiwa katika pepo ni moja katika maji. Hili ni suala kubwa sana, binadamu yeyote utakapochimba kisima basi ujue *Alhamdulillahi* Mwenyezi Mungu atakupunguzia. Sasa hili nalo niwashukuru wamejitahidi kiasi kikubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawasifu tuko katika hatua nzuri. Nawapa mori kuwa waendelee tumaliziwe haraka sana majimbo yetu matatu haya ili tupate kunufaika haya maji kwa kutumia pamoja na kulimia. Tunaomba hili suala liharakishwe zaidi kwa hapa walipofika. Wananchi wa Kitope wamenipa salamu rasmi nikupongezeni na jitihada ziendelee.

Mhe. Mwenyekiti, nikiingia kwenye suala la umeme namshukuru sana Kaimu Meneja na mimi ningeomba wizara imfikirie impe moja kwa moja Umeneja. Kwa sababu kama ni kutazamwa ameshafikia *level* nzuri. Kwa kweli alikuwa anatupa taarifa nzuri kama mtangazaji wa mpira kutokana na matatizo ya umeme na amefikia pahala pazuri sana.

Halafu isitoshe ametupa ile *offer* ya kuwa wanakijiji tunao uwezo wa kukopa umeme kwa kuuingiza kwenye majumba yetu. Sijui kama inaendelea ile, kama inaendelea basi tunaomba iendelee ili wananchi wanufaike kwa mkopo na kuweza kuumiliki umeme kuutia kwenye majumba yao.

Halafu kuna mradi mwengine niliwahi kufuatilia alinambia tu mwenyewe Kaimu Meneja suala la kuwa sisi wawakilishi tujitahidi na nguzo tuwapelekee wananchi, yeye atajitahidi atatusaidia masuala ya waya na mambo mengine. Sasa na hili kama bado lipo tunamuomba aendelee na imani yake atusaidie na tutamwendea.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano kijiji cha Matetema Waziri mwenyewe aliahidi kuwa atapeleka umeme lakini mpaka leo naona kimya na wakati ndio huu *pressure* inapanda, *pressure* inashuka, kwa hivyo, tusaidiwe haraka. Mhe. Mwenyekiti, sitokuwa na zaidi nakushukuru sana, ahsante.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii, mimi naweza kuwa na mchango mdogo sana. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mhe. Mwenyekiti kwa namna ambavyo amesoma ripoti yake kwa utulivu na ufasaha sana. Jambo ambalo naomba nilizungumze katika ripoti yake ni suala la utengenezaji wa magari katika karakana kuu.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC* ya Baraza lako tukufu, mara nyingi suala hili Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali analizungumza na hapendelei magari kutengenezwa katika karakana za binafsi. Ningemuomba Mhe. Waziri aiimarishe karakana kuu ili iweze kuchukua *load* kubwa ya vipando vya serikali.

Najua mafundi wapo lakini zana zimepungua kidogo. Lakini kuwepo mafundi haitoshi, mafundi lazima kila muda wapewe *refresher course* kwa sababu *design* za magari kila baada ya muda zinabadilika. Kwa hivyo, ukimuacha fundi ambaye ni kweli labda ana *degree* ya kwanza lakini kila baada ya muda magari yanabadilika *design*, kama hapati *refresher course* basi kwa kweli atakuwa hana uwezo mzuri wa kutengeneza gari ambazo zimekuja labda baada ya miaka mitatu mbele. Kwa hivyo, ushauri wangu ni

kwamba ajitahidi kui-*equip* karakana na zana za kutosha, lakini pia mafundi kila baada ya muda wapate mafunzo ambayo yatawasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, jengine tuna tatizo kidogo na *Zantel*, ile habari kwamba imehama inaonekana imehama kweli. Sasa hili Waziri labda atwambie amehamisha, ameshindwa nguvu au imekuwaje. Kwa kweli pale mambo yote sasa yanakuwa kwa ndugu zetu Bara sasa haipendezi. Tulisema Makao Makuu ya *Zantel* ni Unguja lazima ibakie Unguja, kusiwe na mambo mengine ya kijanja janja yanayofanya *Zantel* ibakie Bara.

Mhe. Mwenyekiti, imefika pahala kwamba hata *voucher* ya mambo madogo ya kufanywa hapa Zanzibar yote lazima yakasainiwe Bara. Sasa Mhe. Mwenyekiti, Makao Makuu ya taasisi hayaendi hivyo, lazima kuwe na *administration* ambayo masuala yale ya Bara yangelikuja huku, sio ya kwetu sisi yaende Bara ambako kwa kweli hili jambo halipendezi.

Mhe. Mwenyekiti, baya zaidi ambalo naliona huwa wanatoa *offer* kama walivyosema wenzangu, lakini sisi katika *Zantel* ni *shareholder* yaani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini ilipaswa hapa wananchi wa Zanzibar wapate *offer* ambazo ni nafuu zaidi kuliko watu ambao sio *shareholders*.

Mhe. Mwenyekiti, natoa mfano ile *offer* ya mkesha, Wazanzibari wanatoleshwa shilingi mia tano kuanzia saa nne na nusu za usiku hadi saa mbili asubuhi. Ukiwa Bara unatoa mia mbili kuanzia saa nne na nusu asubuhi mpaka saa nne za asubuhi siku ya pili. Sasa sisi punda wetu tumepandishwa mkiani. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi na Waziri wa Fedha lazima waangalie kwamba Wazanzibari wana chao katika kampuni ile na kwa vyovyote vile wao lazima wafaidike zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo nimpongeze Kaimu Meneja wa Shirika la Umeme anafanya kazi nzuri pamoja na matatizo makubwa aliyonayo na kwa kweli anapaswa kupewa *moral support*. Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema mwenzangu kwamba wakati umefika sasa Ukaimu ufike kikomo, mimi jambo hili huwa silipendi hata kidogo. Mtu uende na Ukaimu miaka na miaka, hata kanuni za utumishi zinapinga hivi, lakini sijui kwa nini tunaendelea nalo. Nafikiri Idara ya Utumishi Serikali itusaidie kuhusu suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo lililotokea tunapaswa tujifunze. Kwa hivyo, katika bajeti ijayo tunapaswa kuletewa katika Baraza hili mipango madhubuti ya mkakati wa serikali ili kuwa na umeme mbadala kama hatua itafikia vizuri. Kwa sababu umeme huu wa Tanga na Dar es Salaam hatuwezi kuutegemea moja kwa moja. Kwa hivyo, naomba kujua hasa umeme wa Tanga/Pemba utaanza lini kwa sababu *date* zimekuwa nyingi, mara sijui mwisho wa mwezi wa Oktoba, Disemba, Machi. Naona Mhe. Tafana Kassim Mzee juzi alinambia sijui April, April yenyewe ndio hii. Mhe. Mwenyekiti, wanapaswa Wazanzibari waambiwe ni lini.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo naomba sana nimpongeze Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi ni utiaji wa saini wa barabara ya Wete/Gando, Wete/Konde umeanza. Lakini katika hili wananchi wananiuliza maswali mengi na nashindwa kujibu. Yeye mwenyewe Waziri amesema kwamba barabara hizi za Wete/Konde, Wete/Gando zinakwenda pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ana bahati nzuri tena, Mhe. Rais katika Sherehe za Mapinduzi akawatangazia wananchi wa Zanzibar kwa jumla kama barabara hizi mbili zinajengwa pamoja. Sasa bahati mbaya ya Wete/Konde imeshafika nusu ya Wete/Gando haijaanza. Kwa hivyo, napata maswali mengi, naambiwa vipi hii *parallelism* ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi mpaka ifike mwisho ndio ije ianze hii au vipi, inakuwaje hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba wanisaidie jibu ili nitakaporudi jimboni kesho kutwa niwe nina jibu la kuwaambia wananchi kwamba *parallelism* hii inakusudiwa labda katika hali hii na hii ambayo naweza na mimi kutoa jibu. Vyenginevyo basi naomba ianze. Baya zaidi hichi ni kipindi cha mvua Mhe. Waziri anajua tumekubaliana mimi na yeye angalau barabara ifukiwe katika hatua hii ya mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi na mbunge tukifanya enzi za nyuma ambapo *contractor* hajapewa, lakini mwaka huu *contractor* ameshapewa Waziri ametuzuia anatwambia msifanye. Sasa kama ni hivyo ni vizuri kwamba mvua hizi za masika zinazoendelea isije ikafika hali ikawa wananchi wa Gando wanapata

matatizo ya kuja mjini. Kwa hivyo, tunamuomba afanye kadri inavyowezekana ndani ya wiki hii inayoanza kesho kutwa baada ya sherehe za Pasaka basi angalau ifanyiwe *grading* na ijazwe jazwe, ili wananchi waweze kuja mjini bila ya matatizo na mazao yao.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki nichukue muda wako hata kidogo nakushukuru sana.

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia mswada huu. Nitazungumza kwa ufupi tu kwa sababu na mimi nilikuwa ni mjumbe mmoja wapo katika Kamati hii ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla ya yote nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa jinsi alivyosimamia pamoja na Makamo wake kutuongoza na kupata mambo mengi tu katika ziara tulizotembelea wizara zote hizi tulizokuwa tumepangiwa. Mhe. Mwenyekiti, pili nawapongeza watendaji wa wizara zote mbili kwa jinsi walivyotupokea na kutupa huduma mbali mbali tunapofika katika mawizara yao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakuja kuchangia masuala kama hili la maji, ujenzi, nishati na ardhi, nitaanzia suala la maji. Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza sana Mamlaka ya Maji kwa kuanzishwa na juhudi kubwa waliyokuwa wanaichukua ya usambazaji wa mabomba ya maji katika maeneo yetu yote ya Wilaya ya Mjini mpaka vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, hii kwa kweli imeleta matumaini makubwa sana, isipokuwa tatizo tu kuna baadhi ya maeneo kama walivyosema wajumbe wenzangu maji yanakuwa hayafiki. Kuna baadhi ya siku yanafika utashangaa, yaani maji yanafunguliwa mabomba yale ya zamani yanakuja na udongo, yanakuja na mchwa, watu wanashangaa maji haya yanatoka wapi. Kuna baadhi ya siku yanafunguliwa kama muda wa masaa 24 sasa hili linatushangaza sana. Kwa hivyo, niiombe mamlaka hii iwaangalie zaidi watendaji wao, wale ambao wanawajibika wawajibike, waliokuwa hawafai kuwajibika wawajibishwe.

Mhe. Mwenyekiti, jengine naipongeza sana Idara ya Nishati kwa juhudi inayochukua pamoja na watendaji wake kwa kuanzisha majiko ya gesi. Hii itasaidia sana kupunguza ukataji wa miti kiholela na kuharibu mazingira. Kwa hivyo, hili Mkurugenzi anayehusika na nishati nitamuomba aeleze zaidi majiko yake haya na atoe taaluma zaidi kwa wananchi ili kupunguza uharibifu wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, la pili nampongeza kwa juhudi aliyochukua ya kutafuta wataalam na vijana mbali mbali kupeleka nje kwenda kusoma mambo ya nishati, ili pindipo tukija kuanza masuala yetu ya nishati ya uchimbaji wa gesi na mafuta basi tunakuwa tumeshajiandaa kabisa. Kwa hivyo, hili nampongeza sana waziri.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la umeme. Shirika la Umeme kwa kweli nawapongeza kwa juhudi na ustaamilivu mkubwa waliochukua wakati tulipokuwa tumekosa umeme. Wafanyakazi wale wamestahamili zaidi ya miezi mitatu, hawakukereka, hawakuandamana, wamestahamili mpaka tumerejeshewa umeme na wao bado mpaka leo wako kazini na wanajumuika na kazi zao. Kwa hivyo, kwa hili nawapongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, isipokuwa tu katika umeme kuna mambo kidogo niliomba Mhe. Mwenyekiti, yafanyiwe ukarabati kama itawezekana. Suala hili la kulipa umeme kwa risiki ambayo inakuwa na mambo mengi. Utakuta kuna *VAT*, *label charge*, *domestic*, sijui *democracy* yaani mambo chungu nzima tu *(Makofi).*

Kwa hivyo, hili linababaisha mteja. Leo unakwenda dukani kununua shati imekatwa kodi ya forodha lakini huambiwi, unapewa bei yake tu unanunua basi. Lakini hapa leo kuna nyanja nyingi. Kwa hivyo, utakuta mteja anakwamba na anababaika. Mhe. Mwenyekiti, kama kuna mbinu ya kufanya utafiti angalau kuyapunguza yakawepo mawili tu, basi ifanywe. Iwe bei ya *unit* na *VAT* basi, lakini hayo mengine ya *democracy* ya nini. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningeomba hapo upaangalie sana ili kuondosha usumbufu mdogo mdogo unaowakabili wateja wako.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ujenzi na ardhi. Idara hizi nazipongeza kwa juhudi kubwa wanazochukua kuwapimia viwanja watu mbali mbali, ili watu wajenge nyumba za kileo na kuepukana na nyumba za

kizamani. Isipokuwa kubwa ninalowaomba kwa baadhi ya maeneo ambayo wanataka kujenga nyumba wakipata wafadhili, basi wawepe fikra na mawazo zaidi ya kujenga nyumba za kileo za kwenda na juu, ili waondoshe zile nyumba za mtandao kama treni. Kwa hivyo, aina zile za nyumba tuzipunguze ili tupate maeneo mengi zaidi ya ardhi kwa manufaa ya masuala mengine. Leo tukisema tunawaruhusu watu au wafadhili kuja kujenga nyumba za chini tu, basi maeneo yetu tuliyokuwa nayo madogo na matokeo yake yatapungua haraka na wananchi wetu watakosa baadhi ya mambo mbali mbali ambayo yanategemewa katika ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwa hapa nitaanzia katika mawasiliano ya simu. Juhudi kubwa imechukuliwa na shirika hili kwa kuendeza simu mbali mbali za mikononi ambapo sasa hivi tumefaidika na watu wengi katika kipindi cha nyuma mtu akiwa na simu ya mkononi basi mtu anashangaa, lakini leo *Alhamdulillah* mtu hashangai anaona ni jambo la kawaida tu.

Kwa hivyo, nawapongeza sana kwa juhudi kubwa walizochukua. Tatizo moja ni kwamba minara imekuwa mingi mijini, kwa hivyo waangalie kama kuna uwezekano watafute maeneo.
Mhe. Mwenyekiti, tuna maeneo mengi tu yaliyoinuka ya uwanda kama inawezekana hivyo, basi wafanye hivyo. Lakini kwa wingi wa minara iliyokuwepo mijini sasa hivi kwa kweli inatisha, ingawa haileti madhara ya mionzi, lakini vile ukiupita tu hivi basi unaanza kuona kizunguzungu.

Basi ningemuomba Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi akaliangalia hili kama kuna ukarabati huo wakafanya katika maeneo hayo yaliyokuwa ya wazi ya uwanda.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie katika suala la UUB. Hawa watu wa njia nawapongeza kwa kazi zao kubwa wanazozifanya za barabara, wanajitahidi kwa kweli. Kuna suala moja ambalo nitaomba lichunguzwe na lifanyiwe kazi sana. Katika sehemu nyingi *round about* utakuta kunachimbika haraka sana na kunakuwa na mashimo. Ukija katika *round about* hii ya Malindi, ya Amani na ya Kwerekwe. Utakuta njia ni safi, lakini ukifika pale kuna mashimo, kwa hivyo sijui kuna upungufu gani, sijui kama ndio hiyo lami ni hafifu au sijui kuna utaalamu gani ambao unahitajika pale. Kwa hivyo, katika utengenezaji wa sehemu kama zile ningeomba waangalie sana na ziwe madhubuti zaidi. Barabara utakuta ni nzima lakini ukifika sehemu zile utakuta zimeharibika. Kwa hivyo, ningewaomba wajitahidi sana.

Vile vile nawapongeza katika juhudi kubwa wanazofanya kwenye ujenzi wa barabara katika majimbo na maeneo mbali mbali. Ingawa kwangu bado, lakini natumaini Mhe. Waziri na mimi atanitizana na kunifikiria kwenye barabara ya viwanja vingi kuendea Kwaboko na barabara ya kutoka Amani Fresh kuendea Mboriborini na Kilimahewa imepangwa *rote*, lakini sasa hivi rote wanakatiza za gari kwa sababu haipitiki. Kwa hivyo, ukosefu wa kujenga kiwango cha lami basi angalau kifusi kizito, ili kwenye barabara zile na wananchi wanaokaa mule wapate kuzitumia. Kwa hivyo, nafikiri Mhe. Waziri ujumbe huu umefika na mimi utanitifikiria.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu bandari. Bandari nawapongeza sana kwa kazi waliyoifanya. Hii ziara ya kutembelea mashirika ni nzuri sana. Kwa sababu mwanzo nilivyokuwa nikifikia kabla ya kutembelea sivyo na ilivyo. Kwa kweli wamejitahidi sana bandari, tokea kumalizika bandari yetu basi baadhi ya makontena mengi yanashusha mizigo yao hapa Zanzibar. Meli nyingi zinafuraha kuja kushusha mizigo Zanzibar kulingana na zana tulizokuwanazo na utendaji wao mzuri wa wafanyakazi wa bandari. Kwa hivyo, suala hili nawapongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nije kwenye Mamlaka ya Anga. Mamlaka hii inastahili sifa, kwanza kwa juhudi yote waliyochukua ya kujenga *canopy* pale imesaidia. Pili kutengeza njia mpya ya kurukia na kutulia ndege ambapo imeleta matumaini mazuri ya uwanja wetu na kuweza kujulikana kimataifa. Kwa hivyo, kwa suala hilo nawapongeza.

Isipokuwa katika marubani wa ndege zile ndogo ndogo wawe wanaangalia sana afya zao, ili wasije wakaathirika. Kwa sababu kuna wengine utawakuta wanarusha ndege ina matatizo, lakini wameshayaona basi wanajiamini kwa ule ujuzi wao waliokuwanao basi anaona mimi nitawahi, halafu sio muda mrefu utasikia ameshatua Kiwengwa. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri hawa marubani wakawa wanaangaliwa zaidi afya zao, isijekuwa mambo ya bia au sigara zinawachanganya na kuweza kutokea

matatizo kama hayo au kama yale yaliyotokea huko nyuma. Ndenge imeondoka na kufika angani imefunguka mlango. Nyengine kama hiyo iliyosikika juzi kuwa ndege kwa ghafla tu imetua Kiwengwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia na kujali muda niende kwenye usafiri wa meli. Nayapongeza makampuni mbali mbali binafsi kwa jinsi walivyojitokeza ili kusaidia mambo ya usafiri. Leo kama ingekuwa hatuna makampuni binafsi sijui tungesema nini kwa wananchi wetu. Meli zetu ambazo tulikuwa tunazitegemea zimeshalala tungekwenda wapi? Kwa hivyo, mamlaka hii ya meli pamoja na mkurugenzi wake nawapongeza kwa kuwapa uhuru makampuni mbali mbali ili kuleta meli na kuweza kusaidia.

Kwa hivyo, kubwa ninaloomba ni mkaguzi wa meli awe makini kuzikagua, ili yasijekutokea matatizo kama haya yaliyokuwa yanatokezea. Vile vile ningeomba hili himizo la kutafuta meli zetu basi lifanywe haraka. Uwa sehemu nyengine lakini ufanikiwa hapa ili tupate kufanikisha.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa muda ulionipa, ninaishia hapa na ninaziunga mkono ripoti za kamati hii.

Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa hizo dakika tano. Kwa haraka haraka nataka nizungumzie kwanza Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuishukuru sana Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuzianza zile barabara sita za Kusini kuwa ndio za mwanzo katika barabara zilizomo katika jimbo langu. Barabara ya Mtambile Mwambe ambayo keshaizungumzia Mhe. Hija, sina haja ya kuyarudia naunga mkono yote yale ambayo ameyazungumza Mhe. Hija.

Halafu barabara ya pili ni barabara ya Mtambile Kangani, nayo hii imeanza matengenezo yake, lakini matengenezo haya Mhe. Mwenyekiti, yameleta balaa kwa watu wa Kangani baada ya mvua kuanza kunyesha. Kwa hivyo, nachukua nafasi hii kumuomba Mhe. Waziri, achukuwe juhudi na hatua maalum kwa ajili ya kuokoa hiyo hali kwa kipindi hiki cha mvua mpaka baada ya mvua za masika zitakapomalizika aendelee na shughuli yake ya matengenezo. Kwa sababu hivi sasa hata gari la ng'ombe halipiti, sikwambii kwenda kwa miguu. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri achukuwe hatua za dharura ili aweze kuihami hiyo hali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo, kwenye Wizara hii hii ya Mawasiliano na Uchukuzi, mara nyingi Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili linazungumzia wizara kujitayarisha na kununua vyombo pamoja na vifaa vya uokozi baharini. Kwa sababu mara nyingi sasa hivi ajali zinatokea na wala hakuna vyombo vya uokozi. Kwa hivyo, maisha ya wananchi wetu wanaosafiri kwa kutumia bahari yanahatarishwa sana. Namuomba sana Mhe. Waziri suala hili alitilie sana maanani kwa ajili ya kuwaokoa wananchi wetu wanaosafiri kwa kutumia bahari.

Baada ya hapo nakwenda kwenye Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Mhe. Mwenyekiti, hapa kwenye ripoti hii imezungumzia kuwa katika usambazaji wa umeme Pemba wamefikia asilimia 80, kuna asilimia 20 tu ndio bado hazijapata umeme kisiwani Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa asilimia hizo 20 ni vijiji vya Jaani, Mitundafumoni na Kivumoni. Halikadhalika na vijiji vya Kigongoni na Gae la Mtungi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, linalonisikitisha ni kwamba kuna baadhi ya watendaji katika Shirika hili la Umeme, sijui niseme nini? Kwa sababu wananchi wa vijiji hivi wamepeleka barua zao kwa meneja wa tawi la Shirika la Umeme Pemba, kwa ajili ya kwenda kuwapimia na kuwafanyia tathmini kwa ajili ya kuweza kufikisha umeme katika vijiji vyao. Sasa hivi imepita miaka mitano hakuna hatua iliyochukuliwa. Suala hili niliwahi kumueleza Mhe. Naibu Waziri hasa kwa vijiji hivi vya Kigongoni pamoja na Gae la Mtungi.

Mhe. Mwenyekiti, aliwahi kukabidhiwa mfanyakazi wake mmoja na meneja wa tawi, lakini huyu jamaa hata mimi nashindwa kumuelewa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa wizara hii inayohusika awasimamie hao watu wake, ili waende kufanya tathmini ya kupeleka umeme kule na wananchi waliojikusanya kwa ajili ya kulisaidia shirika waweze na wao kutia nguvu zao baada ya kupata ile tathmini yenyewe. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Ahsante.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi japokuwa kwa muda finyu kabisa na nitajitahidi kuyapunguza mengi ambayo nimekusudia kuyasema.

Mhe. Mwenyekiti, nianze moja kwa moja na Shirika la Meli. Mwenzangu aliyekaa kitako amemalizia, lakini mimi nilikuwa nataka kupunguza kipengele na nizungumzie hili suala zima la utaratibu wa usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, mengi yameshasemwa hasa kuhusu suala la uuzaji wa tiketi. Mimi nataka kuweka msisitizo wa umuhimu wa vikao baina ya kamati, inawezekana sio kamati iliopo sasa hivi tu lakini na zile zitakazokuja pamoja na wamiliki wa vyombo ni suala muhimu, kwa sababu kuna mikakati mingi ambayo wizara pamoja na kamati kwa kushirikiana tumekusudia itekeleze sasa. Vikao vitaweza kuonesha pahali gani pana matatizo na wapi parekebishwe vipi kwa ajili ya kuweka suala zima la usafiri wa baharini kuwa katika hali nzuri na ya kisasa kwa ajili ya kuokoa maisha ya watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze sana mrajis wa Shirika la Meli kwa shughuli zake anazozifanya na niseme kwamba masuala ambayo tulishauri kama kamati, basi yafanyiwe kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye upande wa Mamlaka ya Maji. Mamlaka hii nataka niwapongeze sana kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya na shughuli zinaonekana. Kama ujenzi wa matangi na shughuli nyengine mbali mbali ambazo zinafanyika. Kwa hapa nilikuwa nina ushauri kuwa hali halisi ya upatikanaji wa maji bado ni tatizo na mimi nilidhani labda ni kwa maeneo yetu tu ya mjini, lakini Mhe. Salmin Awadh amesema sana kuhusu eneo la Sogea, lakini hata *swahib* yangu hapa Maalim Mohamed Ali Salim na yeye amesema huko Wambaa kuna tatizo kubwa. Sasa hapa nilikuwa naomba sana kwamba mimi nilifikiri tu kuwa inawezekana ule uungaji wa mashine, watu wengi wameunga mashine za kuvutia maji, nikafikiri labda ndio tatizo kubwa linalosababisha maeneo hasa ya mjini tusipate maji. Lakini kwa sababu hili tatizo limeenea mpaka maeneo mengine ya Pemba na sehemu za ng'ambo, basi nadhani mamlaka inatakiwa ifanye kazi ya ziada ya kufanya utafiti na kujua zaidi ni nini tatizo la maji. Kwa sababu kwa upande wa Wilaya ya Mjini tayari kazi kwa sehemu kubwa ya mradi ule wa Japan umeshafanyika na sasa hivi iko kwa upande wa Magharibi na bado maeneo ya mjini tuna matatizo makubwa ya maji.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tulikuwa kwenye ziara hiyo na wenyewe wameshuhudia maeneo sugu kabisa kama Michenzani na maeneo mengine ambayo tulipitia.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa suala zima la Idara ya Upimaji wa Mipango Miji. Kwa mujibu wa ripoti ni kwamba kuna viwanja karibu 2000 au zaidi vinapimwa. Sasa mimi nilikuwa nina ushauri tu kuwa nadhani tubadilishe utaratibu. Kuna Mhe. Mjumbe mwenzangu hapa alizungumza suala zima la eneo jipya linalopimwa lakini kukawa kuna nyumba kila mtu kajenga kivyake, huyu kajenga kaelekea huku na huyu kaelekea kule. Kwanza haileti sura nzuri kimandhari.

Vile vile kwa upande mzima wa kupeleka miundombinu inakuwa ni matatizo. Tunaiona miji ambayo imejengwa kiholela inavyokua. Sasa hapa ushauri wangu ni kwamba aidha kuwe na maelekezo maalum kuwa eneo fulani lililopimwa ujenzi unaohitajika uwe ni wa aina fulani. Au kujengwe nyumba na watu badala ya kuwa wanaomba kwa ajili ya kupatiwa viwanja, basi wawe wanapeleka maombi yao kwa ajili ya nyumba. Hii itaondosha matatizo kadhaa yakiwemo ya migogoro.

Katika ripoti yetu au katika shughuli zetu za kamati Mhe. Mwenyekiti, tulivyofanya tumeshuhudia migogoro sugu hasa kisiwani Pemba kwa sababu ndio tulipata nafasi nzuri ya kutembelea. Kwa hapa Unguja tulikuwa twende Matemwe, lakini safari ikawa imehairika. Sasa kule tulikuwa tulikuta migogoro baina ya JKU na wananchi kwa Makangale. Pia tulikuta mgogoro wa Chake Chake pale Wawi wanaita ndugu kitu na Valantia. Katika mfumo wetu ambao tunao sasa hivi, hii migogoro kidogo inashida kutatulika, lakini tukienda katika utaratibu wa kisasa, nadhani itakuwa migogoro kama hii itaweza kupungua sana Mhe. Mwenyekiti.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikazie tu nati pale ambapo wenzangu walipopita kuhusiana na suala zima la Kaimu Meneja wa Shirika la Umeme. Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba kijana huyu anafanyakazi nzuri na miongoni mwa kazi moja ambayo ni ya kupigiwa mfano aliyoifanya na utendaji wake ulipelekea Serikali ya Mapinduzi kusamehewa deni kubwa la fedha ambazo zilikuwa zinadaiwa na

watu wa ORYX, kutokana na yale mafuta ya IDO yaliyokuwa yanasafirishwa kupelekwa kule. Kwa hivyo, ule utendaji wake ulipelekea deni lile likafutika lote na mambo yanakwenda vizuri mpaka juzi tulipowapitia. Kwa hivyo, tungeomba sana wizara na wanaohusika kwamba tungependa huu ukaimu umalizike na badala yake awe meneja kamili.

Mhe. Mwenyekiti, nina michango mingi sana, lakini kwa kuheshimu muda nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa maelezo ya wizara yangu juu ya ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Mwenyekiti, wachangiaji walikuwa ni wengi na kufikia 11. Walitaka maelezo marefu lakini muda hauruhusu kutoa maelezo mengi. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, pengine utatuvumilia sijui kama tutamaliza na Mhe. Tafana Kassim, lakini tutajitahidi sana kutoa majibu yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya huo muda nitaomba niseme tu kwamba wizara yetu imechangiwa na wajumbe 11 wafuatao. Halafu baadae nitakuwa ninajibu pengine kwa mpangilio au si kwa mpangilio.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu
Mhe. Ali Suleiman Ali
Mhe. Salmin Awadh Salmin
Mhe. Haji Mkema Haji
Mhe. Hija Hassan Hija
Mhe. Ali Abdalalla Ali
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
Mhe. Said Ali Mbarouk
Mhe. Ali Denge Makame
Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin
Mhe. Zakiya Omar Juma

Mhe. Mwenyekiti, alianza kuzungumzia na Idara ya UUB, lakini pia alichanganya na ujenzi wa barabara nyingi tu. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki ambacho kimezungumzia ripoti, pengine kutokana na muda kuna baadhi ya mambo ya wizara yetu yanaonekana kama yameandikwa kuwa yameshapitwa na wakati. Kwa sababu kama kitabu hiki kinavyosema barabara ya Mazizini Fumba ujenzi wake unaendelea na barabara ya Mshelishelini Pwani Mchangani ujenzi wake unaendelea. Mhe. Mwenyekiti, barabara hizi tayari zimekwisha na zimeshafunguliwa katika sherehe za Mapinduzi na ziko katika hali nzuri.

Pia barabara ya Amani Dunga inaendelea vizuri na tunatarajia mwezi wa huu wa Aprili tutaanza na barabara ya Mfenesini Bumbwini. Vile vile tunayo lami ya kutosha ambayo imenunuliwa na fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia mfuko wa barabara. Kwa hviyo, tunayo lami na sasa hivi hatuna tatizo la lami.

Mhe. Mwenyekiti, barabara za Kusini Pemba zimezungumziwa na wajumbe wengi, zimeanza lakini kitu chochote kinapoanza kina matatizo yake na yale masharti ya misaada wenyewe yalikuwa kidogo magumu, lakini kwa sababu vifaa vyengine ilikuwa tupate vipya na vyengine vile vyetu sisi vya idara ama vitengenezwe vitumike katika ule mradi ili baadae tuvitumie sisi kwa shughuli zetu nyengine baada ya mradi kumalizika.

Mhe. Mwenyekiti, mwanzo tulikuwa tuna tatizo la kuchelewa kwa baadhi ya vifaa na sisi kama wizara hatukutaka kuingilia taratibu za ununuzi, maana ukiingilia taratibu za ununuzi unaweza ukaleta madhara baadae. Nafurahi kwamba vifaa vimeshafika na vyengine viko bandarini Pemba, tunatarajia kufufua *bulldozer* jengine na kazi zitaendelea kama zilivyopangwa. Kuhusu vile vyuma. Tunakwenda sana Pemba na tumeona lile kuwa linatatizo kweli, tukawauliza kuwa hawawezi kutumia mbao, wakasema inawezekana na sasa hivi mbao zimepatikana kutoka huko huko Pemba. Tunatarajia kazi itabadilika na itakwenda kwa kasi zaidi, ili tuweze kufikia lengo tulilokusudia.

Halafu kuhusu Idara ya Leseni kupatiwa fedha za kutoka mwenyekiti alizungumzia. Ni kweli kwamba kwanza hakuna idara inayopata pesa asilimia 100, lakini ni lazima tuishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ninamshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais anayeshughulikia Fedha na Uchumi, anatusaidia sana na kwa wizara yetu sisi tunasema kwamba anafanyakazi zaidi ya kawaida. Kwa sababu sisi ni wa moja wa watumiaji wakubwa wa fedha ya serikali hii wizara yetu na Mhe. Dk Mwinyihaji kila tunapomuendea na shida zetu za kikazi, basi anatusaidia sana. Lakini kwa hakika fedha zetu nyingi zinatumika katika barabara, yaani mabilioni ya fedha yanatumika katika barabara. Kwa sababu hata tukipata wafadhili lakini lazima kuna mchango wa SMZ katika miradi yote na inakuwa sio fedha kidogo. Kwa hivyo, ni lazima macho yetu yanakuwa yako kwenye barabara.

Pamoja na hayo Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Leseni tunawashukuru na nina msifu sana Mkurugenzi huyu wa Idara ya Leseni, kwa sababu kabadilisha mazingira ya idara. Zamani wale waliokuwa kwenye kamati walipokwenda pale Karakana Kuu, basi kulikuwa kuna senyenge mbovu mbovu tu watu wakawa wanavamia, lakini sasa hivi tumejenga kuta na hizi ni juhudi za Mkurugenzi na timu yake, tunamshukuru sana na tunatarajia kwamba baadae jicho lake sasa ataangalia katika utafutaji wa vifaa vipya vya Karakana na kuwasomesha mafundi wetu ili waweze kusonga mbele.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ramadhan Nyonje pia alizungumzia kuhusu bandari, akazungumzia Shirika la Meli na kwamba anga na bandari ziwe mamlaka. Mhe. Mwenyekiti, mchakato unaendelea wa anga, lakini bandari hatujafika huko. Lakini anga tumeshaanza mchakato kwa ngazi ya wizara tumemaliza, tunatarajia kupeleka makatibu wakuu na BLM kwa ajili ya kupata ridhaa ya kuibadilisha Idara ya Anga kuwa kama ni Shirika au mamlaka, lakini kitu kimoja kati ya hivi tunataka kwenda nacho. Kwa hivyo, haya hata sisi wizara tunaona kwamba muda umefika wa kuifanya idara ambayo inajitegemea.

Mhe. Mwenyekiti, kuhudu gari kutengenezwa katika Karakana Kuu, hili nalo tunalifanyia kazi na tayari tumelizungumza katika ngazi ya serikali kuu na limetolewa uamuzi kuwa hali hiyo ifanyike.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu meli. Serikali inaendelea na taratibu za kutafuta meli mpya ili tuweze kuwa na usafiri wa uhakika. Kila siku tunazungumza kwamba Zanzibar ni nchi ya visiwa na ili tuwe salama ni lazima serikali iwe na mkono wake katika usafiri wa majini.

Mjumbe wa pili kuchangia alikuwa ni Mhe. Ali Suleiman Ali, yeye alitupongeza sana na akasema barabara zinakwenda vizuri na bandari zinafanyakazi vizuri. Tunamshukuru Mhe. Ali Suleiman. Pia alitaka tununuwe meli mpya kwa sababu ni muhimu. Tunakubaliana na yeye na suala hili halina ubishi.
Mhe. Salmini Awadh Salmin yeye alizungumzia mambo mawili makubwa na hili suala la kwanza alisema atatoa shilingi katika bajeti. Mhe. Mwenyekiti, bajeti haijafika sisi tunazungumzia ripoti za kamati. Tulipoanza kujenga barabara basi kazi ilikuwa kubwa lakini tuliiweza na kama tuliweza kujenga barabara, basi sina wasi wasi wowote kwamba tunaweza kujenga na hivyo vikuta vyenyewe. Lakini hatuwezi tukajenga vikuta halafu vikawa havina ubora.

Kwa hivyo, tumezungumza na kampuni ambayo sioni vibaya kuisema. Tulizungumza na kampuni ya MECO kwamba watie vile vikuta pale, na kwa sababu pia tunataka kujenga na *round about* pale Mwanakwerekwe, kwa pamoja kazi hii tutawapa wao. Katika ujenzi huo tumekubaliana kwamba watakapojenga *round about* basi tutawapeleka na wafanyakazi wetu wawili au watatu, washirikiane nao ili na wao wachote ujuzi zaidi kutoka katika kampuni ile ili baadae hizi *round about* za mjini tuweze kuzishughulikia na tuepukane na yale Mhe. Ali Denge Makame aliyozungumzia kwamba barabara nzima lakini *round about* mbovu. Kwa hivyo, hili nalo tunawahakikishia Wajumbe wa Baraza hili kwamba halitofikia kutoleana shilingi, nafikiri shilingi itatolewa kwa mambo mengine, sio kwa barabara ya Magomeni, nafikiri hili halitofikia hapo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu fedha za Benjamini Mkapa. Ni kweli kwamba fedha hizi zimekuja, lakini ziko Wizara ya Fedha na Uchumi na ni busara kwamba zikae huko hadi pale tutakapoamua tunazifanyia lini kazi hii. Waheshimiwa Wajumbe ni lazima tujuwe kwamba kila mheshimiwa hapa anahitaji barabara na uwezo wetu hatuwezi tukaenda au tukajenga barabara tano au kumi kwa pamoja, ni lazima tujenge moja tukimaliza ndio twende nyengine.

Fedha hizi za ujenzi wa barabara, kwa sababu makisio yalikuwa ni kujenga sisi wenyewe, hatukukisia kuwa waje wajenge makampuni makubwa, kilomita zenyewe 3, 4 au 7. Ukiwapa kampuni kubwa fedha zile tulizozipata kutoka SMT, basi hazitoweza kukidhi mahitaji ya ujenzi wa barabara ile. Kwa hivyo, tunaangalia nafasi ya Idara yetu ya UUB ili ile kazi wapewe wao waitekeleze kama walivyojenga ile njia ya kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Haji Mkema Haji alisema wawekezaji wanaleta meli mbovu. Mhe. Mjumbe meli mbovu haziletwi, isipokuwa meli ambazo zimekwishatumika. Wengine wanajitahidi kuleta mpaka meli mpya wenye uwezo mkubwa. Lakini hatuwezi tukafunga kamba tukasema lazima ulete meli mpya, kwa sababu tunajua hapa kwamba hata gari zilizokuwa sio mpya zinaletwa. Usafiri wa majini Zanzibar ni muhimu sana. Siku moja tukiwa hatuna meli hapa itakuwa tatizo lake ni kubwa sana na tutakosa mambo mengi sana hata uchumi wetu utadorora. Kwa hivyo, tunaangalia na sasa hivi tuna utaratibu kwamba meli kabla ya kuanza kufanya kazi basi huko inakonunuliwa maafisa wetu wanakwenda kukagua na kuridhika na ubora wake ndio inaletwa meli nchini.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Cheju Unguja Ukuu wajumbe wanasema bado na Pongwe bado. Mhe. Mwenyekiti, hili ni kweli bado. Asubuhi nilimsikia Mhe. Ame Mati Wadi akisema amebahatika sana, lakini na Mhe. Haji Mkema Haji na yeye jimbo lake amebahatika sana, ana barabara nyingi za lami. Kwa bahati nzuri hizi barabara mbili pia ni moja kati ya barabara tatu ambazo BADEA wamekubali kuzifadhili tena. Nafikiri Dk Mwinyihaji tulikuwa tunaulizana safari yetu itakuwa lini. Kuna barabara ya Miwani ya Mhe. Tafana Kassim Mzee, barabara ya Cheju aliyozungumza Mhe. Haji Mkema na barabara ya Pongwe Jumbi. Barabara hizi zote BADEA ameonesha nia ya kuzifadhili na tunatarajia kufunga naye mkataba, ili tutangaze mjenzi wa barabara hizi. Kwa hivyo, Mhe. Haji Mkema Haji bado jimbo lake litaendelea kunufaika na ninahakika kwamba kama kampeni ni barabara, basi utarudi tena hapa Barazani bila ya wasi wasi wowote *(Makofi)*.

Kuhusu Bandari lengo letu kule ndani si kuweka *parking*, isipokuwa kwa *tax* pamoja na gari za mizigo na gari za abiria tunataka zishushe na kupakia na baadaye kuondoka. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe hili tunalifanyiakazi na kama unafungiwa minyororo, basi Manispaa kidogo maana yake tunasikia Waheshimiwa Wajumbe kama saba hivi wameshafungiwa minyororo. Hivyo, tutajitahidi kuongea nao, ili suala hili waliangalie kwa umakini.

Tatizo ambalo wanawafungia minyororo watu pale ni kwamba wengine wakifika ndio wamefika, hawaondoi gari zao na mikokoteni ya shoki shoki ipo kidogo inakuwa inaleta kero. Lakini sasa tutaangalia tufanye nini na ikiwezekana tutakuja kuangalia eneo angalau Waheshimiwa muweke gari zenu kwa muda kama dakika 10-15 ili muweze kufanya shughuli zenu na kuondoka.

Halafu kuhusu *land craft*, kwamba kwa nini inataka kuwekwa pale pale nazo. Tumeamua kujenga gati ya *land craft* pale ya muda, baadae tukishapata vifaa vya kutosha kule ndani, *crane* mpya na mambo mengine tutaziondoa tutazirejesha kule kwenye gati kubwa na pale kuendelea na gati ya abiria kama kawaida. Tumeziondoa kule Forodhamchanga kwa sababu kuna uharibifu mkubwa wa mazingira kutokana na hizi *land craft* kwenda kule na mambo mengine. Kwa hivyo, tumeondoka kule na kuleta pale ambapo mnaona hivi sasa panatengenezwa kwa ajili hiyo.

Kuhusu Bungi kwamba hivi sasa imekuwa mgongo wa kasa. Mhe. Mjumbe nakuhakikishia kwamba utarejea tena kuwa mgongo wa ngisi. Kwa sababu tulikuwa na tatizo la lami kidogo siku za nyuma, lakini hivi sasa tayari tumeshapata lami na tutaika barabara na kuitengeneza pamoja na kuweka lami mpya.

Vile vile pale nadhani ile mizizi ya miembe inasababisha matatizo ya barabara kukatika mara kwa mara. Kwa mfano, tulipita na Katibu Mkuu na kuulizana hivi tunaweza kuipitisha barabara hii sehemu nyengine badala ya hapa katikati ya miembe, lakini tukaona ni moja sehemu ya utalii na barabara ile ipite katikati ya miembe. Kwa hivyo, tutaendelea kuifanyia matengenezo kila wakati. Isipokuwa wale wanaoipa udongo Mhe. Mjumbe utusaidie, kwa sababu watu wako pamoja na masheha wako unao na wala haiwezekani Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ikawakamate watu wanaiba udongo Bungi na Mhe. Mwakilishi upo, masheha na viongozi wengine wapo, serikali ipo kazini ya Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya. Kama kunaibiwa udongo basi tusaidieni ili huo udongo usiibiwe.

Mhe. Hija Hassan Hija alikuwa Mheshimiwa wa tano. Mhe. Hija na yeye alikuwa na hoja zake za msingi za barabara za Kusini Pemba nimeshazieleza. Lakini uchache wa vifaa ni kweli upo lakini utamalizika. Hili la mafuta kwamba hakuna kwenda kuchukulia kokoto jipya kwangu. Naomba basi baadae tutakwenda Pemba na anieleze kwa kina ili tuweze kulipatia ufumbuzi.

Kuhusu kuwa mkataba ulisema kwamba walipwe shilingi elfu moja za Kenya lakini wanalipwa shilingi elfu tano za Tanzania, sijui kama unasema hivyo mkataba, mkataba wenyewe umefungwa Tanzania sijui kama ukafungwe kwa fedha za Kenya nafikiri hiyo itakuwa maneno ya watu tu, kwa sababu yule msimamizi anatoka Kenya. Pengine yeye labda analipwa fedha hizo basi na wao wanaona labda walistahiki kulipwa fedha za Kenya, lakini sioni kama lina mambo makubwa sana.

Meli ya MV. Maendeleo kuwa itarudi lini, tunategemea kati kati ya April lakini haumaliziki mwezi wa April itakuwa Zanzibar.

Meli ya Serengeti haikuwa mbovu isipokuwa iliungua na hata kitu kipya kinaungua. Haikuwa mbovu mpaka siku iliyoungua. Kwa hivyo, maneno yetu hayakuwa labda kama umeilani kama ulivyosema kuwa imelanika sawa, lakini haikuwa mbovu.

Barabara ya Mgagadu kuhusu fidia. Mhe. Mwenyekiti, sisi tulivyokwenda Pemba kabla ya ujenzi wa barabara ile mimi niliagiza kwamba nyumba zote zichukuliwe kwa video, halafu zipigwe picha. Kwa sababu wakati mwengine nyumba inakuwa ishakuwa na nyufa kabisa kabla hata hatujafyeka sisi, lakini ukijenga barabara unaambiwa nyufa hii ulipopitisha *bulldozer* lako na nini. Kwa hivyo, tumezipiga picha nafikiri hakuna mtu atakayezulumiwa kupata haki yake.

Mhe. Ali Abdalla Ali alisema madereva sasa hivi tunaambiwa kwamba lazima wasomee vyuoni, lakini kuna wengine mbona wanafundishana wenyewe. Mhe. Mjumbe wale wanaofundishana wenyewe wanapewa kibali maalum na Idara ya Leseni, kwa sababu wanakuwa vyuoni lakini yale mafunzpo ya ziada mtu akenda kuomba kibali anapewa ili amsaidie mwenzake na afanikiwe.

Lakini pia *route* ya njia. Hii anayetaka au wanaotaka wanaomba kwa barua kwa Mkurugenzi na barua pia inapelekwa kwa halmashauri ya mji wenye kuhusika. Wataalamu wetu wa idara wanakuangalia wakiridhika wanaona kwamba kuna haja basi wanatoa *route.* Kwa hivyo, Mheshimiwa kama na nyinyi mna shida huko kuna eneo basi andikeni barua kwa Mkurugenzi na ataleta watu wake kukagua.

Mhe. Mjumbe wa saba alikuwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kuhusu nyumba za Pangeni bado hazijalipwa. Suala hili ni kweli na tumelipa baadhi ya fidia katika Shehia ya Mchangani, Dunga Bweni na Kilombero na hivi karibuni tunatarajia kulipa Shehia za Mbuzini, Tunduni, Mitakawani pamoja na Pangeni yenyewe. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe hili tunalo na tunaendelea na utaratibu wa kulipa nyumba zinazohusika *(Makofi).*

Kuhusu daraja la Kitope – Kinduni gari nne za kifusi nafikiri watendaji wangu wamekusikia na watakusaidia, ili mambo yaende vizuri. Kwa hivyo, tutakumbushana kazi hii iende vizuri na wewe uweze kukaa vizuri *(Makofi)*.

Madaraja ya Kaskazini Unguja. Kwa kweli hayo ni madaraja ambayo yamo kwenye mradi ambapo tumezungumza na Serikali ya Japan watusaidie kuyafanyia ukarabati. Lakini wakati tunasubiri Japan basi sisi wenyewe kama ambavyo tulivyoanza kwa barabara ya Kinazini – Bububu na haya tutaanza kuyashughulikia kila ambapo haja ya kufanya hivyo itatokezea.

Mhe. Said Ali Mbarouk alikuwa mchangiaji wa nane alizungumzia kuhusu Karakana Kuu iendelezwe, vifaa vipatikane pamoja na mafundi waendelezwe. Kwa kweli yote haya kwa Karakanu nayakubali.

Kuhusu *Zantel* kwamba imehama. Mhe. Mwenyekiti Kampuni ya *Zantel* bado haijahama, isipokuwa hivi sasa kuna mabadiliko ya uongozi na ameletwa kijana mwengine mpya ambaye anaitwa Moyo. Kwa hivyo,

huyo alikuja kujitambulisha na ametuahidi kufanya mabadiliko ya kuweza kuiboresha *Zantel* hapa Zanzibar *(Makofi)*.

Vile vile kuhusu barabara ya Wete – Konde na Wete – Gando zinakwenda sambamba. Kwa sababu ya kuanza moja kutangulia sio kama nyengine ndiyo imeachwa. Kwa kweli zote utazishughulikia, lakini tulikuwa na tatizo kidogo la kitaalamu la kubadilisha eneo la kutoa barabara ya Wete – Gando.

Nafikiri sasa wataalamu wangu, mjenzi pamoja na msimamizi wa ujenzi wameshakubaliana, kwa sababu hatukutaka kwenda na zile *cross* kubwa za kwendea Gando na tulitaka kupita katikati ya bonde halafu tunyanyue twende juu. Nadhani kazi hiyo imekubalikana na tukianza hapo basi tunaweza kwenda sambamba, ingawa ya Wete – Konde itakuwa mbele zaidi kuliko ya Wete – Gando, lakini zitakuwa zinakwenda kwa sambamba barabara zote mbili.

Mhe. Ali Denge Makame kuhusu suala la minara ni mingi ambayo inatia kizunguzungu. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tunayo Kamati Maalum ya Kuratibu, ili watu wasipate kizunguzungu *(Makofi)*.

Vile vile tunawashawishi sana wenye Kampuni za Simu washirikiane kwa kutumia minara ya pamoja. Lakini unajua katika ushindani wa kitu cha aina moja basi wanakuwa wagumu sana kutumia minara ya aina moja.

Kwa mfano, wakati mwengine mtu akiwa katika masuala ya ufadhili wa mpira, basi anaweza kukwambia kama Kampuni ya Simu inakufadhili anaweza kukwambia kwamba usivae tena nembo ya Kampuni yoyote ya Simu na unaweza kuvaa nembo ya bidhaa nyengine, lakini sio bidhaa kama ile yake yeye. Kwa hivyo, wakati mwengine wanakuwa wagumu sana kutumia mnara wa aina moja watu hawa.

Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin umetushukuru kwa matengenezo ya barabara mbili, lakini umesema imekuwa balaa kutokana na mvua za masika. Kwa hivyo, tunakuahidi kwamba tutawasiliana na wenzetu walioko huko Pemba, kwa ajili ya kutizama na kuona wafanye nini, ili kunusuru hali hiyo. Sasa baada ya kikao hiki kati au mwisho wa mwezi wa April nitakuwa Pemba, kwa yule ambaye anahitaji twende jimboni kwake basi tutakwenda, pia nitawaeleza nyote kama niko Pemba kwa muda wa siku tano au kumi na tutafanya hizo ziara za pamoja *(Makofi)*.

Vile vile wizara inunue vifaa vya uokozi baharini. Kwa kweli hilo ndilo lengo letu na uwezo utaporuhusu basi tutanunua. Pamoja na hayo tayari tumeshazungumza na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kwamba kitu gani cha kufanya na tunaendelea kuzungumza nao, ili kuona upande wetu tunafanya na wao wanakuja Bandarini kuwekeza katika shughuli za uokozi.

Mhe. Zakiya Omar Juma yeye alikuwa ni mchangiaji wa mwisho, tena ni Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ambaye ni muhimu kwa sababu anachangia sana kwenye vikao. Kwa hivyo, yeye alizungumzia umuhimu wa vikao vya kamati na wamiliki wa vyombo na mimi nakubali umuhimu huo.

Lakini nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe, wakati mnapopanga ratiba zetu za kuzunguka wizara yangu basi muzitia na ratiba za kwenda kwenye meli kabisa. Tatizo ni kwamba hamupangi kwenye ratiba na halafu baadaye kamati inani-*direct*, kwa sababu wale watu wengi hawakai Zanzibar na wanakaa Dar-es-Salaam na wengine wanakaa sehemu nyengine.

Kwa kweli wao wanapenda sana kwenye vikao vile waje wenyewe na wala wasiwakilishwe. Kwa maana hiyo, lazima wakati mnapopanga zile ratiba muingize kwenye ratiba zenu za mwanzo, ili na mimi niwaarifu mapema kwamba kutakuwa na jambo fulani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niseme kwamba ninawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote, kwa kweli baadhi ya mambo wamenifunua macho, ambayo tutayafanyiakazi kabla ya bajeti ya mwaka huu *(Makofi)*.

Nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kukushukuru wewe mwenyewe binafsi pamoja na Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ambayo inaongozwa na Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu akisaidiwa na Mhe. Hamad Masoud Hamad, ambapo kwa dharura wote leo hawapo.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja nikienda na hoja za wachangiaji nikianza na ile ya Mwenyekiti wa Kamati, ambapo yeye alipendekeza kuwe na matengenezo ya mara kwa mara ya hii *Cable* yetu ya Fumba – Tanga. Kwa hivyo, napenda kukuthibitishia Mhe. Mwenyekiti pamoja na Baraza lako hili kwamba hivi sasa kuna utaratibu wa kila wiki mafundi wanakwenda Fumba na Ras Kilomoni kwa ajili ya kuangalia *pressure* na *vacuum (Makofi)*.

Vile vile *ZECO* inao mkataba na wataalamu wetu kutoka Afrika ya Kusini, mmoja anayeshughulika na mafuta na mwengine *cable*, kila baada ya miezi mitatu wanakuja hapa kwa ajili ya kuangalia kama kuna jambo lolote linahitajika kwa lengo la kunusuru tatizo lisitokee kubwa zaidi.

Jambo jengine ambalo Mwenyekiti wa Kamati alilizungumzia juu ya suala la kuhakikisha kwamba Mji Mkongwe unaendelea kuwa hifadhi. Nafikiri juzi tumepitisha hapa mswada ule unaohusu masuala ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe. Kwa kweli mswada ule utasaidia sana kuona Mji Mkongwe unaendelea kuwa katika hifadhi na wala hautofutika *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Ali Suleiman Ali yeye zaidi alitoa pongezi kwa *ZECO* pamoja na Mamlaka ya Maji, ambapo kwa kipindi kile cha tatizo la ukosefu wa umeme waliweza kufanyakazi kubwa. Kwa upande *ZAWA* aliwashukuru sana pamoja na tatizo la umeme waliweza kufanya jitihada za kuwa na majanareta katika maeneo mbali mbali.

Kwa kweli kuhusiana na hili napenda kutoa maelezo machache, katika kipindi kile ambacho *ZAWA* ilikuwa imelazimika kutumia majanareta, kwa wastani kwa wiki walikuwa wakitumia zaidi ya shilingi milioni 56, kwa ajili ya kuendesha yale majanareta. Hali hii inaonesha ni kiasi gani serikali imejidhatiti kuona inapunguza hili tatizo *(Makofi)*.

Mhe. Salmin Awadh Salmin yeye alizungumzia juu ya suala la nyumba ambazo zilijengwa hapa Posta na watu walivunjiwa nyumba zao. Ni kweli kuna watu walivunjia nyumba zao baadhi yao walipewa fedha na wengine walipewa nyumba. Lakini wakati walipopewa walipewa pamoja na barua ikiwa ni uthibitisho wa hati kwamba wao ni wamiliki halali wa nyumba zile.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli baadhi yao wamezipoteza barua hizo kwa sababu ni muda mrefu na wamekuwa wakienda afisini. Isipokuwa mimi mwenyewe binafsi pamoja na Mhe. Mwakilishi tutahakikisha kuona kwamba wale wote wenye tatizo hilo basi moja kwa moja waje afisini kwangu saa 1:15 asubuhi wanione, ili tushirikiane kuona wanapatiwa hizo hati zao.

Jambo jengine ni kuhusu tatizo la maji katika maeneo ya Sogea, ambapo alisema kwa asilimia mia moja hawana maji. Kwa kweli tumelisikia na kutokana na uhodari wa Mhe. Salmin Awadh Salmin akiwa Mwakilishi wa Jimbo hilo, basi tutashirikiana na Mamlaka ya Maji Zanzibar, ili kuona hatua kwa hatua tatizo kubwa ni kitu gani.

Lakini ninaimani kwamba tatizo hili linaweza kumalizika baada ya Mradi wa Maji wa Awamu ya Pili kumalizika badi tatizo hili nalo linaweza kupungua kwa kiasi kikubwa.

Vile vile Mhe. Haji Mkema Haji naye alitoa pongezi kwa wenzetu hawa wa *ZECO*. Pia alishauri kwa yale maeneo ambayo hayajapata umeme, ambayo yako ya aina mbili kwa alivyokusudia nadhani, yaani kuna maeneo baada ya kurudi umeme hawana umeme kutokana na kuibiwa kwa nyaya, lakini kuna maeneo ambayo bado yakiwemo Manyami na Pongwe bado umeme haujafika, pamoja na maeneo mengine ambayo Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin ameyazungumza. Kwa hivyo, shirika litaendelea na jitihada za kuona maeneo hayo yanapatiwa umeme.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kusema jambo moja hiki kipindi cha miezi mitatu ambapo tumepata tatizo la umeme. Kwa kweli limerudisha nyuma kwa kiwango kikubwa sana, maeneo yote ambazo *ZECO* ilipanga kupeleka umeme likiwemo Jimbo la Uzini, kama vile maeneo ya Ghana, Kiboje – Mwembeshauri, Dongongwe pamoja na maeneo mengine mengi yakiwemo na yale ya Msengele *(Makofi).*

Hata hivyo, kwa kuwa hali ya umeme imerejea, basi *ZECO* itaweza kujipanga vizuri, ili kuona wananchi wote kwa ilivyo azma ya serikali kuwapatia huduma hii ya umeme.

Jambo jengine ambalo Mhe. Mjumbe ambalo amelizungumza na nafikiri watendaji wamelisikia juu ya suala la Mahakama ya Nyumba hairidhishi kabisa na wala haipendezi kama Hakimu anakaa kwenye gari. Kwa hivyo, mimi binafsi nitahakikisha kwamba taasisi inashirikiana na watendaji kuona hili liko katika hali nzuri, kwa sababu umaridadi unaficha umasikini Mhe. Mwenyekiti *(Makofi).*

Pia kwa upande wa maji Mhe. Mjumbe alizungumzia. Ni kweli kuna maeneo ambayo pamoja na jitihada za *ZAWA*, lakini bado kuna maeneo ambayo huko nyuma maji yalikuwa yakifika na hivi sasa hayafiki. Mhe. Mwenyekiti, kuna matatizo mengi inawezekana mashine zimezeeka au hata visima vyenyewe navyo sasa vimekuwa na upungufu wa maji. Lakini hivi sasa kuna maendeleo ambapo watu wamekuwa wakitumia kwa ajili ya kumwagilia katika baadhi ya maeneo ambayo mabomba yale yanapita na wala si tatizo na hayo ni maendeleo, kwa sababu maji lazima yatumike kwa matumizi ya nyumbani pamoja na mashambani. Hata hivyo, tutajitahidi kuona kwamba tatizo hili linapungua hatua kwa hatua.

Wazo lake la kuwa na Mamlaka hapa Tunguu. Nafikiri tutalichukua na wala sijambo baya na tutalifanyia kazi na tukiona linafaa basi tutalichukulia hatua, ili tuweze kufanikisha vizuri.

Kuhusu suala la upungufu wa mafuta ambao umekuwa ukitokea mara kwa mara. Zanzibar zipo kampuni nne ambazo zimepewa leseni ya kuleta mafuta hapa nazo ni hizi zifuatazo:-

1. *United Petroleum*,
2. *Zanzibar Petroleum*,
3. *GAPCO* na
4. *British Petroleum (BP)*.

British Petroleum wao wanaleta mafuta ya ndege tu.

Lakini kampuni zote hizi zinatakiwa zihakikishe kwamba wakati wote zinaleta mafuta. Kumekuwa na hoja kwamba kule Mombasa wanapata tabu ya kupakia kwa sababu kipaumbele hupewa zaidi zile meli kubwa na hilo sisi si letu.

Isipokuwa wao wahakikishe wanaleta mafuta kama wataleta kwa pakacha au ndoo ama kitu gani, lakini walete mafuta kama tulivyokubaliana na tuondoe usumbufu wa mara kwa mara, mafuta yanaadimika na matokeo yake wakati mwengine watu wananua mafuta na kuweka ndani na kusababisha maafa. Kwa hivyo, hoja hiyo si ya msingi, isipokuwa wao wahakikishe kwamba wanaleta mafuta wakati wote kama ambavyo leseni zao zinavyowaruhusu.

Jambo jengine ni kuhusu viwanja vya Matemwe. Mhe. Mwenyekiti, hili nimelisikia na wala sitaki nitoe jibu la moja kwa moja, isipokuwa tumelisikia na tutalifanyia kazi, ili kuondoa hili tatizo ambalo lipo.

Mhe. Hija Hassan Hija naye alitoa pongezi kwa *ZAWA* pamoja na *ZECO*, lakini aliwataka *ZECO* wasibweteke kwa sababu ya umeme kurudi. Kwa hivyo, napenda kumhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba *ZECO* hawajabweteka na wamejipanga vizuri.

Suala la kukosekana na umeme pale Kianga kunatokana na kuungua kwa ile *transformer*, lakini jitihada zinafanyika, ili wananchi wale wapatiwe *transformer* nyengine. Kwa kweli kuharibika kwa *transformer* ile imesababisha tatizo la maji, ambapo hivi sasa janareta ambayo ipo pale inafanyakazi na kuhakikisha angalau watu wale wanapata maji.

Kuhusu suala la Msengele. Ni kweli wananchi wa Msengele kupitia kwako napenda niwapongeze binafsi na wala hawatokunyima kura nataka nikuthibitishie kwenye Kura za Maoni watakupa. Kwa kweli wananchi wa Msengele wametoa shilingi milioni 4 zao kwa ajili ya kupelekewa umeme kule na mimi nimekwenda kijijini kule mara mbili *(Makofi)*.

Vile vile napenda kuwashukuru sana wananchi wale, kwanza kwa ukarimu wao, yaani tumekwenda pale tukala mseto kwa kuku, ndizi. Lakini kwa ridhaa yao wananchi wale wamejitolea miti yao kukatwa bure bila ya malipo, ili *line* ile ifike *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wakati nili-*contradict* na Meneja, kwa sababu wao wameshasema wakati watu wa Kilimo wameshafanya *survey* pamoja na tathmini, basi sikuona kwa nini wasite, basi niliwaambia watu wa Msengele wakate miti. Kwa hivyo, miti hiyo tayari imeshakatwa, lakini kwa bahati mbaya kama nilivyosema kwamba tatizo hili la umeme lilipotokea miezi mitatu karibu kila kitu kilisita. Kwa maana hiyo, nguvu zetu zote za kifedha zilielekea kwenye matengenezo ya *cable* yetu ya Fumba – Tanga.

Nadhani nioneshe hapa kiasi gani ambacho kimetumika kwa gharama za matengenezo ya ile *cable* Mhe. Mwenyekiti. Kwa mfano, mpaka hivi sasa fedha ambazo zimeshalipwa kwa ajili ya matengenezo pale ni shilingi mia saba na hamsini na tano milioni, laki sita na sitini eflu, mia tano na kumi na nane. Lakini bado kuna jumla ya shilingi milioni 130 kutokana na ankara ambayo ya hivi karibuni hizi bado hazijalipwa.

Sasa utaona kwa kiwango gani tulilazimika kusitisha shughuli nyengine kuelekea kufanya matengenezo ya hii *cable*. Kwa hivyo, bado nia ipo pale pale na ninawaomba wananchi wote na wala sio wa Msengele tu, isipokuwa ni wote wawe na subira, kwa kweli maeneo hayo yatapata umeme na subira huvuta kheri *(Makofi)*.
Katika suala hili la kuhakikisha kwamba *ZECO* hawakubweteka, lakini kuna Mjumbe mwengine ambaye aliuliza swali hili nafikiri Mhe. Said Ali Mbarouk pamoja na Mhe. Ali Abdalla Ali, yaani walitaka kujua hatua ambayo tumefikia kwa upande wa majanareta.

Mhe. Mwenyekiti, napenda niwahakikishie kwamba kwa kweli tumefikia hatua nzuri na hata *ZECO* wenyewe wameshaanza kujenga *base* kwa ajili ya kuweka majanareta haya na karibu nusu yake, kwa sababu haya majanareta yatakuwa kama 36, sasa kiasi vitanda 18 tayari zimeshajengwa kazi inaendelea *(Makofi)*.

Nadhani si vibaya kuwataja wale ambao wamesaidia kuhakikisha kwamba tunakuwa na umeme wa dharura, ambao kwa wakati huo utakuwa wa *Megawatt* 25. Kwa kweli wenzetu wa Norway wametuchangia dola za Kimarekani milioni 4, *SIDA* dola milioni 4.5, UK dola milioni 3 na Zanzibar imechangia dola milioni 1.5 *(Makofi)*.

Kwa hivyo, hii inaonesha kwamba *ZECO* haikulala, lakini pamoja na hayo pia inaendelea kuangalia njia nyengine zikiwemo *Wind Power, Solar Power* na mambo mengine kama haya.

Mhe. Ali Abdalla Ali yeye alitoa pongezi kwa ZAWA kwa mradi wa maji ambao unaendelea kule, ambapo utawanufaisha wananchi wa Jimbo la Mfenesini, Kitope, pamoja na Bumbwini. Kwa kweli jitihada zinaendelea, ili kuona mradi huo unamalizika haraka kwa ajili ya watu kufaidika.

Vile vile alitaka kujua suala la *cable* limefikia hatua gani kwa kupunguza muda. Ni kweli ile *cable* mpya ambayo itakuwa na uwezo wa *Megawatt* 100 ilikuwa imalizike mwaka 2013, lakini hivi sasa upo uwezekano *cable* ile ikakamilika mwaka 2012 *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, pia alitaka kujua juu ya suala la uhakiki wa hizi eka. Kwanza nia ya wananchi kuwapa eka tatu sote tunaifahamu, kwa sababu watu walikuwa ni wanyonge na kwa makusudi kabisa baada ya Mapinduzi ya Zanzibar Rais wa Kwanza aliamua kugawa ardhi kwa eka tatu kwa wanyonge, ili wazitumie kwa ajili ya kilimo. Lakini sote tunajua na wengine tumenunua humo, wengi waliopewa hizi eka wameziuza na kupoteza ule mwelekeo wa ile dhamiri.

Kwa hivyo, ni kubwa ya kufanya uhakiki na kuona kwa kiasi gani watu wamekwenda kinyume na ile dhamiri. Kwa kweli inawezekana kama tutawachukulia hatua za kisheria kwa kukiuka yale matumizi yaliyokusudiwa, basi baada ya uhakiki huu tutaweza kujua ni wangapi wamekiuka huu utaratibu na wangapi wanaendelea na huu utaratibu wa kuzitunza hizi eka kwa dhamiri iliyokusudiwa. Kwa maana hiyo, kama kuna haja ya kuwafungulia mashtaka basi tunaweza kufanya hivyo baada ya kujua nani amekiuka ile dhamiri.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk naye ametoa pongezi kwa wizara nzima kwa ujumla, yaani *ZECO* pamoja na Mamlaka ya Maji Zanzibar. Lakini alipenda kujua kama kuna wananchi wamechangia nguzo, basi *ZECO* nayo inawasadia waya. Kwa kweli utaratibu ule bado upo, isipokuwa hivi sasa nguvu za *ZECO* zimepungua kidogo na *ZECO* uwezo wake utakaporudi katika hali ya kawaida tutaendelea.

Kuhusu suala la mikopo kwa watu wetu wa vijijini, bado utaratibu wetu ule upo na zaidi tunafanya ule kwa wananchi wa vijijini ambao uwezo wao ni mdogo. Nadhani haitokuwa vyema kupeleka umeme pahala, lakini watu wakashindwa kuutumia.

Kwa hiyo, bado utaratibu ule upo na wale wateja ambapo wanapokuwa wamepata wadhamini na wengi wadhamini hawa wanakuwa ni Wawakilishi. Nafikiri Mhe. Mjumbe ujitayarishe wananchi wako watakapokuwa tayari umeme umeshafika pamoja na wewe mwenyewe utakapokuwa tayari kuwadhamini, kwa ajili ya kupatiwa umeme, basi tutaendelea na utaratibu huo.

Jambo jengine ambalo nadhani limezungumzwa karibu na Wajumbe wote na mimi sina ufafanuzi wa hili. Lakini nafikiri hizi ni dua zenu na dua njema ni nzuri juu ya Meneja wetu ambaye kwa muda mrefu amekuwa akikaimu, kwa sababu amefanya vizuri na mtu kama amefanya vizuri wajibu wake ni kutunzwa, basi watunzaji wanasikia na watafanya hivyo *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Said Ali Mbarouk naye alizungumzia kuhusu suala la meneja pamoja na majanareta ambayo tayari nimeshayatolea ufafanuzi.

Mhe. Ali Denge Makame yeye ni Mjumbe wa Kamati alikuwa na machache tu ya kuzungumza likiwemo hili la gesi. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hivi sasa wengi wetu tubadilike tutumie gesi katika masuala ya kupikia, yaani tupikie kwa kutumia majiko ya gesi ambazo zinasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira. Masuala ya risiti ni mambo ya kawaida pale kuwa na *VAT*, *Labour Charge*, yaani kuonesha ule mgawanyo mzima uliolipishwa.

Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin naye alisema kuna wananchi wa vijiji vyake wakiwemo wa Gaelamtungi kwa muda mrefu wamepeleka barua zaoo kule kwa ajili ya kwenda kupimiwa. Mhe. Mwenyekiti, inawezekana hilo limefanyika, kwa sababu pengine *ZECO* hawakwenda mpaka leo, labda niombe radhi kwa niaba yao na wala si jambo jema.

Lakini ningekuomba wewe mwenyewe binafsi na mimi mara nyingi nakuweko Pemba. Kwa hivyo, napenda sana niwashukuru baadhi ya Wajumbe wa Pemba akiwemo shahibu yangu Mhe. Ali Moh'd Bakari, yaani muda wote amekuwa akija na kupanga na baadaye tunakwenda jimbo kwake, tayari ameshaniambia tukimaliza twende tena kwa ajili ya maeneo yake angalau kufanya *survey*.

Kwa maana hiyo, Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin nakuomba wakati nitakapokuja basi uje na wala usiandike barua, isipokuwa uje unione binafsi na mimi nitachukua jitihada za kwenda kwa pamoja mimi, wewe na watendaji wa *ZECO* angalau kwenda kufanya *survey* au kuona kwa macho, yaani ile kukaa na kuzungumza na wananchi wa vijiji vya Gaelamtungi na maeneo mengine ambapo na wewe pia utapata faraja *(Makofi)*.

Mwisho kabisa Mhe. Zakiya Omar Juma ambaye yeye amezungumzia kuhusu suala la Mipango Miji na ushauri wake tunauchukua. Vile vile amezungumzia suala la maji ambalo lipo mbali na maeneo ya huku Ng'ambu, lakini hata maeneo ya Michenzani na juzi tulikwenda pamoja na kamati katika maeneo yale na jitihada zitafanywa kuona tatizo linaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya yote haya narudia tena kukushukuru wewe mwenyewe binafsi na kamati, lakini yale yote ambayo wajumbe wako wameyazungumza yote yalikuwa ni ya manufaa kwa mamlaka na wizara na tutayafanyia kazi ipasavyo. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Zakiya Omar Juma (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wajumbe wote lakini kabla ya hapoMhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na nawashukuru sana wajumbe kwa michango yao mbali mbali. Aidha, nipokee zile shukurani na pongezi nyingi ambazo kamati yetu ilipewa na tunashukuru sana kwa michango yao ambayo ni adhimu na ni ya kujenga.

Mhe. Mwenyekiti, pia niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri pamoja na watendaji wao wote kwa mashirikiano yao ya dhati wakati kamati yetu ilipokuwa tukifanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa ufafanuzi wao wa hoja mbali mbali na masuala ambayo yameulizwa na wajumbe tunawashukuru sana kwa ufafanuzi mzuri. Pia niwashukuru sana wajumbe kwa michango yao hiyo na kwa hayo machache na kulinda muda Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale ambao wanakubaliana na ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi wanyanyue mikono, wasiokubaliana. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba kuna ripoti ya Mwenyekiti wa PAC anasema anachukua nusu saa ili tukija Jumamosi tuanze kuichangia halafu tuende na Kamati ya Katiba na Utawala Bora. Mimi nafikiri sitaki kuwahoji lakini naweza kusema kwamba ni bora tufanye hivyo ili Jumamosi tuweze kupata muda mfupi wa kuweza kujadili mambo. Nafikiri tukubaliane hivyo.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, mimi nina wazo mbadala kwa kuwa Jumamosi hatuna masuala na majibu mimi ningeshauri kwamba leo tuahirishe hapa tulipofika na Jumamosi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu saa saba nina hakika tukiwa hai itakuwa mpaka Waziri Kiongozi atakuwa ameshamaliza hotuba yake.

TAARIFA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, uongozi wa michezo wa Baraza la Wawakilishi linawatangazia wajumbe kwamba wageni wetu wa michezo kutoka Arusha watawasili Zanzibar kesho saa tisa alasiri. Wajumbe watapewa ratiba ya shughuli hiyo na jengine ni kwamba siku ya Jumamosi wageni wetu watakuja ndani ya ukumbi wa Baraza kuona shughuli za Baraza kwa muda mfupi. Hilo ndilo tangazo la kwanza.

Waheshimiwa Wajumbe shughuli zetu za mkutano huu wa kumi na tisa wa Baraza la Wawakilishi bado hazijakamilika na tunakabiliwa na siku ya mapumziko kuanzia kesho ambapo ni Ijumaa Kuu. Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa utamaduni wetu katika Baraza hili ni kutokuwa na vikao vya Baraza siku ya sikukuu na siku ya mwisho wa wiki, kwa heshima kubwa basi ninamuomba Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi atoe hoja ya kuliomba Baraza likubali kukutana siku ya Jumamosi tarehe 03/04/2010 saa 3:00 asubuhi ili tuweze kumaliza shughuli zetu zilizobaki na kufunga mkutano wetu siku hiyo hiyo ya Jumamosi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu kwa kuwa shughuli zetu bado hatujamaliza na kama ulivyosema kwamba tumekabiliwa na siku za sikukuu pamoja na siku za mapumziko. Kwa hivyo, naomba kutoa hoja kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba

watukubalie tuendelee na kikao chetu siku ya Jumamosi tarehe 03/04/2010 saa 3:00 asubuhi. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyanyue mkono juu, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 1:40 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 03/04/2010)